

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Pili – Tarehe 9 Aprili, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dharura kwa Mwaka 2005/2006 (*The Annual Report and Accounts of Capital Markets and Securities Authority for the Year 2005/2006*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma kwa mwaka 2006 [*The Annual Report and Accounts of Parastatal Pension fund for the Year 2006*]

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma kwa Mwaka 2006/2007 (*The Annual Report and Accounts of the Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2006/2007*).

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

Ofisi za Wabunge Katika Jengo la Bunge

MHE. PONSIANO D. NYAMI aliuliza:-

Kwa kuwa, ofisi ni muhimu sana mahali popote pale kwa ajili ya kutekeleza majukumu kwa ufanisi na hata kutunza nyaraka muhimu:-

(a) Je, ni lini Wabunge watapewa ofisi zao katika majengo ya Ofisi za Bunge Dodoma?

(b) Je, kwa nini hakuna vyumba maalum kwa Wabunge na Mawaziri kwa ajili ya kukaribisha wageni wao?

(c) Je, kwa nini jengo lililoko upande wa mashariki mwa Ukumbi wa Bunge likipakana na Chuo cha *CBE* lisiendelezwe kwa ajili hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ofisi ni muhimu sana kwa kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuzitumia katika kutekeleza majukumu yao ya uwakilishi wa wananchi kwa ufanisi zaidi. Azma ya kuwapatia ofisi Waheshimiwa Wabunge katika majengo ya Bunge hapa Dodoma ipo na kwa kuanzia, tayari Wenyeviti wa Kamati, pamoja na Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge, wameshapatiwa ofisi ndani ya Jengo la Utawala.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa vyumba katika majengo ya Bunge tuliyonayo, imekuwa ni vigumu kutenga ofisi kwa kila Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, katika Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, Ofisi ya Bunge inatarajia kujenga majengo yatakayokidhi mahitaji mbalimbali kwa Waheshimiwa Wabunge, ikiwa ni pamoja na kuwapatia ofisi na vyumba maalumu kwa ajili ya kuwawezesha Mawaziri na Wabunge kukutana na wageni wao.

(c) Mheshimiwa Spika, jengo lililoko upande wa Mashariki karibu na Chuo cha *CBE* Dodoma ni mojawapo ya majengo yatakayotumika hapo baadaye. Mpango huu wa miaka mitano, unatarajiwa kukamilika kabla ya mwaka 2011. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge, avute subira wakati jitihada za kutafuta rasilimali, pamoja na kutekeleza madi huo zinafanyika.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, wakati Bunge hili linaanza, Mheshimiwa Spika alitoa ahadi kwa Wabunge kwamba, katika jengo hili hili upande wa chini ya ukumbi huu, vitatengenezwa vyumba kwa ajili ya Ofisi za Wabunge. Je, kwa kuanzia isingekuwa ni vizuri vikatengenezwa angalau vyumba 26 kwa maana ya Mikoa 26 ili Wabunge wote waweze kuwa na Ofisi yao kwa maana ya mkoa; je, hili haliwezekani?

La pili, kwa vile mara nyingi Serikali huwa inahidi iwe kwenye Majimbo au hata hapa Bungeni na suala hilo huwa ni la kuahidiwa wakati wote; ni lini Serikali itasema ukweli bila maneno ya kubembeleza au kuwapa ahadi Wabunge ambazo hazitekelezeki; je, hiyo siyo sifa mbaya kwa Serikali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kuhusu eneo lililopo chini ya Ukumbi huu; ikumbukwe kwamba, eneo hili lilikuwa limetengwa kwa ajili ya kuegesha magari, baadaye wazo hili lilipobadilishwa, tulifikiria kwamba, tungepata ofisi lakini kutokana na ushauri wa kitaalamu, haikuwezekana kufanya *partition* katika eneo hilo na kama inavyojulikana sasa hivi tunaitumia kama *canteen*. Hata hivyo, azma ya kuwa na Ofisi za Wabunge ipo na nimesema kuna mpango kabambe wa Maendeleo wa Bunge kati ya leo na 2011 na katika mpango huu Waheshimiwa Wabunge watapewa ofisi.

Pili, ahadi za Serikali kuhusu Ofisi za Wabunge katika majimbo yao ni ahadi za kweli tatizo ni fedha. Wabunge ndiyo wanaopitisha bajeti na watakumbuka katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, tulipitisha shilingi bilioni moja na hadi sasa zimekwisha tolewa shilingi milioni 165, ninaamini zinagawiwa kwa majimbo yasiyopungua sita. Kwa hiyo, hadi ifikapo Juni, yaani mwisho wa mwaka wa fedha, inatarajiwa kwamba, fedha hizi zote shilingi bilioni moja zitakuwa zimetoka na zitakuwa zimegawiwa katika majimbo mbalimbali, vivyo hivyo katika mwaka ujao wa fedha na mwaka mwingine hadi zoezi zima la kuwapatia Wabunge ofisi katika majimbo yao litakapokamilika.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, katika mojawapo ya vikao vya Bunge hili, tuliarifiwa kwamba, Ofisi ya Bunge imepewa jengo lililokuwa Ofisi za *Tanganyia Motors* ili iweze kulitumia; sasa je, Bunge liliahidiwa kwamba ile ilikuwa ni kwa ajili ya mazoezi ya Wabunge kulinda afya zao; na je, hili limefikia wapi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Benson M. Mpesya, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo: Kwanza, tukumbuke kwamba, jengo hili lina mgogoro na mgogoro huo unashughulikiwa sasa hivi na utakapotatuliwa jengo hilo litatengwa kwa matumizi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na matumizi ya mazoezi kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge, *canteen* ndogo, maktaba ndogo na pia kuna sehemu za juu kutakuwa na Ofisi za Wabunge na Mawaziri.

SPIKA: Tunaendelea, kabla sijamwita Mbunge anayeuliza swali linalofuata, ninapenda kutambua na mtambue kwamba, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, kwa sasa ni Kaimu Kiongozi wa Upinzani. (*Makofi*)

Baada ya maswali, nitatoa tamko kuhusu kuondoka kwa wenzetu katika Ukumbi huu na maana yake kwa mujibu wa Kanuni. Basi sasa ninamwita Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, aulize swali lake.

Na. 17

Mali/Madeni na Vyanzo vya Mali za Viongozi wa Juu

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 2002, Sura Na 368 inatamka kwamba, kila Kiongozi wa Serikali wa ngazi ya juu, kuorodhesha madeni, vyanzo vya mali zake alivyozipata kila mwaka:-

(a) Je, ni Viongozi wangapi waliopatikana na udanganyifu wa mali walizonazo na ni hatua zipi zimechukuliwa dhidi yao tangu Sheria hiyo ianze kutumika?

(b) Je, ni Sheria ipi ya Maadili inayowabana wenye *NGOs, CBOs* na kadhalika, ambao hutumia vibaya misaada ya wahisani kwa kujilimbikizia mali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, ninapenda kutoa maelezo machache ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inasimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995. Katika Sheria hiyo, Kifungu 4(1), kimeorodhesha Viongozi wanaowajibika kutoa Tamko la Rasilimali na Madeni yao kila mwaka. Orodha hiyo iliyoreshwa kwa Tangazo la Serikali Na. 209 la tarehe 22 Julai, 2005, kwa kuongeza idadi ya Viongozi, ambao hapo awali hawakuwepo kwenye Sheria hiyo, kwa mfano, Wasaidizi Wakuu wa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi wa Wizara, Wakurugenzi Wasaidizi wa Wizara na Wakuu wa Mashirika hayo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni Viongozi waliotajwa katika Sheria hii tu ndio ambao wanawajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na wala siyo kila Kiongozi wa Serikali wa ngazi ya juu. Viongozi wengine ambao hawakutajwa na Sheria hii, Maadili yao husimamiwa na vyombo vingine vinavyosimamia ajira na nidhamu ya Viongozi hao. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni moja ya Mamlaka zinazosimamia maadili ya Viongozi hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, hupitia orodha ya mali na madeni ya Viongozi, inayowasilishwa kila mwaka na viongozi hao kwa Kamishna na kufanya mlinganisho (*Verification*) wa mali na madeni yaliyotamkwa na hali halisi ya mali na madeni hayo. Aidha, Sekretarieti hupokea malalamiko kutoka kwa raia wema, kuhusu rasilimali za baadhi ya Viongozi wa umma na kufanya uchunguzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, kuhusu uhalali wa mali hizo. Tuhuma zinazoelekea kuwa za rushwa, huwasilishwa katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, yaani TAKUKURU. Aidha, malalamiko mengi yanayopokelewa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, hayahusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, hivyo kwa kawaida hupelekwa kwenye Mamlaka zinazohusika, kwa ufumbuzi wa malalamiko hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tuhuma za ukiukaji wa maadili, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, huzifanyia uchunguzi wa awali na kama ikithibitika kuwa kuna dalili za ukweli, huwasilishwa kwenye Baraza la Maadili ili zifanyiwe uchunguzi wa kina. Baraza linapaswa kufanya uchunguzi wa kina na kumshauri Kamishna hatua za kuchukua. Hadi sasa hakuna Kiongozi aliyepatikana na udanganyifu wa mali alizonazo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Na. 13 ya 1995, haihusu viongozi wa vyombo visivyo vya Kiserikali, yaani *NGOs, CBOs* na kadhalika. Mamlaka nyingine chini ya Sheria mbalimbali, zinazohusika na usimamizi wa taasisi hizo, ndiyo zinazoshughulikia maadili. Kwa mfano, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, husimamiwa chini ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002 (*The Non-Governmental Organizations Act No. 24 of 2002*).

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake kutokana na swali la msingi, lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, ameelezea hapa kuhusu Viongozi mbalimbali na akagusia pia kwamba, Sheria ina tofauti kwa viongozi wa juu. Swali langu lipo hapa, hivi hawa Marais wetu wanajaza *forms* zao mwezi Desemba kama sisi; na pale anapostaafu, akijulikana kwamba alichojaza si sahihi ni hatua gani zinachukuliwa dhidi yake?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Sheria, anawajibika kujaza *forms* hizo na hata Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na kadhalika. Hadi sasa, hakuna lalamiko lolote ambalo

limefikishwa kwenye Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, likidai kwamba kiongozi yeyote ambaye amemaliza muda wake, hajaorodhesha mali baada ya kumaliza muda wake wa miaka mitano.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Sheria hii inamtaka Kiongozi kuorodhesha mali pale anapoingia madarakani na siyo pale anapoondoka; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, Viongozi wetu hawajilimbikizii mali pale wanapoona wanakaribia kufikia mwisho wa madaraka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sussan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria inatamka kwamba, kila kiongozi muhusika, anatakiwa ajaze *form* hii kila ifikapo tarehe 31 Desemba, hii ni pamoja na wale ambao wanamaliza muhula wao wa kazi. Ninapenda kusisitiza kwamba, kiasi cha shilingi elfu moja kinahitajika ili upate nafasi ya kuhakiki *forms* hizi ambazo ziko katika Ofisi ya Kamishna wa Maadili ya Viongozi wa Umma.

SPIKA: Sasa anayeuliza swali linalofuata simwoni ndani ya ukumbi ni Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi, kwa niaba yake Mheshimiwa William H. Shellukindo atauliza.

Na. 18

Kibali cha Kujenga Barabara ya Mbaramo – Mlalo

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.N.Y. MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI) aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikwisha tenga fedha ili kusaidia nguvu za wananchi kujenga Barabara ya Mbaramo hadi Mlalo, lakini utekelezaji ukakwamishwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa madai kuwa Barabara hiyo ingeharibu vyanzo vya maji katika msitu wa Shangayu; je, Wizara imekamilisha utafiti wake ili kibali hicho kitolewe sasa?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, ninaomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Ninaomba kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, ilikusudia kujenga Barabara ya kutoka Mbaramo hadi Mlalo kupasua msitu wa Shagayu, yenye urefu wa km 45. Serikali kupitia Mfuko

wa Barabara, ilitenga kiasi cha Sh. 115,000,000 katika mwaka wa fedha 2004/2005, pia mwaka 2005/2006, Serikali ilitenga Sh. 66,000,000 hivyo, kufanya jumla ya Sh. 181,000,000 ili kusaidia nguvu za wananchi kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, iliomba kibali cha kupitisha barabara kwenye Msitu wa Shagayu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii; kwa barua Kumb. Na. LDC/R.12/0302, Vol.II/31 ya tarehe 12 Agosti, 2005. Wizara ya Maliasili na Utalii, ilijibu kwa barua yenye Kumb. Na. JA.166/486/01/86) ya tarehe 30 Januari, 2006, ambayo ilikataa kutoa kibali cha kupitisha barabara hiyo katika hifadhi na kushauri kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa athari ya mazingira (*Environmental Impact Assessment*).

Mheshimiwa Spika, kama inavyoeleweka, upembuzi yakinifu hugharimu kiasi kikubwa cha fedha. Katika mwaka 2004/2005, makisio ya kufanya utafiti huo ilikuwa shilingi milioni 60, hivyo kwa sasa ni wazi kuwa gharama hizo zitakuwa zimepanda sana. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto hadi sasa haijafanikiwa kupata fedha za kutosha za kuiwezesha kugharamia upembuzi yakinifu wa athari ya mazingira. Hata hivyo, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo, ziliombewa kibali ili ziweze kutumika katika matengenezo ya barabara zifuatazo: Barabara ya Mwangoi – Mlalo km 5 kwa kiasi cha Sh. 75,000,000; Barabara ya Mlalo – Baghai km 7.4 kwa kiasi cha Sh. 40,000,000, kutoka Baghai hadi Mbaramo, ndilo eneo la msitu lilioombewa kibali km 37.6 + 7.4 = km 45; na Barabara ya Mnazi – Mbaramo km 5, kwa kiasi cha Sh. 66,000,000. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, iliona ni busara fedha hizo zitumike katika matengenezo ya Barabara nilizozitaja hapo juu, kwa vile fedha hizo zingeendelea kukaa na kupoteza thamani yake, wakati Barabara nyingine zilikuwa na matatizo kama haya.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali kwa ujumla, imeweka mkazo mkubwa katika suala zima la kulinda mazingira ya nchi yetu. Hivyo, ninapenda kuishauri Halmashauri ya Lushoto kuwa, kama bado inaona umuhimu wa kutengeneza Barabara hiyo, watoe maamuzi ya kutenga fedha za kutosha wakishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili utafiti wa athari ya mazingira ufanyike kama ilivyoshauriwa na Wizara ya Maliasili.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; atakubaliana na mimi kwamba, Wilaya ya Lushoto imejaa misitu kwa hiyo mtazamo wa kuleta maendeleo uzingatie kwamba kuna maeneo ambayo huwezi kufika bila kupita kwenye misitu; kwa mfano, barabara inayotoka Lushoto kwenda Mtai inapita msitu wa Shume; barabara inayotoka Bumbuli kwenda Mgwashi inapita kwenye Msitu wa Mazumbai na sehemu zote hizo zina mito; barabara zimetengenezwa, madaraja yapo na hakuna uharibu wowote wa mazingira; je, hii si kuchelewesha maendeleo ya watu waliopo Kata ya Mbaramo?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa William H. Shellukindo, kama ifuatavyo:-

Ninapenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kweli Wilaya ya Lushoto imezungukwa na misitu, pamoja na milima na barabara zao nyingi zinapitia kwenye misitu hiyo. Ninaomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, inabidi tufuate Sheria za Mazingira, kama barabara italeta athari kubwa kwa mazingira yetu pia haitakuwa na maana kwa Serikali. Kama nilivyosema kwamba, kwa kuwa barabara hii ni muhimu, ikijengwa kwa kupitishwa katika msitu huu, itakuwa imepunguza urefu wa barabara hii. Ndiyo maana nimesema kwamba, Wilaya ya Lushoto tukishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, tuone ni uwezekano gani unaweza ukafanyika ili iweze kutengenezwa barabara hii kwa ajili ya Wakazi wa Vijiji vya Mbaramo, pamoja na vijiji vingine vinavyoizunguka Kata ya Mlalo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunahamia sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa sababu swali lililokuwa liulizwe na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambile, yeye ni mmoja wa wale walioondoka humu ndani ya Ukumbi, kwa hiyo, litajibiwa kwa maandishi na Waziri kwa kulifikisha kwa Katibu.

Sasa ni zamu ya Wizara ya Afya swali linaulizwa na Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mbunge wa Ilala.

Na. 20

Hitaji la Mashine ya X-Ray Hospitali ya Ilala

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU aliuliza:-

Kwa kuwa, *x-ray* kwenye hospitali zote za Wilaya ya Ilala, Kinondoni na Temeke zimepitwa na wakati na uwezo wake ni mdogo; na kwa kuwa Serikali katika mkutano wake wa Aprili, 2007 iliahidi kuleta *x-ray* mpya lakini haikuwekwa katika bajeti ya mwaka 2007: Je, Serikali inatoa tamko gani mwaka huu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, ninaomba nitoe maelezo mafupi ya utungulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi, imekamilisha Mradi wa Kuboresha Huduma za Uchunguzi wa magonjwa nchini, kwa

kuzipatia hospitali zote Tanzania Bara, mashine za *x-ray*, *ultra sound*, vifaa vya upasuaji, vifaa vya kutakasia nguo na baadhi ya hospitali kupatiwa mifumo mizuri ya umeme na maji. Kufuatia kukamilika kwa Mradi huo, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi, imefanya upembuzi yakinifu ili kujua mahitaji halisi ya hospitali zote za wilaya mpya hapa nchini. Serikali ya Uholanzi, imekubali kuendeleza Mradi huu wa Kuboresha Huduma za Uchunguzi nchini kwa kuchangia asilimia 50 ya gharama ya Mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2008/2009 hadi 2009/2010, kwa kuzipatia hospitali zote za wilaya mpya, vifaa vya uchunguzi, pamoja na kurekebisha vyumba vya kutolea huduma za *x-ray* ili vikidhi masharti ya usalama wa mionzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, mashine za *x-ray* za Hospitali za Manispaa za Dar es Salaam, zimepitwa na wakati na uwezo wa kufanya kazi ni mdogo sana, hasa ikilinganishwa na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika Manispaa hizo. Kwa kuzingatia hilo, imeamuliwa kuwa hospitali zote za Manispaa za Dar es Salaam, zifaidike na Mradi nilioutaja katika maelezo yangu ya utangulizi. Aidha, kwa kuzingatia ukubwa wa idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika hospitali hizo, kila hospitali itapatiwa mashine za *x-ray* mbili, kama ilivyo kwa hospitali za mikoza.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia fedha zilizobaki katika mradi wa awamu ya kwanza, tayari Wizara yangu imekwishafanya utaratibu wa manunuzi wa mashine chache za *x-ray* na inatarajia kuwa, mashine hizo zitawasilishwa nchini katika kipindi cha miezi sita ijayo kutoka Uholanzi. Ninaomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Mbunge lako Tukufu kuwa, katika Jiji la Dar es Salaam, Hospitali ya Amana, ndiyo itakayokuwa ya kwanza kupatiwa mashine hizo, ikifuatiwa na hospitali za Temeke na Mwananyamala. Aidha, Hospitali za Wilaya Mpya zitakazoanza kupatiwa mashine za *x-ray* ni Chato, Mkuranga na Tandahimba. Serikali itaendelea kutoa mashine hizo kwa hospitali zote za Wilaya Mpya kulingana na uwezo wa bajeti ya Serikali na ushiriki wa mdau wetu, yaani Serikali ya Uholanzi.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na ninamshukuru vilevile kwa kutambua Jiji la Dar es Salaam linavyopokea wagonjwa wengi. Dawa ni pamoja na huduma, ninasikitika kusema toka Julai, 2007 mpaka hii leo, Serikali imegharamia dawa katika Hospitali ya Amana kwa Sh. 56m tu. Julai mpaka mwezi wa Desemba, tumehudumia wagonjwa laki mbili katika Hospitali ya Amana. Je, Serikali inategemea miujiza ipi tuifanye kwa kuhudumia wagonjwa hawa bila kutupatia pesa stahiki ambazo tunatakiwa tuzipate?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ninapenda kumtangazia Mheshimiwa Waziri kwamba, tokea Jumamosi mpaka jana, tumepokea wajawazito mia nne katika Hospitali ya Amana na wote hawa wanategemea kujifungua kwa usalama kwa kutegemea dawa hizi hizi; je, Serikali ina tamko gani kuhusu tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, huduma bora zitakwenda vizuri kama kutakuwa na dawa za kutosha na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, amepata Sh. 56m tangu Julai mpaka Desemba. Ninachoweza kusema, ninaomba nilifuatilie swala hili halafu nitampa majibu kabla hatujamaliza kikao hiki na nitamwandikia kwa maandishi.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa kushirikiana na Serikali Kuu, imeweza kuanzisha hospitali ndogo pale Vijibweni, lakini hospitali hiyo bado haijaitimia vizuri kuwa na vifaa kama hivi ambavyo Mheshimiwa Mussa Zungu ameuliza katika swali lake; je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia hospitali ndogo ya Vijibweni, vifaa vya kisasa ili kukidhi haja iliyokusudiwa ya kuipunguzia mzungu Hospitali ya Temeke?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza katika jibu langu la msingi ni kwamba, Serikali itatoa vifaa kulingana na uwezo. Hospitali ya Vijibweni, ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Mbunge, vifaa ambavyo inahitaji kwanza, Halmashauri inahitajika kununua vifaa, lakini kama anazungumzia swala la *Ultra Sound* na *X-rays* ambavyo tumevizungumzia kwenye swali la msingi ni kwamba, tumesema tutatoa kwanza katika hospitali, halafu hospitali ndogo zitakuja kupatiwa huko baadaye kama ikiwezekana na vifaa hivi vikiwa vimetosheleza katika Wilaya husika tulizozisema.

Na. 21

**Ahadi ya Kutengeneza Barabara ya Pugu - Vikumburu
kwa Kiwango cha Lami**

MHE. ATHUMANI S. JANGUO aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo tarehe 8 Desemba, 2007 Wananchi wa Kisarawe walihidhiwa na Mheshimiwa Rais kuwa matatizo yao ya maji na barabara yatatatuliwa na Serikali na hasa barabara ya Pugu hadi Vikumburu kwamba ingetengenezwa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa hadi hivi sasa ahadi hiyo haijatekelezwa:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi hiyo?

(b) Kwa kuwa wakati wa kutayarisha bajeti ya mwaka 2008/2009 ni sasa; je, Serikali inaweza kuwaeleza Wananchi wa Kisarawe wategeme nini katika bajeti hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kuimarisha, kujenga na kuifanyia matengenezo barabara ya Pugu – Vikumburu, yenye urefu wa kilometa 95 kwa viwango mbalimbali kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais kama ifuatavyo:-

Kilometa 6.2 kutoka Pugu hadi Kisarawe, zimeshajengwa kwa kiwango cha lami. Kazi hiyo ilianza mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2006/2007. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilipanga kutumia kiasi cha shilingi milioni 584 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 334 zimetumika kugharamia matengenezo yafuatayo: Matengenezo ya kawaida, kilometa 60 kutoka Pugu hadi Maneromango; matengenezo ya muda maalum, kilometa 2.5 kutoka Kazimzumbwi hadi Mpuyani; matengenezo ya sehemu korofi eneo la Bukela, Kurui, Mlima Mkunani na Mlima Vikumburu; na matengenezo ya dharura kutoka Maneromango hadi Chole. Matengenezo hayo yatawezesha maeneo yaliyotajwa kupitika wakati wote. Aidha, ujenzi wa barabara kutoka Yombo – Vikumburu, jumla ya kilometa kumi kwa kiwango cha changarawe, utafanyika kwa gharama ya shilingi milioni 180. Vilevile kazi za matengenezo ya kawaida kilometa 30 na matengenezo maalum kilometa tano, yatafanyika kwa gharama ya shilingi milioni 70. Zabuni kwa ajili ya kazi hizi imekwishatangazwa na kazi inatarajiwa kukamilika Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, kufuatia juhudi hizi, kwa sasa barabara hii inapitika vizuri. Kwa sasa Serikali haina uwezo wa kujenga barabara yote kutoka Kisarawe – Vikumburu kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha barabara hii katika mwaka ujao wa fedha, kuhakikisha kuwa inaendelea kupitika katika majira yote ya mwaka.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo hayaridhishi sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda kumkumbusha na kumwuliza; je, anafahamu kwamba, huo utengenezaji wa lami wa kilomita 6.2 ulikuwa kabla ya ahadi ya Rais, kwa hiyo, kulijibu swali hili kwa namna hiyo ni kutaka kuwababaisa Wananchi wa Kisarawe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba katika ahadi ya Rais kulikuwa na ahadi ya kuiendeleza barabara hiyo mpaka kule Mtanza, Wilaya ya Rufiji; je, Serikali hivi sasa inafanya juhudi gani kuhakikisha kwamba, Wilaya ya Kisarawe na Rufiji zinaunganishwa?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Athumani Janguo liliuliza barabara ya Pugu hadi Vikumburu na kwa hiyo jibu letu ilibidi tuanzie Pugu kama ambavyo aliuliza na kwa maana hiyo ujenzi wa kilomita 6.2 kuanzia Pugu hadi Kisarawe ilibidi tujibu. Hata hivyo ni kweli Rais aliahidi kwamba, barabara hii yote mpaka Vikumburu itaimarishwa na juhudi ambazo tunazifanya ni kuimarisha. Nilichosema ni kwamba, kwa kiwango cha lami kwa barabara yote, kwa sasa Serikali haina fedha, lakini itahakikisha kwamba barabara hii inapitika wakati wote wa mwaka.

Kuhusu suala lake la kuunganisha Wilaya ya Kisarawe na Rufiji, juhudi zitafanyika katika mwaka ujao wa fedha, kwa kutumia fedha za *Road Toll* ili tuone namna ya kuunganisha barabara hiyo ili iweze kuimarika na Wilaya mbili hizi ziweze kuunganika.

Na. 22

Matumizi ya Lugha ya Kiswahili

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN aliuliza:-

Kwa kuwa Bara la Afrika linachukua hatua za makusudi ili liweze kutumia Lugha ya Kiswahili kwa lengo la kusaidia kuleta maendeleo ya kiuchumi (kibiashara), kijamii na hata kisiasa:-

(a) Je, kwa nini Bunge la Afrika Mashariki halitumii Lugha ya Kiswahili katika shughuli zake badala yake linatumia Lugha ya Kiingereza?

(b) Je, nchi yetu ya Tanzania inafanya jitihada gani za makusudi kuliwezesha Bunge la Afrika Mashariki liweze kutumia Lugha ya Kiswahili badala ya Kiingereza?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bunge la Afrika Mashariki, linafanya kazi zake kwa kuzingatia yale yaliyoelekezwa ndani ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kifungu Na. 137 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kimeainisha kuwa, Lugha ya Kiingereza ndiyo lugha rasmi itakayotumika katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kwamba, Lugha ya Kiswahili imeelekezwa kama lugha ya mawasiliano (*lingua franca*). Jitihada bado zinaendelea ili kukifanya Kiswahili kiwe moja ya lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b) Mheshimiwa Spika, juhudi za kuendeleza Lugha ya Kiswahili, zimefikia hatua nzuri katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kutokana na kusainiwa kwa Itifaki ya Kamisheni ya Kiswahili. Mojawapo ya lengo la kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ni kutambua na kuendeleza Lugha ya Kiswahili kutokana na mahusiano ya karibu, yaliyojengeka kwa muda mrefu kati ya Wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tanzania pekee ndio imeomba Makao Makuu ya Kamisheni hii yawe Zanzibar. Hivyo basi, Tanzania tunalo jukumu kubwa la kuhamasisha utekelezaji, pamoja na kujenga uwezo kupitia sekta husika ili tuweze kutoa walimu wa kutosha wa Lugha ya

Kiswahili kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimaye kukuza Kiswahili ili kiweze kutumika katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Spika, inanisikitisha kwamba, Bunge la Afrika linazungumza Kiswahili na sisi tunakataa kuzungumza lugha hiyo na bahati nzuri chimbuko la Kiswahili ni Afrika Mashariki. Je, Waziri haoni kwamba, kutozungumza Kiswahili katika Bunge la Afrika Mashariki ni udhaifu wa aina fulani na unahitaji marekebisho haraka? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, hatua mbalimbali zinachukuliwa kwa nia ya kukifanya Kiswahili nacho kiwe lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kutokana na Mkataba wa Afrika Mashariki, mambo haya lazima yafuate hatua zote kwa kuhusisha nchi wanachama kufikia hatua hizo. Hata hivyo, kuhusu AU kutumia Kiswahili, lazima Mheshimiwa Hoogan aelewe kwamba, AU ilikuja mwanzo, suala hili lilianza zamani katika Umoja wa Afrika na ndiyo maana tukafikia sasa kuzungumza Kiswahili katika Bunge la Afrika. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jitihada zinafanywa ili hatimaye na sisi tuweze kuzungumza Kiswahili katika Bunge letu.

Na. 23

Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI aliuliza:-

Kwa kuwa, sababu mojawapo inayodumaza sekta ya kilimo kwa miaka mingi ni uwekezaji mdogo wa rasilimali muhimu kwenye sekta hiyo ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu:-

(a) Je, tangu awamu ya pili ya MKUKUTA kuanza mwaka 2005/2006 Serikali na wabia mbalimbali wa maendeleo wamewekeza rasilimali (fedha) kiasi gani kwenye sekta hiyo kila mwaka Kimkoa?

(b) Je, ni miradi mingapi iliyonufaika kama *sub-sector* na wawekezaji hao yaani kilimo cha mazao, usindikaji wa mazao na masoko ya ndani na nje kwa bidhaa hizo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, ninapenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Uwekezaji katika kilimo unahitaji fedha nyingi pia unakwamishwa na majanga mbalimbali yanayotabirika na yasiyotabirika. Aidha, hakuna utaratibu maalum wa kutoa mikopo kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo. Mikopo inayotolewa siyo ya kusaidia

wawekezaji kwa sababu ni mikopo ya muda mfupi na riba yake ni kubwa. Kutokana na sababu hizi, ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika kilimo umekuwa ni mdogo. Kwa ujumla, uwekezaji katika kilimo kuanzia mwaka 1990 hadi 2007, ulikuwa ni asilimia sita tu ya uwekezaji wa jumla, ukilinganisha na asilimia 23 na 17 katika sekta za madini na ujenzi. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya kilimo mwaka hadi mwaka, kwa mfano, mwaka 2005/2006 asilimia 5.78 (shilingi bilioni 233.3) ya bajeti yote ya Serikali ilielekezwa kwenye kilimo, ikilinganishwa na asilimia 4.71 (shilingi bilioni 157.7) mwaka 2004/2005.

Mwaka 2006/2007 asilimia 5.78 (shilingi bilioni 276.6) na mwaka 2007/2008 asilimia 6.1 (shilingi bilioni 375.4). Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme – ASDP*), ambayo inatekeleza malengo ya Ilani ya CCM na MKUKUTA, imewezesha kiwango cha rasilimali kuongezeka katika kilimo. Asilimia 75 ya rasilimali za Serikali na Washirika wa Maendeleo, zinawekezwa kwenye ngazi ya Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Programme – DADPs*) na asilimia 25 kwenye ngazi ya Taifa kupitia mipango ya Wizara katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2007/2008, Serikali na Wabia wa Maendeleo, wamewekeza kwenye sekta ya kilimo kama ifuatavyo: Mwaka 2005/2006 shilingi bilioni 4.4, mwaka 2006/2007 shilingi bilioni 14.0 na mwaka 2007/2008 shilingi bilioni 103.2 zimepangwa kuwekezwa. Mchanganuo wa uwekezaji kimkoa umetolewa ambao unaonyesha kuongezeka kwa fedha zinazopelekwa katika mikoa. Kwa mfano, kwa Mkoa wa Mara, fedha zilizopelekwa zilikuwa shilingi milioni 219.0 mwaka 2005/2006, shilingi milioni 519.4 mwaka 2006/2007 na shilingi bilioni 2.3 mwaka 2007/2008.

(b) Mheshimiwa Spika, miradi inayotekelezwa ni ile inayoibuliwa na wananchi chini ya *DADPs*. Miradi hii ni mingi na inatofautiana kati ya Wilaya na Wilaya na Kijiji na Kijiji, kutegemea na vipaumbele vyao. Aidha, maeneo makuu yanayopewa kipaumbele katika uibuaji wa miradi ni haya yafuatayo: Uwekezaji katika miradi ya kuendeleza kilimo ambayo inahusisha miradi ya uzalishaji, ujenzi wa miundombinu kama vile umwagiliaji, masoko na barabara za Vijijini; uwekezaji katika uboreshaji wa huduma za kilimo kama vile huduma za ugani utafiti na mafunzo; na uwekezaji katika kujenga uwezo wa utekelezaji wa mipango kwa watendaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, miradi yote inayoibuliwa na kutekeleza chini ya maeneo haya, inalenga katika kongeza tija, uzalishaji, kipato cha mkulima na kuboresha usalama wa chakula. Tunazishauri Halmashauri kuendelea kuwahamasisha na kuwasaidia wakulima kuibua miradi, kupanga na kutekeleza miradi ili wakulima hao wanufaike zaidi na rasilimali zinazotolewa na Serikali.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ninataka kujua Serikali ina mikakati gani katika kuanzisha miradi ya kuhifadhi chakula kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini?

Pili, je, ni sababu zipi zinazopelekea mabonde yote nchini kwa mfano, Bonde la Mto Mara yasiendelezwe kwa shughuli za kilimo?

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Ningeomba *Technical Division*, wanaouliza maswali ya nyongeza hawaonyeshwi kabisa katika *screen* sijui kuna nini leo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, mikakati ya kuhifadhi chakula inanzia kwa mkulima mwenyewe; mkulima anapolima lazima ajiwekee akiba. Serikali inaweka akiba ya chakula kwenye *SGR* yake ambayo ipo kwa mujibu wa sheria kwamba, haiwezi kuhifadhi zaidi ya tani laki moja na elfu hamsini na chakula hiki ni kwa ajili ya dharura kwa miezi mitatu, wakati Serikali inajipanga kuagiza chakula kutoka nje. Kwa hiyo, kila mkulima ahakikishe anajiwekea chakula cha kutosha kumfikisha msimu unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bonde la Mto Mara, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri za Mkoa wake, wakae na kushirikiana na wananchi kuweza kuibua miradi ya kilimo ambayo itawezesha kutumia fedha za *DADPs* ama *ASDP* ili kuweza kutumia bonde hili kwa umwagiliaji na shughuli nyingine za kilimo.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Kwa kuwa wakulima wengi vijijini wanakuwa hawana sifa za kukopa katika Mfuko wa Pembejeo; je, kwa nini Serikali isiruhusu Halmashauri za Wilaya kukopa matrekta katika Mfuko wa Pembejeo na kisha Halmashauri kuwakopesha wakulima katika vikundi vidogo vidogo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Serikali inaruhusu Halmashauri ziweze kudhamini wakopeshwaji. Sasa kama Halmashauri zenyewe zitajiingiza kwenye shughuli za kukopa kwenye Mfuko wa Pembejeo, Serikali haina kipingamizi, inaweza kufanya hivyo lakini jambo zuri ni pale ambapo Halmashauri zitadhamini wakopaji, pamoja na vikundi vidogo vidogo vya *SACCOS* na Vyama vya Ushirika, kusudi waweze kukopa kwenye Mfuko wa Pembejeo na waweze kurudisha. Hii ni kwa sababu itakavyojiingiza tena katika biashara hiyo ni kwamba, Serikali tena imejiingiza kwenye biashara ya kukopa na kuwahudumia wananchi ambapo tulishajitoa.

Michango Katika Shule za Msingi

MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. AZIZA S. ALLY) aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekwishawatangazia kuwa Elimu ya Msingi ni ya bure hapa nchini; na kwa kuwa sasa hivi maana hiyo imepotea kabisa kutokana na michango mingi mashuleni:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu michango hiyo?
- (b) Je, michango iliyokusanywa kwa kipindi cha 2005-2007 ni kiasi gani, inaingia mfuko gani na inatumikaje?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Elimu ya Msingi kwa Shule za Serikali kwa sehemu kubwa inagharamiwa na Serikali. Kwa Waraka wa Elimu Na. 7 wa mwaka 2001, Serikali ilifuta ada na michango iliyokuwa kikwazo kwa baadhi ya wazazi wasio na uwezo kuandikisha watoto wao kwenda shule. Lengo la kufuta michango hiyo ni kuwawezesha watoto wote wapate nafasi ya kuandikishwa na kuhitimu Elimu ya Msingi, ambayo ni haki ya msingi ya kila mtoto kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995. Aidha, Serikali iliamua kufidia gharama za uendeshaji wa shule kwa kutoa ruzuku ya uendeshaji kwa kila shule. Hata hivyo, kutokana na ruzuku hiyo kutokidhi mahitaji yote katika shule, wazazi kupitia mikutano yao na vikao vya Kamati za Shule, huamua kuchangia gharama kwa kutoa michango. Kwa mujibu wa Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 1999, michango inayochangwa na wazazi ni lazima kwanza ipate kibali cha Afisa Elimu Kiongozi. Hata hivyo, wananchi wote kwa ujumla, wana wajibu wa kuchangia maendeleo ya shule yao bila kuachia wazazi wa wanafunzi peke yao.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna takwimu za michango iliyokusanywa kwa Shule za Msingi katika kipindi cha 2005-2007, kwa sababu michango hiyo ni ya wazazi na wananchi wa eneo husika, kwa ajili ya kufanikisha lengo mahususi kwa kipindi hicho. Mapato na matumizi ya michango hiyo, inatakiwa kutumika kama ilivyoainishwa na wazazi na taarifa kusomwa katika Mikutano ya Wazazi na wananchi wote. Hata hivyo,

uamuzi wa kuchangisha unatakiwa kuzingatia uwezo wa wazazi na ambao hawana uwezo watoto wao hawapaswi kuachishwa au kusimamishwa shule.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri kuhusiana na suala hili linalouliza habari ya michango mingi sana ambayo inaendelea katika shule zetu. Kwa kuwa lilikuwa ni jambo jema Serikali kufuta michango iliyokuwa kero huko nyuma ili kuwezesha watoto wote kusoma na ukawekwa utaratibu mzuri sana kwamba michango yote lazima iidhinishwe na Afisa Elimu Kiongozi, lakini tutakubaliana kwamba shule nyingi za msingi, sekondari na hasa shule binafsi; ipo michango mingi sana ambayo ni mzigo mkubwa sana kwa wazazi; je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu jambo hili?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, baadhi ya shule na hasa zisizo za Serikali, kumekuwa na michango mingi. Hata hivyo, ninaomba kurudia tena kwamba ni wajibu wa shule hizo zote, baada ya kukutana na Kamati zao au Bodi za Shule kwa shule zile za sekondari, kuleta maamuzi yao kwa Afisa Elimu Kiongozi ili aweze kutoa kibali. Madhumuni ya kibali hicho ni kuhakikisha kwamba, wananchi hawaumii na kwamba kulikuwepo na umuhimu wa michango hiyo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu hilo, ninaomba nitoe rai kwa Wabunge wote kuendelea kuhamasisha wananchi kuzichangia hizi shule kwani nyingi zimejengwa kwa nguvu za wananchi na ni vyema tukashirikiana. Kikubwa tuhakikishe tu michango hiyo inatumika kama ilivyokusudiwa na ninatoa agizo kwa wakuu wa shule na wenyeviti kwamba, watoe taarifa za mapato na matumizi ili kurudisha imani kwa wananchi na kwamba tuendeleze jukumu hili la elimu kwa wananchi wote.

Na. 25

Mradi wa Maji ya *BADEA* na *OPEC*

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MOHAMED G. DEWJI) aliuliza:-

Kwa kuwa katika kutekeleza Mpango wa Maji Safi kwa Watanzania wote, Serikali ilipata msaada toka *OPEC* na *BADEA*, kiasi cha shilingi bilioni kumi na mbili kilichoidhinishwa miaka minne iliyopita:-

- (a) Je, miradi hiyo ilikuwa ni ya aina gani?
- (b) Je, miradi hiyo ilianza kutekelezwa lini?
- (c) Kama haijatekelezwa, je, ni kwa nini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), ninapenda kutoa maelezo kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, inatekeleza Mradi wa Maji Mjini Singida kwa mkopo nafuu kutoka Mashirika ya *Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA)* na *OPEC Fund for International Development (OFID)* kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 12.43, sawa na shilingi bilioni 14.5. *BADEA* itatoa Dola za Marekani milioni 5.5 na *OFID* itatoa Dola za Marekani milioni 5.0. Mchango wa Serikali ya Tanzania kwa Mradi huo ni Dola za Marekani milioni 1.93. Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na *BADEA* ulisainiwa tarehe 9 Februari, 2003 na ule kati ya Serikali ya Tanzania na *OFID* ulisainiwa tarehe 30 Mei, 2003. Mradi huu ulipangwa kukamilika Aprili, 2008 na unahusu maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Mradi wa Majisafi: Unahusu ujenzi wa chanzo kipya cha maji, ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji wa majisafi. Chanzo cha maji cha Bwawa la Itamka, ambacho awali kilikuwa kitumike kilifanyiwa uchunguzi na Kampuni ya *Consulting Engineering Centre* ya Jordan mwaka 2005/2006 na kugundua kuwa, maji na udongo wa bwawa hilo vina chumvi nyingi na hivyo kuonekana kuwa chanzo hakifai kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa chanzo mbadala cha maji chini ya ardhi, ulianza Januari, 2006 na kukamilika Januari, 2007. Uchunguzi huo ulifanywa na Wakala wa Serikali wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*).

Matokeo ya uchunguzi yanaonyesha kwamba, kuna uwezekano wa kupatikana kwa maji mengi chini ya ardhi katika maeneo ya Mwankoko na Irao, ambayo yatakidhi mahitaji ya Mji wa Singida kwa miaka kumi na mitano ijayo. Kwa hivi sasa Wizara iko kwenye mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kusimamia ujenzi na mkandarasi wa kujenga mradi wenyewe.

(ii) Mradi wa Majitaka: Pamoja na mradi wa majisafi, *BADEA* walitoa Dola za Marekani 280,000 kwa ajili ya uchunguzi (*feasibility study*) wa mfumo wa majitaka kwa Mji wa Singida. Uchunguzi huo ulifanywa na Mhandisi Mshauri - *AAW Consulting Engineers*, kuanzia Oktoba, 2004 na kukamilika Februari, 2007. Aidha, Serikali inatarajia kujenga mfumo wa majitaka kwa kutumia fedha za Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kwa kifupi kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miradi inayotekelezwa ni ya aina mbili; mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na mradi wa upembuzi yakinifu kuhusu uondoaji wa majitaka.

(b) Mheshimiwa Spika, miradi hiyo miwili, ilianza kutekelezwa kwa pamoja Oktoba, 2004 kwa kupata wahandisi washauri wa kufanya usanifu.

(c) Mheshimiwa Spika, miradi imeanza kutekelezwa sasa kama nilivyoeleza kwenye utangulizi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upatikanaji wa chanzo cha uhakika cha maji, lilichangia sana katika kuchelewesha kukamilisha kwa utekelezaji wa mradi wa majisafi. Hata hivyo, ni matarajio ya Wizara yangu kuwa, ujenzi wa mradi huo utaanza katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009. Hivyo, Serikali imewaomba *BADEA* na *OFID* kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi huu hadi tarehe 31 Desemba, 2010. Aidha, ili kuendelea kupunguza makali ya tatizo la maji Mjini Singida, Wizara yangu imetoa shilingi milioni 55 kupitia Programu ya Sekta ya Maji, kwa kazi za dharura za kuboresha mfumo wa majisafi uliopo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza kama ifuatavyo: Kwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu sana na mpaka sasa hivi utekelezaji wake ni wa kusuasua na wananchi wa Singida Mjini wanapata adha sana ya maji kwani wanapata kwa mgao kwa siku tatu kwa wiki; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atanieleza ni mkakati upi wa haraka utakaosaidia Mji wa Singida kupata maji kila siku kuliko ilivyo sasa wakati wakisubiri mradi huu mrefu ukikamilishwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, utaratibu unafanywa kwa ajili ya kuendeleza mradi huu kwa upeo huo wa muda mrefu. Hata hivyo, Wizara yangu inao mpango mzuri kabisa, ambao unasaidia kukarabati miradi ya maji ambayo hivi sasa aidha, imechakaa au imeharibika kabisa na hata Mji wa Singida kama nilivyosema hapa, tayari tumeshapeleka shilingi milioni 55 kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya maji. Pamoja na hayo, ninaomba nimkaribishe ofisini Mheshimiwa Diana Chilolo, nimwonyeshe kabisa mikakati tuliyonayo ambayo ni ya *Quick Wins* kwa ajili ya kurekebisha hali hii, wakati tunasubiri fedha hizo za kutoka nje kwa wafadhili.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mradi huu awali ulikuwa uchukue maji katika Lambo la Itamka, ambalo lipo katika Jimbo la Singida Kaskazini; na kwa kuwa maji yale yakaonekana kwamba yana chumvi; katika Kijiji cha Ilongero ambacho ni kama kilomita 15 kufika Singida na katika kijiji kingine cha Msange, maji yaliyopatikana ni mengi sana; kwa mfano, Msange tumechimba mita 100 chini tumekutana na mto, yale maji yanaweza yakachukuliwa wakatengeneza miundombinu kupitia vijiji vya Singida Kaskazini vyote mpaka kufika Singida Mjini na watu wa Singida Kaskazini wanakanywa maji na watu wa Singida Mjini wakapata maji ya kutosha; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba, wanahitaji kuangalia uwezekano wa kuyatumia maji ya Ilongero na maji ya Kijiji cha Msange kwa

manufaa ya kuleta maji safi na salama katika Mji wa Singida huku wakinywesha vijiji vyote vinavyofuatana hadi kufika Singida Mjini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Ninapenda nikiri na mimi binafsi nilitembelea eneo hilo na anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, niliuona mradi ule wa maji. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa yeye alikwishatembelea na kuona hali yenyewe, ninakiri kwamba, kweli mimi binafsi sijatembelea, lakini ninajua kwamba utaratibu wetu ni ule ule. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa Mheshimiwa Spika ameku-*backup*, basi tuwasiliane katika hili na utaratibu wetu ni ule ule kwamba, tunazishauri Halmashauri za Wilaya, tunatumia wataalamu wetu kule kuwasaidia kutafuta vyanzo mbadala vya maji. Tatalichunguza suala hili na kwa utaratibu wa Programu yetu ya Kuendeleza Sekta ya Maji, basi miradi hii itatumika kama vyanzo mbadala.

Na. 26

Mradi wa Maji wa Kitumbi hadi Manga

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kutekeleza mradi wa maji katika Kijiji cha Kitumbi hadi Manga baada ya uthibitisho wa vipimo vya maabara kuwa maji ya Kitumbi ni salama:-

- (a) Je, utekelezaji wa mradi huo umeshaanza ili kupunguza tatizo la maji kwa vijiji vya Kitumbi, Kwenkwale, Mkata, Tengwe na Manga?
- (b) Kama utekelezaji wake bado; je ni lini mradi huo utatengewa fedha?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa, utekelezaji wa mradi huo utaisaidia sana kufidia upotevu wa fedha uliofanyika baada ya Serikali kushindwa kusimamia utekelezaji wa miradi ya Vijiji vya Mkata na Kwanyanje vilivyotarajiwa kugharimiwa na fedha za Benki ya Dunia?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, baada ya uthibitisho wa vipimo vya maabara kuwa maji ya Kitumbi ni salama, Wizara yangu imefanya kazi zifuatazo kwa lengo la kuwapatia maji wananchi wa vijiji vilivyopo jirani na chanzo hiki cha maji:-

(i) Upimaji wa wingi wa maji umefanyika na kubaini kuwa chanzo kina uwezo wa kutoa maji kiasi cha meta za ujazo 50 kwa saa.

(ii) Tathmini ya mahitaji ya maji iliyofanyika Desemba, 2007 imebainisha kuwa maji ya Kitumbi yanakidhi mahitaji ya maji kwa vijiji vya Kitumbi (mita za ujazo saba kwa saa); Kwenkale (mita za ujazo tatu kwa saa); Kwangalu (mita za ujazo nne kwa saa); Mkata (mita za ujazo 21 kwa saa); na Manga (mita za ujazo tatu kwa saa).

Kijiji cha Tengwe kitatafutiwa chanzo cha maji kingine katika utekelezaji wa programu ya kuendeleza Sekta ya Maji.

(b) Mheshimiwa Spika, fedha za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji zitapelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni inashauriwa kuviweka Vijiji vya Kitumbi, Kwenkale, Mkata, Tengwe na Manga ambacho kinajumuisha Kitongoji cha Tengwe katika mipango yao kulingana na vipaumbele vya Wilaya ili vijiji vilivyoainishwa kuwa na uwezekano wa kupata maji ya chanzo cha Kitumbi viweze kujengewa mradi wa maji kwa kutumia maji hayo ya Kitumbi.

(c) Mheshimiwa Spika, mradi wa maji katika Kijiji cha Mkata haukutekelezwa kutokana na kukosa chanzo cha maji baada ya kuchimba visima viwili na vyote vikakosa maji. Aidha, mradi wa maji wa Kijiji cha Kwanyange haukutekelezwa kutokana na mkandarasi kushindwa kujenga mradi huo na hivyo Halmashauri ya Wilaya kusitisha Mkataba. Kwa kuwa, Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini utafungwa mwezi Juni, 2008, vijiji vyote ambavyo miradi yake itakuwa haijakamilika wakati huo, vitaingizwa kwenye Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji vikiwa ni vijiji kumi vya ziada ambavyo tayari vimekwisha chaguliwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukaguzi wa hesabu za fedha (*Financial Auditing*) uliofanywa na wakaguzi, ilidhihirika kuwa, hakuna fedha ambazo zimetumika kinyume na mipango iliyokuwa imepangawa kufanyika. Fedha zimelipwa kulingana na kazi zilizofanyika.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Kwanza, kwa kuwa miradi ya Benki ya Dunia iliyotaka kuondoa tatizo la maji katika Vijiji vya Mkata na Kwanyange haikufanikiwa na hivyo wananchi kuona kwamba ni fursa iliyopotea kwa ajili ya urasimu wa upatikanaji wa fedha zile za Benki ya Dunia; je, Wizara ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba fedha zile zinazotengwa na Benki ya Dunia zinapatikana kwa wakati kwa sababu sasa ni miaka minne?

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, fedha za utekelezaji wa Programu wa Maendeleo ya Sekta ya Maji zitapelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Je, fedha hizo zitapelekwa lini kwa sababu ninaelewa wazi vijiji hivi tayari vimekwishawekwa kwenye mpango, lakini la ziada ni kwamba kupatikana kwa maji katika vijiji hivyo kutapunguza karibu asilimia 33 ya upungufu wa maji katika Jimbo la Handeni?

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kunithibitishia ni lini programu hii itaanza ili iondoke mezani twende kufanya vitendo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inaendelea kujipanga kufuatilia fedha hizi za *World Bank*, tayari Serikali hivi sasa imeweka mipango yake ya muda mfupi kama nilivyoeleza katika majibu ya mwanzoni; kwa sababu hatuwezi tukawa tunasubiri fedha za *World Bank* ambazo mlolongo wake ni mrefu, wakati watu wetu wanahitaji kunywa maji. Kwa hiyo, ipo mikakati ya muda mfupi, ambayo tunaitumia ili tuweze kutoa angalau fedha kwa ajili ya kukarabati au kujenga vyanzo kwa kiwango ambacho kinalingana na upatikanaji wa fedha tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kufuatilia, lakini haya mambo ya kuwasiliana na Mashirika hayo, kama mnavyojua, yana utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba upande wa pili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha zimekwishapelekwa na hata mwaka 2006/2007, fedha za maji zimekwishapelekwa katika Halmashauri za Wilaya. Nilichojifunza mimi katika ziara zangu fupi nilizozifanya kwenye Halmashauri ni kwamba, fedha hizi zinapopelekwa, Waheshimiwa Wabunge wengi hata Madiwani hawapati taarifa. Kwa hiyo, wanabaki wanatuuliza mambo ambayo tayari fedha ziko kule. Hata hivyo, ninayo orodha ya fedha zote zilizopelekwa katika Mikoa yote na katika Wilaya zote, siwezi nikaisoma hapa.

Ombi langu ni kwamba, fedha hizi zinapopelekwa huko na nitamwomba na Mheshimiwa Waziri, tufanye utaratibu wa kutoa nakala kwa Waheshimiwa Wabunge ili wajue kama fedha hizo zimepelekwa wazifuatilie; kwa sababu inasikitisha kwamba hata Madiwani ukienda huko nao wanakuuliza swali hilo hilo, wakati zipo kwenye Halmashauri zao.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nikuhakikishie kwamba, Ofisi ya Bunge itafanya kila linalowezekana ili nakala hizo ziwafikie Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana leo, hili ni suala la muhimu sana. Kwa hiyo, toa nakala za kututosha. Ahsante sana.

Ahaa! Samahani, Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa jibu la ziada.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri kwa swali la msingi na pia swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la vijiji kumi katika kila Wilaya ambavyo vitafadhiliwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia, tumekuwa tukilipata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi na sisi wenyewe tukiwa Wabunge; mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri linatuhusu. Ninaomba nitoe ufafanuzi mfupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti, 2007 ndipo tulipokubaliana na Benki ya Dunia kwamba, sasa tufuate masharti yao, kwa sababu kufuata masharti yetu hakutotupeleka mbali katika kutekeleza mradi huu; maana yake tutumie *guide-lines* zao. Sasa tulianza mchakato huo baada ya kuchelewa zaidi ya miezi sita; mwezi Septemba, 2007 na mwezi Oktoba, 2007 matangazo yalitolewa na Halmashauri za Wilaya katika magazeti mbalimbali, kuwaomba wataalamu waelekezi wapeleke *interest* kuonyesha kwamba wanataka kufanya kazi na hizo Halmashauri katika kutekeleza hiyo miradi kumi katika kila Wilaya. Mwezi Novemba, 2007 ilikuwa ndiyo mwisho wa kupeleka maombi kwa hao wataalamu waelekezi kwa Halmashauri za Wilaya mbalimbali.

Mwezi Novemba, 2007, Wizara ilifanya semina Mbeya na Arusha, kutoa maelekezo kuhusu utaratibu huu wa Benki ya Dunia ili tusikwame safari hii. Baada ya pale Halmashauri zikaenda kuanza mchakato wa kuwataka hao kufungua *bids* za hao wataalamu waelekezi. Taarifa za tathmini zimeanza kuwasilishwa Wizarani na mpaka sasa, tumepata taarifa kutoka Halmashauri za Wilaya 120 na tayari tumeshazipeleka hizo taarifa Benki ya Dunia ili kupata *no objection* ili waturuhusu tuendelee. Kwa hiyo, matarajio yetu ni kwamba, baada ya kufuata hizo taratibu walizozitaka, basi mradi huu unaweza ukatekelezwa kama ulivyopangwa, pamoja na kwamba umechelewa. Kwa hiyo, ninaomba kutoa matumaini kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutaufuatilia na kuusimamia kikamilifu ili unapoanza mwaka wa fedha wa 2008/2009, mradi huu wa vijiji kumi kwa kila Wilaya uwe umeanza na tunaziomba zile Halmashauri ambazo bado mpaka sasa hazijakamilisha waweze kukamilisha, zinajifahamu lakini tutaendelea kuzikumbusha.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa ufafanuzi mzuri.

Na. 27

Kiinua Mgongo kwa Askari Polisi

MHE. AMEIR ALI AMEIR aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Bajeti uliopita, Serikali ililiarifu Bunge kuwa, viinua mgongo katika ajira za Polisi vitashughulikiwa kwa Ari na Nguvu Mpya ili Askari wote wawe na mfumo mmoja wa pensheni:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani hadi sasa katika kulishughulikia jambo hilo na kama bado haijaanza ni sababu gani zilizokwamisha kazi hiyo?

(b) Kwa kuwa, Serikali iliahidi kulishughulikia jambo hilo kwa haraka; je, Serikali haioni kuzidi kuchelewa kulifanyia kazi, kunawavunja moyo na kuwakatisha tamaa wale wote ambao wanategemea kustaafu katika kipindi hiki au kuna mipango gani kwa Askari watakaostaafu baada ya kauli ile iliyotolewa Bungeni?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, kwa ruhusa yako ninapenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *Police Force Service Regulations* 1995, kifungu cha 12(b)(1) – (4), Askari Polisi anapoajiriwa hufanya kazi kwa Mkataba wa miaka mitatu mitatu hadi anapofikisha miaka 12 katika utumishi Jeshini. Baada ya Utumishi wa miaka kumi na mbili, Askari anakuwa na haki ya kuchagua atawaliwe na sharti mojawapo kati ya Mfumo wa Malipo wa Bakshishi (*Gratuity*) au Pensheni. Uchaguzi huu ni uamuzi wa Askari mwenyewe. Uaratibu huu unawahusu Askari wa vyeo vya chini, ambao hawajafikia cheo cha Mkaguzi Msaidizi. Askari wote kuanzia cheo cha Mkaguzi Msaidizi mpaka Mkuu wa Jeshi la Polisi, wao hutawaliwa moja kwa moja na Masharti ya Pensheni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali hapo juu, utaratibu wa mfumo wa mafao ya kustaafu ni kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi. Hata hivyo, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya Askari na wananchi kuhusu mfumo huu wa viinua mgongo vya Askari, Jeshi la Polisi lilichukua hatua ya kukusanya maoni ya watu mbalimbali wakiwemo Askari wenyewe na kugundua kwamba, mfumo huu bado unafaa kutumika kwa manufaa ya Jeshi lenyewe na Askari pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalifanyia kazi suala la mafao ya Kiinua Mgongo na Pensheni kwa Askari Polisi na Watumishi wengine wa Umma. Mpango wa Serikali ni kuona namna bora ya kuboresha mishahara ya Askari na stahili zao nyingine ili mafao yao ya kustaafu au kuacha kazi, ambayo hutolewa kutegemea mishahara wa mwisho wa Askari, yaweze kuwa bora zaidi na kukidhi matarajio ya huduma yao kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia maslahi ya Askari Polisi, Wizara yangu tayari imeshawasilisha mapendekezo ya mishahara mipya na posho nyingine za Askari mbele ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Mishahara. Hivyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, tuvute subira wakati Serikali inayafanyia kazi mapendekezo hayo.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa suala hili lina maana ya viinua mgongo; na kwa kuwa mara nyingi Askari wanapostaafu wanasumbuka sana kufuatilia viinua mgongo vyao na hususan wale wanaotoka Zanzibar ambao ni sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano, lakini pia na wale wanaoishi katika sehemu mbalimbali katika Mikoa yao kuja Dar es Salaam; je, Naibu Waziri haoni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuweka vitengo katika maeneo yale ili kuwaondolea usumbufu Askari hao wanapostaafu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ayasemayo tumekwishayaona katika Wizara kuhusu wastaafu na tumepokea barua za wastaafu ambao wamekuwa wanaomba taratibu zitazamwe kuhusu mafao yao. Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, analishughulikia suala hili akiwahusisha Wakuu wa Idara mbalimbali hasa Wakuu wa Jeshi la Polisi katika Wizara. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umetutupa mkono.

Na. 28

Sheria ya Kuzuia Uzembe wa Madereva

MHE. MARIA I. HEWA aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na ajali nyingi zinazojitokeza barabarani na kusababisha maafa kwa uzembe unaofanywa na madereva kuendesha magari vibaya: Je, ni kwa nini Serikali isitunge sheria ya kuwabana matajiri wa Makampuni au magari kufutiwa leseni zao pindi ikibainika kuna uzembe umetendeka?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kumekuwepo na ajali nyingi zinazotokea barabarani na kusababisha maafa makubwa kwa wananchi na mali zao kwa sababu ya uzembe unaofanywa na madereva wanaoendesha magari vibaya na kusababisha ajali. Serikali imeliona tatizo hilo na katika kulishughulikia, imetunga Kanuni ili kuwabana wamiliki wa magari hasa ya abiria, yakiwemo ya watu binafsi, Makampuni na Taasisi nyinginezo, ambayo madereva wake wametenda makosa ya Usalama Barabarani kwa uzembe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vifungu vya 17(3) na 29 vya Kanuni hiyo, zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali, GN. Na. 218 la tarehe 26 Oktoba, 2007 ni kosa kwa mmiliki wa gari la abiria, mtu binafsi au kampuni, kukiuka masharti ya leseni ya usafirishaji (*condition of licence*), ambayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa, gari lake linaendeshwa katika mwendo ulioruhusiwa kisheria (*a licensed passenger vehicle adheres to specified speed limits*). Iwapo atakiuka masharti hayo, hatua zinazoweza kuchukuliwa na Mamlaka ya Usafirishaji (*SUMATRA*) ni pamoja na kufutiwa leseni ya usafirishaji, adhabu ya kifungo au kulipa faini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia imeshatoa Kanuni Mpya za Usalama Barabarani za mwaka 2007, ambazo zinaelekeza kuwepo kwa makundi mbalimbali ya leseni za udereva. Suala hili linashughulikiwa na Wizara ya Fedha, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania. Pindi utaratibu huu utakapoanza kutumika, itasaidia kupunguza ajali za barabarani.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili mafupi tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba katika kujibu kwake, kuna Kanuni ambayo wameitunga kuwabana matajiri hao, lakini niombe basi katika swali langu la kwanza kwamba, baada ya kutokea ajali watu huumia, wengine hufa na wengine hupona kwa nusura tu ya Mwenyezi Mungu; je, siyo wakati muafaka sasa Serikali ikaingilia kati kwa sababu huwa anaachiwa tajiri tu na mwenye bima kujadili kumlipa huyo mwathirika wa ajali; Serikali ikaona umuhimu wa kumlipa kwanza aliyepata ajali kulikoni kuthamini gari kwanza?

La pili, viwango hivyo ambavyo wanalipwa hao ambao wamepata ajali, kukatika mikono, kukatika miguu au hata kufa, vipo chini sana kwa wakati kama huu ambapo sasa tunapaswa kujadili viwango vipya. Je, Serikali ina tamko gani kuhusu viwango hivyo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, alivyosema kuhusu ulipaji baada ya ajali, utaratibu ni kwamba, malipo yanaachwa kwa mwendeshaji gari na yule ambaye amepata ajali. Kwa kweli hili ni suala la kisheria, ninadhani tunaweza tukalitazama kufuatana na Kanuni, lakini si suala ambalo Serikali inaweza ikaliambia peke yake. Kwa sababu ni kitu ambacho lazima kifuata utaratibu na kama hilo analiona hivyo, ningeshauri kwamba, tuzungumze na Mheshimiwa Mbunge, tuweze kutazama kama tunaweza kuboresha Sheria hiyo.

Maana yake hatuwezi tukaamua tu kusema kwamba, Serikali inaamua, lakini ni suala ambalo linawahusu wadau mbalimbali. Kwa hiyo, kuhusu viwango na kuhusu nani alipwe kwanza, ninafikiri ni suala ambalo linawahusisha watu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ni kitu ambacho hatuwezi tukakiamua kwa pamoja hapa kwa haraka. Hiki ni kitu ambacho kinataka mazungumzo kwa watu wote wanaohusika na hatimaye kitengenezewe sheria na chombo cha kutengeneza Sheria ni Bunge lako Tukufu. Ahsante sana.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa sheria inasema madereva wasiende zaidi ya kilomita 80 kwa saa, lakini wapo madereva ambao wanaokwenda zaidi ya kilomita hizo kwa saa hasa madereva wanaowaendesha Viongozi wetu na hasa Mawaziri; je, sheria hii inasemaje? Kama hawaruhusiwi kwa nini wanawapeleka Mawaziri kwa spidi kubwa namna hiyo kuhatarisha maisha yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hiyo anayosema Mheshimiwa Mbunge ya kusema kwamba madereva wa Mawaziri kwa kweli mimi naweza kusema ni *allegation* Itunaipokea, lakini ni kitu ambacho sidhani kwamba kisheria ni sheria ya kusema kwamba twende kilomita 80 na katika barabara wapo polisi trafiki wako pale kutilia mkazo hiyo lakini nafikiri kama hiyo inasemekana kwamba ni hivyo basi tutawaambia madereva husika waende kwa mujibu wa taratibu na sheria inavyosema kwa *speed limit*. Lakini bado nitasema kwamba hiyo ni *allegation* kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ingawa muda unaonekana umekwisha lakini nadhani itabidi swali hili moja linalofuata tulifikie. Lakini kabla nilitaka kusema tu kwamba labda Wizara ingetazama hii spidi ya 80 ni ya chini sana na ife! (*Makofi*)

Ndiyo! Hivi nani anatoka Dodoma mpaka Dar es Salaam kwa spidi 80? Hakuna mtu! Kwa hiyo, tuchukue hali halisi, mambo haya yaliwekwa wakati wa miaka 1970 magari yalipokuwa ya ovyo ovyo, sasa kuna magari yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, samahani siruhusiwi lakini nimeibiaibia kidogo. Mtu una VX halafu uende spidi 50 au 80 laah! Haiwezekani.

Na. 29

Mikopo ya Wajasiriamali

MHE. JAMES P. MUSALIKA aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kujibu swali Namba 59 katika Mkutano wa Kumi Serikali ilisema kuwa Wilaya ya Geita haitapata Mkopo wa awamu ya pili kwa sababu katika awamu ya kwanza ilipata zaidi ya matarajio; kwa kuwa pamoja na hali hiyo Serikali iliahidi kuwa imetenga fedha kwa ajili ya wajasiriamali wa Jimbo la Nyang’hwale ambao mgawo wa kwanza haukuwafikia; je, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2008 ni wajasiriamali wangapi kutoka katika vijiji vya Busolwa, Shabaka, Nyang’hwale, Mwingiro, Kharuma, Nyungwa, Kakora, Kafita na Bukwimba walipata mikopo hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang’hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mbunge kuwa nilipokuwa najibu swali lake Na. 59 katika Mkutano wa Kumi wa Bunge hili hapo tarehe 4 Februari, 2008, Serikali iliahidi kutenga fedha kwa ajili ya wananchi walioko kwenye maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya utoaji wa fedha za mikopo kwa wajasiriamali. Katika kutekeleza ahadi hiyo Serikali imekwishatenga kiasi cha shilingi bilioni 2.29 kwa ajili ya kutoa mikopo katika maeneo ambayo hayakufikiwa kwenye awamu hiyo ya kwanza vikiwemo na vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vilivyopo katika Jimbo la Nyang’hwale Wilayani Geita.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimeeleza nilipokuwa nikijibu swali hilo la Mheshimiwa Mbunge, Serikali ilikwishateua asasi za fedha 14 zitakazoshiriki katika utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali katika awamu hii ya pili hususan kwenye maeneo ambayo hayakufikiwa.

Mchakato wa kutekeleza mpango wa utoaji mikopo katika awamu hii ya pili ulianza tarehe 15 Januari, 2008 chini ya usimamizi wa Benki Kuu kwa kuanza kuwekeana saina za mikataba ya makubaliano baina yake na Asasi za Fedha zinazoshiriki katika mpango huu. Kwa Wilaya ya Geita Mkataba wa makubaliano kati ya Benki Kuu na Asasi husika ukishakamilika utaratibu wa utoaji wa mikopo utanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kufuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa mpango huu ili wananchi waweze kupatiwa mikopo hiyo ya wajasiriamali wakiwemo na wale walioko kwenye vijiji vya jimbo la Nyang’hwale alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ambavyo mgawo wa kwanza haukuwafikia. Napenda kuendelea kutoa mwito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kujiunga katika ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) ambao utawajengea tabia ya kujiwekea akiba na kujiunga na kujipatia mikopo kwa masharti nafuu.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linauliza kufikia tarehe 15 Machi, 2008 ni wajasiriamali wangapi katika Kata ambazo nimesema za Busolwa, Shabaka, Nyang’hwale hadi Bukwimba zote zile katika jimbo walikuwa wameshapata;

Kwa kuwa tarehe 6 Aprili, 2008 nilipokuwa nafanya Mkutano wa hadhara katika Kata ya Busolwa wajasiriamali na wananchi wengi waliuliza pesa hizi na ahadi kwa sababu huwa wanafuatilia matamshi ya Serikali; na kwa kuwa sasa hivi Waziri hajajibu swali; jje, anaweza kusimama kujibu swali hili?

La pili, kwa kuwa kimsingi pesa hizi za wajasiriamali hazitoshelezi kwa sababu wajasiriamali wengi sana nchini wanazihitaji na wamekwishahamasishwa na SACCOS na vikundi llakini pesa hazitoshelezi; je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba pesa zile za EPA zilizoibiwa Benki Kuu zinazorudi sasa hivi wamekwisharudisha zaidi ya shilingi bilioni 60, pesa hizi sasa wapewe wajasiriamali ili wazalishe pamba, mahindi, dengu, korosho, kahawa ili waongeze pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza alilouliza Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vijiji vingapi vimekwishapatiwa mikopo alikiri kwamba halijapatiwa jibu. Jibu nimelitoa, ni kwamba sijapata mchakato wa kuwekeana saina baina ya Benki Kuu na asasi husika ili ziweze kutoa mikopo katika hayo maeneo na hivyo vijiji ndiyo inayoendelea. Kwa kweli hilo ndilo jibu. Kwa sasa hivi zoezi la utoaji wa mikopo huko vijijini halijafika kwa sababu utaratibu huo wa kukamilisha uwekaji saina kati ya Asasi za Fedha na Benki Kuu bado unaendelea. Kwa hiyo, wakati wowote zoezi hilo litakapokamilika vijiji hivyo vitafikiwa na kama nilivyokuwa nimeahidi utaratibu wa kuomba pamoja na kupitisha maombi hayo utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hili la pili la kwamba fedha hazitoshelezi, mimi nakubaliana naye kwamba fedha hazitoshi. Lakini kwanza lazima tuishukuru Serikali kwamba hapo ilipoanzia ni kama kichocheo na ikumbukwe kwamba fedha hizi za mikopo zinapokopeshwa ni za mzunguko, kwa hiyo, nataka nitoe wito kwamba kwa wale ambao walikwishakopeshwa kwa awamu ya kwanza na hata watakaokopeshwa awamu ya pili wawe na ile nidhamu ya kurudisha fedha hizi ili ziweze kuwafikia na wengine ambao wanataka kuzikopa.

Kwa hiyo, Serikali imetoa kama kichocheo ili fedha hizi ziende kama mzunguko na kuwafikia watu wengi zaidi. Hivyo suala la kwamba tutafute fedha zingine za kutoka katika vyanzo vingine pamoja na hivyo walivyovitaja pengine naona si muafaka sana badala yake tutumie fursa hii ambayo Serikali imetukabidhi.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naitia kinyumenyume tu. Namshukuru Mhudumu wa Bunge kwa kunisaidia kupitia vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya wajasiriamali waliokopeshwa katika vijiji vya Busolwa, Shabaka, Nyang'hwale, Mwingiro, Kharumwa, Nyungwa, Kakora, Kafita na Bukwimba napenda kujibu kama ifuatavyo kwa kuongezea jibu zuri alilolitoa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Takwimu hizi bado tunawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita hawajatujibu lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anatoka katika Wilaya hiyo vilevile namshauri naye angekwenda kukaa kupata takwimu hizi kutoka Wilayani kwake. Lakini tutakapokuwa tumezikamilisha tutamtumia vilevile kupitia Wizara yetu.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Tatizo la Wilaya ya Geita ni ukubwa na wingi wa watu pamoja na vikundi vinavyohitaji fedha hizo. Wilaya ya Geita ukubwa wake unaweza kulingana na baadhi ya Mikoa na baadhi ya fedha zinazotolewa katika Mkoa unakuta ni shilingi bilioni 1, lakini Wilaya ya Geita kwa idadi yake ya watu na vikundi inakaribia Mkoa wa Singida, Lindi na sehemu kidogo ya nchi ya Zanzibar. Je, katika kugawa fedha hizo wanafikiria kwamba kuna baadhi ya Wilaya ambazo zinahitaji kupewa mgawo sawa na mikoa? (*Makofi*)

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi mwongozo tunaotumia ni kwamba kila Mkoa unapata mgawo sawa na mikoa mingine yote. Lakini vilevile tungependa kusema vipaumbele ni vikundi gani vinavyopaswa kupata, vinapangwa na Wilaya yenyewe ambayo ndiyo inawasilisha mapendekezo hayo katika Benki ambazo zimepewa hizo fedha.

Kwa hiyo, hatujaingia katika utaratibu wa kuangalia kila Wilaya ina ukubwa gani na utendaji gani kwa sababu tukifanya hivyo unaweza ukajikuta Dar es Salaam peke yake inaweza ikachukua fedha zote. Ndiyo maana tukachukua utaratibu kwamba kila Mkoa kwa sasa hivi upate mgawo sawa halafu vipaumbele vipangwe na Wilaya zenyewe.

Kwa hiyo, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Geita iizingatie ukubwa wa Wilaya yake, iizingatie idadi ya watu walionao na wapange vipaumbele sawa sawa ili fedha zinapokwenda kila sehemu ziweze kufika japo kwa uchache. Fedha hizi zinapaswa kutengeneza kwa mfuko unaozunguka (*Revolving Fund*). Tena mategemeo yetu ni kwamba fedha zinapokuwa zinazunguka na wale waliokopa wanarejesha, wale ambao hawajafikiwa watafikiwa bila matatizo yoyote.

MASWALI YALIYOJIBIWA KWA MAANDISHI

Na. 19

Wahusika wa Matumizi Mabaya ya Fedha za Serikali

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Kwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha za Bajeti ya Serikali kimetengwa na kupelekwa TAMISEMI kwa ajili ya Maendeleo ya Wananchi; na kwa kuwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayoishia tarehe 30 Juni, 2006 ilionyesha kuwa TAMISEMI kuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali ambapo kuna fedha zimetumika bila hati za malipo, hali ambayo ni kikwazo katika kutekeleza dhana nzima ya MKUKUTA:-

Je, ni wahasika wangapi wamewajibika na ni akina nani (kwa majina) katika ngazi ya Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kote nchini tangu ripoti hiyo ilipobainisha ufasidi huo?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, zinatoa maoni na mapendekezo (*Audit Opinions and Recommendations*) ya hatua zinazofaa kuchukuliwa na Mamlaka husika. Mapendekezo haya yanatokana na kazi za ukaguzi zilizofanyika katika kipindi mahususi. Maoni ya Ukaguzi yamegawanyika katika sehemu kuu tatu; yaani Hati Safi au Inayoridhisha (*Unqualified Opinion*), Hati Yenye Shaka (*Qualified Opinion*) na Hati Mbaya (*Adverse Opinion*).

Maoni ya Mkaguzi, yanatokana na hoja au masuala ambayo hayakupatiwa ufafanuzi wakati wa ukaguzi na katika kipindi ambapo taarifa za ukaguzi zinatayarishwa. Kati ya hoja zinazotokea mara nyingi ni kutoonekana kwa nyaraka za fedha (*Accounting Documents*), akati wa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2006, kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hapakuwepo na hoja za fedha kutumika bila hati za malipo na Wizara ilipata Hati Safi (*Unqualified Audit Opinion*). Aidha, katika kipindi hiki, Sekretarieti za Mikoa 16 zilipata Hati Safi na tano zilipata Hati zenye Shaka, kutokana na kukosekana kwa baadhi ya kumbukumbu. Sekretarieti za Mikoa hiyo ni zile za Mbeya, Kigoma, Lindi, Mtwara na Manyara. Dosari hizo zimekwisharekebishwa na kuwasilishwa kwa Wakaguzi. Hakuna Sekretarieti ya Mkoa iliyopata hati mbaya. Katika ngazi ya Halmashauri; Halmashauri 53 zilipata Hati Safi, 62 zilipata hati zenye shaka na Halmashauri nne zilipata Hati Mbaya (*Adverse Audit Opinion*), nazo ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali kukabiliana na hali hii mbaya; kwa mfano, baada ya Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilishwa Bungeni, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliwaita Maafisa Masuhuli wa Wizara, Wenyeviti, Mameya, Wakurugenzi, Waweka Hazina na Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri zote nchini, tarehe 29 Aprili, 2007. Katika kikao hicho, Mheshimiwa Rais, aliwaagiza Viongozi hao kupeleka taarifa hizo kwenye vikao vya Mabaraza ya Madiwani ili zijadiliwe na aliwaagiza Wakuu wa Mikoa, wahudhurie vikao vitakavyojadili Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila Halmashauri. Mijadala ambayo iliamua hatua mbalimbali za kuchukua katika kurekebisha hitilafu zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, juhudi nyingine ni pamoja na agizo la tarehe 29 Mei, 2007 la Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipoaziagiza Wizara, Mikoa na Halmashauri zote, kuunda Kamati za Kusimamia, Kudhibiti na Kukarabati Mapato na Matumizi ya Serikali katika ngazi hizo. Serikali imeajiri Wahasibu na Wakaguzi wa ndani 930 na kuwapeleka kwenye Halmashauri mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la menejimenti mbaya ya fedha za umma. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeanzisha utaratibu wa kuhakikisha kuwa inapata nakala ya hoja za ukaguzi unaofanywa katika Halmashauri kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wake. Na Kitengo cha Ufuatiliaji kilichopo chini ya ofisi yangu, kinafanya ufuatiliaji katika Halmashauri kila robo mwaka kimkoa ili kutathmini *value for money* ya fedha zinazopelekwa huko.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ni Mamlaka kamili, hatua mbalimbali za kutekeleza mapendekezo ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, zilitekelezwa ikiwa ni pamoja na kujibiwa kwa hoja za Mkaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika hoja zote zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, hapakuwepo na hoja inayohusiana na wizi wa fedha za umma. Hoja zilizokuwepo, zilionyesha udhaifu katika udhibiti wa ndani (*Internal Control Systems*), ambao umedhihirika kushindwa kudhibiti makosa yaliyosababisha kuibuliwa kwa hoja mbalimbali. Hata hivyo, hatua za kinidhamu na kisheria zimechulikuwa na baadhi ya watumishi kulingana na uzito wa kosa. Orodha ya baadhi ya wahusika nitaiwasilisha kwa Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na sasa ni matangazo ila kabla sijaanza kusoma matangazo na mimi hapa nimeulizwa swali na Mheshimiwa Mbunge mmoja mwanamke kwamba mwaka jana nilitamka matokeo ya utafiti ambao ulionyesha kwamba baadhi ya wanaume wanapigwa na wake zao. Sasa niliomba nirejee, ana jambo la haraka kuhusiana na takwimu hizo. Takwimu zinasema asilimia 35 ya wanaume wa Tanzania waliooa wanapigwa na wake zao ila hawasemi kwa sababu inaonekana ni jambo la aibu kukimbilia Polisi kusema mkeo amekupiga. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa pamoja na kwamba tunacheka, asilimia hii ni pamoja na Wabunge. Ndio maana yake wote ni wale wale tu. Basi Mheshimiwa mhusika nadhani umeipata takwimu na unaweza kuendelea.

Wageni wetu leo ni kama ifuatavyo. Wapo wageni wa Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mbunge wa Ruangwa, nao ni Bw. Jean Philip Grow kutoka Kampuni ya *Clean Energy Capital Limited, London*. Yuko wapi sijui? Aha! Yule pale! Ahsante sana. *I am not sure you follow Swahili but you are warmly welcome, Tanzania loves visitors. Welcome to Tanzania*. Na mwenyeji wake mwingine ni Dr. Fredrick Ringo, Mwakilishi wa Kampuni hapa nchini, yule pale! Karibu sana Dr. Ringo.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Professa Idris Mtulia ambao ni mkewe ambaye hakumtaja jina lakini Mrs. Mtulia. Yule pale! Ahsante sana. Karibu sana! Pia na rafiki zao Bwana na Bibi Marijani. Wale pale kutoka Rufiji! Karibuni sana!

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wanafunzi nadhani na walimu kutoka shule maarufu ya Al Haramain ya Dar es Salaam. Ningeomba wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Ahsante. Karibuni sana! Nawapongeza walimu kwa mfano mzuri wa kuwaleta wanafunzi waone wao wenyewe ana kwa ana jinsi Bunge linavyoendeshwa. Ahsante! karibuni sana na safari njema mtakaporejea.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na Mkutano wa Kamati ya Huduma za Jamii leo tarehe 9 Aprili, 2008 ukumbi Na. 219 mara baada ya Uchaguzi wa Wenyeviti, shughuli ambayo inafuatia baada ya maswali. Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Kamati za Huduma za Jamii, ukumbi 219 mara baada ya kumaliza shughuli za Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge.

Tangazo langu la mwisho linahusu tukio la Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha CUF wakiungwa mkono sio na baadhi, karibu wote waliokuwemo jana wa Kambi ya Upinzani kutoka humu Bungeni.

Jana nimetafuta ushauri wa kisheria na suala hili linaelekea kuwa na kasoro. Kwa sababu hapa tulichonacho ni mazungumzo baina ya vyama viwili vya siasa ili kupata ufumbuzi wa tatizo linalohusu sehemu moja ya Muungano.

Sasa kwa kiasi gani Bunge hili lihusishwe na jambo kama hilo? Kwa sababu tukiruhusu hali hii ina maana leo na kesho vyama vingine viwili vya kisiasa vikiwa vina ugomvi wao nje ya Bunge hili nao watataka watoke nje ya Bunge. Kwa hiyo, naiomba Kamati ya Kanuni, wanasheria wanatuandikia ushauri, kesho saa 7.00 Kamati ya Kanuni tukutane tulitafakari jambo hili ili tuweze kuliwekea mwongozo na kama kuna upungufu katika Kanuni za Bunge tuliwekee utaratibu.

Kwa sasa natamka tu kwamba wale waliotoka nje ya ukumbi kwa shughuli zisizokuwa rasmi kwa maana ya Bunge hili basi hawastahili kulipwa posho zinazohusika kwa siku zote ambazo watakuwa nje mpaka hapo tutakapotangaza utaratibu mwingine kwa sababu waliyokwenda kuyafanya wala hayahusiani na shughuli za Bunge letu.

Kwa hiyo, Kamati ya Kanuni kesho saa 7.00 ili kulipatia jawabu jambo hili na tutatangaza uamuzi hapa Bungeni.

UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu Kanuni mpya zimetuhitaji kwamba tuwachague Wabunge wenzetu watatu ili waweze kuwa Wenyeviti kwa maana ya *Presiding officers* wakati ambapo Spika na Naibu Spika hawapo. Kanuni mpya zimetenda haki zaidi kwa sababu zimezingatia jinsia na pande mbili za Muungano. Sasa nitamwomba Katibu aweze kutusomea utaratibu mzima wa shughuli yenyewe, Mmbaga naona unashangaa shangaa, huu hapa, utusomee kutuelekeza ili tuweze kupiga kura kwa mujibu wa kanuni.

MAELEZO YA SPIKA KUHUSU UCHAGUZI WA WENYEVITI

KATIBU MEZANI – BI PHOEBE MMBAGA: Mheshimiwa Spika, matakwa ya Kanuni kufuatana na machapisho katika Kanuni za Bunge, sasa kutakuwa na Wenyeviti watatu wa Bunge wataochaguliwa kutoka miongoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuzingatia jinsia na pande za Muungano.

Kwa mujibu wa Kanuni 7(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ya Uongozi imepewa mamlaka ya kupendekeza majina 6 ya Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Bunge kulingana na vigezo vilivyotajwa hapo juu na kuyawasilisha Bungeni ili kupigiwa kura .

Aidha, Kanuni ya 11(2) inatoa fursa kwa Wenyeviti waliomaliza muda wao kuchaguliwa tena kwa sharti kwamba wao wamechaguliwa tena kuongoza Kamati za Kudumu za Bunge kwa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti. Kanuni hiyo iinasomeka kama ifuatavyo, nanukuu: “Wenyeviti wa Bunge watahika madaraka yao kwa muda ambao wataendelea kuwa Wenyeviti au Makamu Wenyeviti na wanaweza kuchaguliwa tena kuwa Wenyeviti wa Bunge iwapo watachaguliwa tena kuwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.”

Kamati ya Uongozi ilikutana jana tarehe 8 Aprili, 2008 ili kujadili na kupendekeza majina kulingana na matakwa ya Kanuni. Baada ya majadiliano Kamati ya Uongozi ilipitisha kwa kauli moja pendekezo kuwa Wenyeviti wa Bunge wanaomaliza muda wao waendeleo kushika nafasi hizo kwa kipindi cha maisha ya Bunge kilichobaki hasa kwa kuwa wamechaguliwa tena kuwa Wenyeviti wa Kamati zao na Kanuni za Bunge hazizuii mgombea yeyote kupitishwa bila kupingwa.

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar Kamati ya Uongozi ilimempitisha bila kupingwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Hivyo, Kamati ya Uongozi inapendekeza Waheshimiwa wafuatao wapitishwe na Bunge kuwa Wenyeviti wa Bunge kwa kipindi kilichobaki cha maisha ya Bunge:-

(i) Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, (Mb.) - Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

(ii) Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama (Mb.) – Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

(iii) Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, (Mb.) – Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelezo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kura za Bunge huwa zinapigwa kwa namna kuu mbili, bado hatujaanza ile *electronic* ambayo itakuwa ni ya tatu. Moja ni kwa sauti, pili, kura zinaweza kupigwa kwa karatasi. Sasa naona kwa hili kwa sababu Kamati ya Uongozi imeleta majina matatu, naomba nitakapowataja kila mmoja, hao ambao walipendekezwa na Kamati ya Uongozi, atasimama mahali alipo kwa sekunde chache halafu nitawahoji kwa kila jina. Kwa hiyo, sasa naomba Mheshimiwa Job Yustino Ndugai – Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira asimame.

Mnataka tuwaulize maswali? Hapana! Hamna!

Ahsante Mhe. Job Yustino Ndugai, sasa nitawahoji wanaoafiki kwamba Ndugu Ndugai achaguliwe kuwa Mwenyekiti wa Bunge waseme “Ndiyo!”

WABUNGE: Ndiyo!

SPIKA: Wasioafiki waseme “Siyo!”

MBUNGE: Siyo!

SPIKA: Kuna mmoja tu ndiye aliyesema “Siyo.” Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndugai amechaguliwa leo tarehe 9 Aprili, 2008. Sasa nitamwita Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

Ahsante! Mheshimiwa Jenista mmemuona, mnamfhamu, wale wanya kama Al-Shymaa amekwishamwona vizuri, kwa hiyo, sasa nitawahoji, wanaoafiki kwamba Mheshimiwa Mhagama achaguliwe kuwa Mwenyekiti wa Bunge waseme “Ndiyo!”

WABUNGE: Ndiyo!

SPIKA: Wasioafiki waseme “Siyo!” Ahaa! Hamna kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama umechaguliwa na Bunge kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Wa tatu ni Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid Mbunge wa Kwamtipura. Yule pale! Yeye Mbunge wa Kwamtipura pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za

Serikali. Sasa nitawahoji wanaosema Ndugu Zubeir Ali Maulid awe Mwenyekiti wa Bunge waseme “Ndiyo!”

WABUNGE: Ndiyo!

SPIKA. Wasioafiki waseme “Siyo!”

Hamna! Kwa hiyo, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid amechaguliwa naye kuwa Mwenyekiti. Kama ilivyo kawaida ya shughuli hizi za Uchaguzi kwa wale pia watapenda kutoa neno la shukrani, ningeomba niwape fursa hiyo kwa sababu ni kawaida.

Mheshimiwa Ndugai ungependa kusema chochote kwa kifupi sana?

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, ningependa kulishukuru sana Bunge lako kwa heshima kubwa sana walionipa ya kuwa Mwenyekiti wa Bunge kwa kipindi hiki kilichobaki cha uhai wa Bunge letu. Hii ni heshima kubwa sana kwangu lakini pia ni heshima kubwa sana kwa wapiga kura wangu wa Kongwa. (*Makofi*)

Naahidi kufanya kazi kwa bidii zaidi kuhakikisha kwamba nakusaidia wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, lakini vilevile kuhakikisha kwamba Bunge letu linaendeshwa na taratibu zake na kanuni kadri ya maelekezo yanavyotakiwa yatekelezwe ndani ya Bunge.

Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa mara nyingine kwa kura zote za Waheshimiwa Wabunge, nasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, na mimi nasimama kwa heshima na taadhima kwanza kabisa nikikushukuru wewe binafsi. Lakini pili nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima nyingine kubwa kabisa ambayo wamenipa na kunidhihirishia katika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, heshima hii si kwangu tu ni heshima kwa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini vilevile kwa wananchi wa jimbo la Peramiho ambalo mimi ninawawakilisha ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami naomba niseme, nitajitahidi kuwa makini na kuwa mtiifu kabisa katika kushirikiana na wewe Naibu Spika na viongozi wengine wowote ndani ya Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu anayewakilisha Serikali yetu, Kiongozi wa Upinzani na Wabunge wengine wote. Lengo kubwa ni kusaidiana kuhakikisha Bunge letu linaendeshwa kufuatana na taratibu au kanuni zilizowekwa na vilevile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kuleta maendeleo ya wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na wananchi wa Tanzania na nawashukuru sana Wabunge wote. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista. Sasa nitamwita Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa maneno machache ya shukrani.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kwanza kabisa kukushukuru wewe mwenyewe lakini vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kwa kweli hii ni heshima kubwa sana na si kwangu tu lakini pia na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura ambao nawawakilisha.

Vilevile napenda nitoe shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaotoka Zanzibar kwa sababu hii ni nafasi mojawapo katika ile sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano. Wote kwa pamoja, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati waliona kwamba ningefaa kuwawakilisha. Kwa hiyo, naahidi na naliahidi Bunge hili kwamba nitashirikiana na Wenyeviti wenzangu ambao tumechaguliwa hivi punde, kuendesha shughuli za Serikali tukishirikiana na wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Serikali katika kuendesha shughuli za Bunge na nitajifunza kutoka kwa hao wote ili tuhakikishe kwamba Bunge letu linakwenda vizuri kwa mujibu wa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kukushukuru tena kwa heshima hii, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninao udhuru kidogo ofisini, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Naibu Spika aje akalie Kiti ili niendeleo na kazi za ofisi.

NAIBU SPIKA: Asalaam Aleykum! Waheshimiwa Wabunge kwanza kabisa nawashukuru sana kwa salamu ambazo nilipewa na Mheshimiwa Spika kwa kutangaza kwamba nilikuwa nauguliwa, na ni kweli nauguliwa na mgonjwa bado yupo *TMJ*. Lakini pia na mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti watatu waliochaguliwa asubuhi hii na nina hakika wote mnafahamu uhodari wao katika kufanya kazi, na Mheshimiwa Maulid tutakuwa naye pamoja na tunaahidi kwamba sisi tutakuwa ni timu ambayo iitaweza kulipeleka Bunge hili mahali pazuri kwa kuheshimu taratibu kanuni na Katiba. Pia tutaheshimu pande zote, sisi ni Bunge la Serikali, ni Bunge la nchi, kwa hiyo, tutafanya kazi kwa mujibu wa Katiba. (*Makofi*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Usambazaji wa Petroli wa Mwaka 2007 (*The Petroleum Supply Bill 2007*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja kuwapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti ambao dakika chache zilizopita Bunge hili limewachagua kwa kura zote za “Ndiyo”, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla kutoa salamu zetu za rambirambi kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, Uongozi wa Mkoa wa Manyara na kwa familia za wenzetu waliopoteza Ndugu na Jamaa zao katika machimbo ya *Tanzanite* huko Mererani, Mkoani Manyara kutokana na mafuriko yaliyoikumba baadhi ya migodi katika eneo la Kitalu B katika maeneo hayo ya Mererani usiku wa tarehe 28/3/2008. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi! *Amen!*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu inamshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoguswa na kulishughulikia suala la maafa haya, ujio wake Mererani tarehe 31/3/2008 kujionea hali halisi na kuwafariji wafiwa ni kielelezo tosha kwa jinsi alivyoguswa na janga hilo.

Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna alivyosimamia zoezi la kuwaokoa ndugu zetu walioathirika na maafa hayo. Pia tunamshukuru Mheshimiwa Spika na wewe binafsi pamoja na Bunge lako Tukufu, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Uongozi wa Mkoa wa Arusha, Wamiliki wa Migodi iliyoathirika, Wachimbaji wadogo, wadau katika Sekta ya Madini na wasamaria wema zikiwemo taasisi za kidini, kwa namna ambavyo kwa pamoja wameshiriki kwa hali na mali katika zoezi linaloendelea la kuwatafuta wenzetu walioathirika na maafa hayo. Michango yenu tunaithamini na tutaienzi daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela na wananchi wa Kyela kwa ujumla kutokana na mafuriko yaliyoikumba Wilaya yao. Kwa heshima na uzito huo huo natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wanaowawakilisha kwa Majimbo ama sehemu au maeneo yaliyokumbwa na mafuriko na kusababisha maafa au uharibifu wa mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wenzetu, Waheshimiwa Benedict Ole-Nangolo, aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto hivi karibuni kwa kura za kishindo na pia Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi Wizara ya Nishati na Madini tunawaahidi ushirikiano mzuri ili kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha Muswada huu ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa nimebeba dhamana ya Wizara

ninayoiongoza. Nakuomba uniruhusu niitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunituua mimi na Naibu Waziri wangu, kumsaidia kuitumikia nchi yetu kupitia Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, nakuomba upokee shukrani zetu kwako lakini pia kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi mnavyoendelea kutuunga mkono kwa kutushauri na kutuelekeza pale inapobidi kufanya hivyo ili kutimiza wajibu wetu, tunasema ahsanteni sana.

Vilevile tunavishukuru vyombo vya habari kwa jinsi ambavyo vimekuwa vikitoa taarifa kwa umma kuhusu shughuli za Wizara yetu na kutukumbusha pale inapobidi sisi Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara yetu kutimiza wajibu wetu ipasavyo. Tunawaahidi wenzetu wa vyombo vya habari kuendeleza ushirikiano uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitumia fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu na wananchi wenzangu wa Jimbo la Sengerema na Watanzania kwa ujumla kwamba mimi na Wizara yangu tutajitahidi kwa maarifa na uwezo wetu wote kuwatumikia Watanzania kwa maslahi ya taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulipata fursa ya kujadiliwa na wadau wa sekta ya mafuta na petroli nchini chini ya usimamizi wa iliyokuwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Kamati ya Nishati na Madini kwa sasa.

Michango na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwenye Semina tuliyofanya chini ya usimamizi wa Kamati ya Nishati na Madini Machi, 2008 imetusaidia sana kutayarisha Muswada huu. Tunaishukuru sana Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge na Makamu wake, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kwa jinsi wanavyotushauri. Kwa ujumla wadau walikubaliana na hoja ya kutunga sheria mpya ya kusimamia Sekta ya biashara ya mafuta ya petroli na kwa kiasi kikubwa tumechukua na kutumia maoni tuliyopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudiwa kutungwa kwa Sheria mpya ya kusimamia baishara ya mafuta ya petroli nchini ambayo itakidhi mahitaji ya mazingira ya sasa ya kiuchumi na kijamii. Hivi sasa biashara ya mafuta ya petroli na bidhaa zake inasimamiwa na Sheria ya Petroli, Sura ya 392. Sheria hii ina upungufu unaokusudiwa kurekebishwa kwa kutungwa kwa sheria mpya.

Sheria hii ilitumika zaidi wakati wa uhaba mkubwa wa fedha za kigeni na pia wakati wa bei za mafuta katika soko la dunia zilipopanda kwa ghafla katika miaka ya 1980. Msisitizo mkubwa katika sheria hiyo ya sasa uliwekwa katika kubana matumizi ya mafuta kama sehemu ya mkakati wa kupunguza matumizi ya fedha za kigeni bila kuzingatia ipasavyo masuala muhimu kama ubora wa bidhaa, usalama wa watu na mali zao na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya sasa ina upungufu ufuatao:-

Kwanza, inalenga zaidi kubana au kupunguza matumizi ya mafuta ambapo athari zake kiuchumi ni kubwa na sasa haiendani na Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003.

Pili, haikuweka mazingira bora ya kuruhusu wawekezaji binafsi kuwekeza kwenye sekta ndogo ya petroli kwa kuzingatia ubora na ushindani ambavyo havikuwa vigezo vya kuzingatiwa wakati wa mfumo wa uchumi wa miaka 1970 na 1980.

Tatu, haikuweka usimamizi thabiti wa ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli yanayotumika nchini.

Nne, haikuzingatia kwa uwazi suala la mazingira na usalama wa watu, vifaa, mitambo na mfumo wa usambazaji.

Tano, hakuweka wazi taratibu za kukusanya taarifa na takwimu muhimu kwa ajili ya kuratibu maendeleo ya sekta ndogo ya petrol nchini.

Sita, haikuhusisha vyanzo vingine vya mafuta vinavyoendelea kujitokeza kutokana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia kama vile *Bio-fuel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungu huo sheria hiyo inakusudiwa kufutwa na inapendekezwa kufutwa kwa Sheria mpya itakayoweka masharti bora ya usimamizi wa biashara ya petroli na bidhaa zitokanazo na petrol nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu ndani ya muswada huu, umezingatia mambo muhimu ya fuatayo:-

(a) Kuainisha na kutenganisha mamlaka na kazi za Waziri mwenye dhamana ya kusimamia biashara ya mafuta ya petroli na mamlaka na kazi za Mdhidhi wa masuala ya Nishati na Maji (*EWURA*).

(b) Kukitambua *EWURA* kama chombo huru kinachosimamia masuala yote ya kiufundi, usalama na kiuchumi katika uendeshaji wa biashara ya mafuta (*technical, soft and economic regulation*).

(c) Kutambua kuwepo kwa ushindani wa haki (*fair competition commission*) kama chombo huru cha kusimamia biashara ya ushindani katika sekta hii ndogo.

(d) Kuhakikisha kwamba biashara ya mafuta inazingatia usalama wa watu, mali, vyombo vya usafiri, miundombinu na uhifadhi wa mazingira.

(e) Kuweka taratibu za kukusanya na kuhifadhi taarifa muhimu za sekta ndogo ya petroli.

(f) Kuzingatia umuhimu wa kuwa na hifadhi ya mafuta ya akiba nchini (*strategical reserve*) na hatua za kuchukua wakati wa dharura ili kuhakikisha taifa linaendelea kupata mafuta.

(g) Kutambua kuwepo kwa vyanzo vya mafuta kama *Bio-fuel* na *sythetic fuel* ambayo yanaweza kutumika pamoja na mafuta ya petroli kwa faida ya nchi.

(h) Kuainisha adhabu mbalimbali stahili zitakazotolewa pindi ukiukwaji wa sheria inayopendekezwa utakapotokea; na

(i) Kuitumia *TPDC* kama *checks and balances* kwa makampuni mengine ambayo yanafanya biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yatu katika hili kwamba *TPDC* kama chombo cha umma, kikiruhusiwa na kuwezesha katika biashara ya mafuta kama makampuni mengine, itatupa nafasi nzuri ya kufahamu mwenendo wa biashara ya mafuta na itakuwa ni rahisi kupitia hesabu zake na kutuwezesha kubaini iwapo kuna udanganyifu wowote katika biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mswada huu umegwanyika katika sehemu kuu kumi na mbili.

Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaojumuisha jina la sheria na kuanza kutumika kwa sheria hiyo. Pia inatoa tafsiri ya baadhi ya misamiati na maneno muhimu yaliyotumika kwenye sheria.

Sehemu ya Pili inawekwa masharti yanayohusu mamlaka na kazi ya Waziri mwenye dhamana ya kusimamia biashara ya mafuta ya petroli nchini. Sehemu hii pia inaainisha kazi ya mamlaka ya mdhibiti wa sekta za nishati na maji (*EWURA*).

Sehemu ya tatu inahusu utaoaji wa leseni za uendeshaji wa biashara ya petroli na utaoaji wa vibali au ruhusa kwa maana ya ujenzi wa vituo vya kuuzia petroli na miundombinu ya kuhifadhi petroli. Sehemu hii pia inaainisha taratibu za kufuata pindi mtu anapotaka kutuma maombi ya leseni.

Sehemu ya nne imeainisha masuala yanayohusu ujenzi wa mabomba ya kusafirishia petroli na usafirishaji wa petroli na gesi. Sehemu hii pia ina masharti ya utaoaji wa leseni na vibali kwa ajili ya shughuli zilizoainishwa chini ya sehemu hii.

Sehemu ya tano inahusu haki na wajibu wa mtu yeyote anayemiliki leseni au kibali. Pia ina vifungu vinavyomtaka mmiliki wa leseni kuheshimu sheria za nchi kufanyiwa upekuzi pale itakapohitajika na pia kutoa taarifa kama itakavyoelekezwa.

Sehemu ya sita inahusu masuala ya ushindani wa haki. Sehemu hii pia inakataza shughuli zozote zinazokiuka kanuni za ushindani wa haki.

Sehemu ya saba inahusu vifungu vya usalama wa jamii na mazingira kwa kuzingatia sheria husika. Sehemu hii inapendekeza matumizi ya viwango vya usimamizi

vya kimataifa na vifungu vinavyohusiana na namna ya kushughulikia uharibifu wa mazingira pindi utakapotokea.

Sehemu ya nane inahusu masuala ya bei za petroli na bidhaa zake. Pia sehemu hii inaweka masharti ya uzingatiaji wa soko huria. Pamoja na hayo sehemu hii inafungua milango kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia bei za huduma kwa walaji kutokana na mazingira husika.

Sehemu ya tisa inahusu masuala ya uagizaji, usafirishaji, uhifadhi, ugeuzaji na usambazaji wa petroli na bidhaa zake. Sehemu hii inampa Waziri mamlaka ya kuanisha vigezo vya petroli itakayosambazwa nchini.

Sehemu ya kumi inaainisha makosa na adhabu mbalimbali zitakazotolewa chini ya sheria inayopendekezwa kutungwa pindi ukiukwaji wa sheria hiyo utakapotokea.

Sehemu ya kumi na moja inahusu utatuzi wa migogoro na ukataji wa rufaa chini ya sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya kumi na mbili inahusu masuala ya jumla kama vile kufutwa kwa Sheria ya Mafuta ya sasa, Sura ya 392, mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na masuala ya mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti au Msemaji wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO – MSEMaji WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Muswada wa Sheria ya Biashara ya Mafuta wa mwaka 2007 (*The Petroleum Bill, 2007*) unaokusudia kufuta Sheria ya Petroli ya mwaka 1981, Sura ya 392, yenye upungufu mkubwa unaokusudiwa kurekebisha, pamoja na kuweka masharti ya jumla na ya mpito kwa sheria inayofutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa niaba ya Wajumbe wenzangu kwa kututeua kuwa Wajumbe wa Kamati Mpya ya Nishati na Madini. Kamati hii imetokana na kuvunjwa kwa iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, ambayo imesababisha kuwepo kwa Kamati mbili yaani, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara. Mimi na Wajumbe wenzangu tumejipanga ipasavyo katika kuisimamia na

kuishauri Serikali katika kutekeleza majukumu yake katika sekta hii ya Nishati na Madini. Tunakuahidi wewe pamoja na Serikali kutoa ushirikiano wa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na wananchi wote wa Mkoa wa Manyara na mingine, kufuatia maafa yaliyowapata wachimbaji wadogo wa Madini ya *Tanzanite* huko Mererani na kusababisha vifo vya watu takriban 74 na wengine kutojulikana waliko. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa Muswada huu uliwahi kujadiliwa na iliyokuwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na ulitarajiwa kuwasilishwa Bungeni Januari, 2008. Kwa kutambua umuhimu wa Muswada huu, Kamati yangu ilitekeleza kazi ya kuujadili kwa mara nyingine katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam, tarehe 2 Aprili, 2008, chini ya Kamati mpya ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyokusudiwa yaliyowasilishwa na Mhe. William M. Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, maoni ya Wadau, Waheshimiwa Wabunge pamoja na maoni ya Kamati katika Muswada huu yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuupitia Muswada huu kwa lengo la kuuboresha katika hatua za awali, Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali kwa majadiliano ya kina kuhusu Muswada wenyewe. Majadiliano hayo yalisaidia sana kuibua mawazo mapya, maoni na hoja nzuri za kuuboresha Muswada huu. Kamati ya Nishati na Madini pia ilipokea maoni kwa njia ya maandishi kutoka kwa wadau yaani wafanyabiashara wa mafuta, maoni yenye changamoto nyingi ndani ya biashara hii ya mafuta. Nakiri kuwa maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu ni matokeo ya mchakato huo wa kubadilishana mawazo na Wadau. Napenda kuwashukuru wadau kutoka BP-Tanzania na Umoja wa Wafanyabiashara ya Mafuta Tanzania pamoja na wadau wote ambao waliitikia mwaliko wa Kamati na kuja kutoa maoni yao kwa lengo la kuuboresha Muswada ulio mbele yetu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kueleweka kwa muswada huu kwa Waheshimiwa Wabunge ni matokeo pia ya Semina iliyotolewa na Wizara ya Nishati na Madini kupitia mada mbalimbali ambazo zilitolewa kwenye Semina hiyo.

Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara, Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Maendeleo la Petroli (*TPDC*) na Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji (*EWURA*) ambao walifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha Wabunge juu ya Muswada ulio mbele yetu. Tunawashukuru kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuweka masharti bora ya usimamizi wa biashara ya petroli na bidhaa zitokanazo na petroli nchini kutokana na mabadiliko ya kisheria na changamoto zilizojitokeza hivi karibuni katika kusimamia usambazaji wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Taarifa ya Bunge lako Tukufu, Sheria hii kwa kiasi kikubwa imezingatia mambo muhimu ambayo hayakuzingatiwa kwenye Sheria inayofutwa:-

(i) Kubaini na kutenganisha mamlaka na kazi za Waziri mwenye dhamana ya kusimamia biashara ya mafuta ya petroli na Mamlaka na kazi za *EWURA*.

(ii) Kuitambua *EWURA* kuwa chombo huru kinachosimamia masuala yote ya kiufundi, usalama na kiuchumi katika uendeshaji wa biashara ya mafuta (*technical, safety and economic regulation*);

(iii) Kutambua kuwepo kwa Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission*) kama chombo huru cha kusimamia biashara ya ushindani katika sekta;

(iv) Kuhakikisha kwamba biashara ya mafuta inazingatia usalama wa watu, mali, vyombo vya usafiri, miundombinu na hifadhi ya mazingira;

(v) Kuweka taratibu za kukusanya na kuhifadhi taarifa muhimu za sekta ya mafuta;

(iv) Kuzingatia umuhimu wa kuwa na Hifadhi ya Mafuta ya Akiba Nchini (*Strategic Oil Reserve*) na hatua za kuchukua wakati wa dharura ili kuhakikisha Taifa linaendelea kuwa na mafuta;

(v) Kutambua kuwepo kwa vyanzo vingine vya mafuta kama yatokanayo na mazao mbalimbali (*biofuel and synthetic fuels*) ambavyo vinaweza kutumika pamoja na mafuta ya petroli kwa faida ya nchi; na

(vi) Kuainisha adhabu mbalimbali zitakazotolewa kwa ukiukwaji wa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati yangu inakubaliana na Muswada huu, kwanza, kwa kuzingatia kuwa sheria hii inakusudia kuboresha mazingira ya uwekezaji ili yaendane na wakati kwa kuruhusu wawekezaji kwenye biashara ya mafuta. Pili, kwa kuzingatia kuwa ushauri tulioutoa katika kikao cha Kamati ulikubaliwa na Serikali na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unafuta dhana ya kuwa uingizaji wa mafuta ya petroli na bidhaa zake utafanywa na wawekezaji binafsi (wenye kampuni za mafuta) isipokuwa iwapo uingizaji utafanywa kwa njia ya uagizaji wa pamoja (*efficient procurement*) kama inavyoelezwa kwenye Ibara ya 33(1) ya Muswada.

Kamati inashauri kuwa masharti yote yatakayotungwa na Waziri kwenye Kanuni kwa lengo la kuweka taratibu bora za kusimamia uingizaji wa mafuta chini ya utaratibu wa uagizaji wenye ufanisi (*efficient procurement*), Kanuni hizo zieleze wazi namna njia hiyo itakavyotumika. Aidha, katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti kwa

wanaokwenda kinyume cha sheria, Kamati inashauri kuwa Kanuni ziainishe wazi adhabu zitakazotolewa kwa watakaokiuka sheria. Ni dhahiri kuwa sheria zinatungwa ili zitoe mwelekeo bora wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali, ni kwa mantiki hiyo Kamati imefarijika na kuwepo kwa Ibara ya 45 mpaka 49 katika Sehemu ya Kumi ya Muswada inayoainisha makosa na adhabu zitakazotolewa kwa watakaokiuka taratibu husika. Sisi tunaamini kuwa hakuna uchumi wa nchi yoyote ambao hauongozwi na sheria, kanuni na taratibu na kwamba watakoadhibiwa ni wale tu watakoendesha biashara zao kinyume na Kanuni zitakazowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria hii pia Kamati ilitafakari kwa undani Ibara 42(2) ya Muswada huu inayotamka adhabu itakayotolewa kwa watakoachanganya mafuta (kuchakachua) kinyume na utaratibu utakaowekwa kwa mujibu wa viwango vitakavyowekwa na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria inayopendekezwa. Ni maoni ya Kamati kuwa kifungu hiki kijumuishe adhabu ya kunyang'anya leseni na Waziri kuandaa Kanuni zitakazoelekeza *EWURA* kushughulikia bidhaa hiyo kwa mujibu wa taratibu zinazozingatia hifadhi ya mazingira na kuzuia athari zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imezingatia kuwa hakuna takwimu sahihi zinazobainisha ni kiasi gani cha mafuta yameingizwa nchini kutokana na Kampuni mbalimbali za mafuta kuwa zinaagiza na kuingiza mafuta nchini zenyewe. Hii imetokana na kutokuwa na udhibiti maalumu wa uingizaji huo.

Kamati inaamini kwamba mfumo wa kuagiza mafuta kwa wingi kwa pamoja (*bulk procurement*) utasaidia kutatua tatizo la upungufu wa mafuta na kupanda kwa bei ya mafuta kusikotabirika. Aidha, kuanzishwa kwa ghala au utaratibu wa kuweka taarifa za mafuta (*National Petroleum Information System*) kutasaidia utoaji wa taarifa sahihi kuhusiana na kiasi cha mafuta yaliyopo sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) limepewa jukumu la kusimamia na kuhifadhi mafuta ya petroli na bidhaa zake kwa kuweka Hifadhi ya Mafuta ya Akiba Nchini (*National Strategic Oil Reserve*) kama inavyoelezwa kwenye Ibara ya 30(3) ya Muswada huu. Ni maoni ya Kamati kuwa hifadhi hiyo ya mafuta ya Taifa itasaidia soko la petroli kuwa katika hali nzuri. Kwa mtazamo huo, Kamati ina maoni kuwa ni vema miundombinu ya Shirika la Tanzania na Italia la Kuchakata Mafuta (*TIPER*) iboreshwe vizuri na kutumika kuweka Akiba ya Taifa ya Mafuta (*National Strategic Oil Reserve*) chini ya uangalizi na usimamizi wa *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na malengo mazuri ya Muswada huu, mafanikio yake hayataonekana ikiwa Wadau hawataelimishwa vizuri jinsi ya kufanya biashara ya mafuta kwa kuzingatia Sheria hii na taratibu kwa maslahi yao na Taifa zima. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara, Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa ngazi mbalimbali kuwaelimisha wananchi waelewe vizuri Sheria hii mpya, waipokee ili waweze kufaidika nayo. Aidha, wadau wahakikishe kuwa wanaipata Sheria hii na kuitumia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali kuwa Kamati imefarijika na kuwepo kwa Sheria hii. Ni ushauri wa Kamati kuwa tathmini za athari za kiusalama na kimazingira zifanyike ili kubainisha maeneo yatakayohifadhi mafuta (*strategic installation*). Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa mafuta wanakuwa na bima itakayomjali na kumlinda mtu atakayeathirika kutokana na matatizo yoyote yatokanayo na mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia majukumu ya Waziri kwenye Sheria hii na vikwazo linavyopata Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) katika kutekeleza baadhi ya majukumu yao chini ya Sheria inayofutwa, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inalipa nguvu za kutosha kisheria Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) ili liweze kufanya ukaguzi wakati wowote kwenye vituo na maeneo yote yanayohusika na usambazaji wa petroli na bidhaa zake. Hii itasaidia kuepukana na madhara yatokanayo na ujanja unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta katika kukwepa kodi au na kujitafutia faida kubwa ndani ya biashara hii.

Kamati inashauri kuwa Wataalamu wanaosimamia mashine za kupima mafuta (*Flow Meters*) wawe waaminifu na njia madhubuti na makini katika upimaji zizingatiwe. Vilevile Watumishi wanaosimamia mashine hizo walipwe vizuri ili wasishawishike kupokea rushwa. Pia wasikae kwa muda mrefu kwenye kazi hizo za mashine, yaani wasikae muda mrefu katika eneo moja la kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa sheria hii, pia Kamati inashauri kuwa miundombinu ya barabara pamoja na usimamizi thabiti wa *EWURA* na Tume ya Ushindani iboreshwe ili kusiwe na kisingizio cha kupandisha bei ya mafuta kutokana na umbali wa watumiaji hasa walioko mbali na Bandari za Tanga na Dar es Salaam. Kamati inaamini kwamba kiasi kikubwa cha kodi itokanayo na biashara ya mafuta inapotea kutokana na wafanyabiashara wa mafuta kukwepa kulipa kodi. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) kuhakikisha kuwa wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kujua kiasi gani cha mafuta yanaagizwa na kiasi gani yanaingia ili kubaini mapato ya Serikali yatokanayo na biashara ya mafuta. Aidha, usimamizi madhubuti wa uingizaji wa mafuta Kurasini *Oil Jet (KOJ)* uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inaelekeza suala la ukusanyaji kodi lifanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) au na Taasisi nyingine itakayotamkwa na Serikali. Kamati inashauri kwamba Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na *TRA* pamoja na Taasisi nyingine zitakazohusika kujipanga ipasavyo katika kusimamia suala la ulipaji kodi ya mafuta. Aidha, Akaunti ya Nishati (*Energy Account*) itakayoanzishwa iwe na usimamizi maalumu na mapato yatokanayo na akaunti hiyo yasaidie katika kuiendeleza *TPDC* ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefarijika na kuzingatia umuhimu wa kuanzishwa kwa Utaratibu wa Kutunza Taarifa za Mafuta Nchini (*National Petroleum Information System*) na Masijala ya Shughuli za Biashara ya Mafuta (*Central Registry of Petroleum Operations*) kama inavyotamkwa kwenye Ibara ya 21 na 23 za Muswada huu. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha uanzishwaji wa mamlaka hizo ufanyike haraka baada ya kuanza kutumika kwa Sheria mpya. Aidha, maandalizi ya Mpango wa

Upatikanaji wa Mafuta wakati wa Dharura (*Petroleum Emergency Supply Plan*) yahusishe pia maoni kutoka kwa wadau wa masuala ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, Kamati inapenda kuushukuru uongozi wa Wizara kwa kukubali kufanya Semina kwa Wabunge wote, Semina iliyoibua michango na mawazo mapya yaliyosaidia kuboresha Muswada huu. Tunawashukuru pia kwa kuzingatia na kupokea ushauri wa Kamati moja kwa moja wakati wa mchakato wa kuchambua na kuujadili Muswada huu kwenye Kamati. Aidha, maeneo mengine kwenye Muswada huu yalifanyiwa marekebisho na Kamati, na Serikali kuyakubali. Kwa hiyo, Kamati imeridhishwa na marekebisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Muswada ulio mbele yetu. Pia namshukuru Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake Mheshimiwa Adam K. Malima, (Mb.), kwa kuwasilisha vema muswada huu kwenye Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu Arthur Mwakapugi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti na Usimamizi wa Nishati (*EWURA*,) Ndugu Haruna Masebo, Mkurugenzi Mkuu wa *TPDC*, Ndugu Yona S. Kilaghane na wataalamu wote kutoka Wizara ya Nishati na Madini, *EWURA* na *TPDC* kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipokutana kuujadili muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa ujasiri, umahiri na michango yao ya kina iliyoboresha muswada huu. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mheshimiwa Mohammed H.J. Mnyaa, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi , Mheshimiwa Dk. James A. Msekela, Mheshimiwa Omar Shekha Mussa , Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa , Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, maarufu kama Mzee wa CHADEMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashillilah na Ofisi yake kwa kuiwezesha Kamati yetu kufanya kazi bila matatizo yoyote. Mwisho, naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Emmanuel Mpanda, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuhudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono muswada huu, na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuwa hapa ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Pili, natoa shukrani zangu kwako binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Biashara ya Mafuta wa mwaka 2007 (*The Petroleum Bill, 2007*) kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6)(c) na 86(6), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa niaba ya Kambi ya Upinzani natoa pongezi kwa wabunge wapya wote waliopata bahati ya kuwa pamoja nasi katika kazi ya kuwawakilisha wananchi. Aidha, tunatoa salamu za rambi rambi kwa ndugu na jamaa wa familia za marehemu wote waliofariki katika migodi ya Mererani hivi karibuni. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira. *Amen!* Aidha, kutokana na neema ya mvua, tunawapa pole wananchi wote waliopata adha kutokana na mafuriko katika maeneo yao na hususan, tunatoa pole kwa Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe pamoja na wananchi wa Kyela kutokana na adha ya mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya kutungwa kwa sheria hii ni nzuri kabisa, na sisi kama Kambi ya Upinzani hatuna shida nayo, japokuwa kuna baadhi ya vifungu ambavyo tunadhani bado vinatakiwa kuwekwa vizuri ili visitoe mkanganyiko katika utekelezaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5(1) cha muswada kinachosema kuwa, nanukuu: *“the authority shall perform technical, economic and safety regulatory functions in respect of petroleum supply,”* Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni kwa jinsi gani *EWURA* kama mamlaka itakavyofanya *“economic regulatory functions”*.

Kifungu cha 5(2)(f) kinachosema kuwa mamlaka ndicho chombo kitakachokuwa na uwezo wa kuidhinisha ushuru wa forodha na bei, dhana nzima ya kifungu hiki ni nzuri lakini pia tuangalie hali halisi ilivyo katika dunia hii ya utandawazi au soko huria ambapo bei hupangwa na nguvu za soko. Kambi ya Upinzani inaona kifungu hiki kiondoe neno *“and prices”* ili bei ya mafuta iendane na gharama za uendeshaji pamoja na bei ya ununuzi wa bidhaa hiyo toka kwa wazalishaji na si kupangwa na mamlaka, vinginevyo iwepo Tume ya Bei kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 31(1) cha muswada kinaungana na yale tuliyotoa kuwa bei katika bidhaa za mafuta ziwekwe na nguvu za soko (*forces of supply and demand*). Kwa mantiki hii ni vyema Serikali iweke wazi ni kifungu kipi kitatumika badala ya kuwachanganya wale wote watakaotumia sheria hii kwenye masula yahasuyo bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6 kinachohusu adhabu kwa mtu/kampuni kukiuka masharti ya kifungu cha 5, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa vyema kwa adhabu zilizotajwa kwenda pamoja yaani faini na kifungu badala ya kuchagua adhabu moja tu. Aidha, mapendekezo kama hayo pia yawe kwa vifungu vya 40(2) na 43(3).

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya 11(1)(2) vinavyohusu kuhamisha leseni, kabla ya kufanya hivyo kwanza ni lazima kupata idhini kutoka kwenye Mamlaka. Kambi ya Upinzani inaona mchezo huu wa kuhamisha leseni kwa idhini ni ishara tosha ya ubabaishaji, hivyo ni bora sheria itamke wazi kuwa kama mwenye leseni atashindwa kukidhi matakwa ya leseni yake awe ameshindwa na leseni hiyo ifutwe badala ya kuhamishiwa kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchezo huu wa kuhamisha leseni ndio unaleta utapeli kwa wafanyakazi na kusababisha migogoro isiyokwisha ya waajiri na wafanyakazi na kupelekea wafanyakazi kuona kama Serikali inashirikiana na wawekezaji hao wababaishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 24(1) na kifungu cha 33(1) vikisomwa kwa pamoja vinaleta mkinzano kwa njia moja ama nyingine. Kwani kifungu cha 24(1) kinasema: “washiriki wote katika biashara ya mafuta, ununuzi na uuzaji wa bidhaa hiyo wasibaguliwe kwa njia ya ubora, wingi pamoja na kwa bei au kwa yoyote ile na hii ni kwa mujibu wa sheria ya ushindani sawa katika biashara”. Wakati kifungu cha 33(1) kinazuia mtu yeyote kuagiza bidhaa ya mafuta nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 37 kinachohusu vigezo (*specifications*) kwa vyombo vitakavyosafirisha bidhaa za mafuta kuwa Mheshimiwa Waziri ndiye atakayeweka vigezo vitakavyotumiwa na vyombo vya kusafirishia bidhaa za mafuta, Kambi ya Upinzani inaona kwa hili itakuwa ni bora kama vigezo vitakavyotumiwa viwe vile vya Kimataifa (*international standards*), hili litaepusha migogoro kwa vyombo vya kusafirishia bidhaa za mafuta ambavyo vimesajiliwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema wachangiaji sasa ni watano na wenyewe ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Lucy Owenya. Sasa namwita Mheshimiwa Gosbert Blandes.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na hasa nikiwa mchangiaji wa kwanza. Mchango wangu ni mfupi.

Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, timu nzima ya Wizara ya Nishati na Madini kwa kuleta Muswada mzuri sana hapa Bungeni. Nasema hongereni sana. Na kabla sijasahau, naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kifungu Na. 5 cha Muswada na hii inahusiana sana na wenzetu wa *EWURA* ambao tumewapa mamlaka ya kutoa leseni. Sasa katika kifungu hiki, mimi *concern* yangu ni neno moja ambalo limetumika pale la

kitaalamu linasema “*may*.” Unaposema “*may*” kwenye kifungu, ni kwamba yule mtu unampa *option*, anaweza akafanya au asifanye. Sasa mimi nataka nipendekeze kwamba badala ya neno *may* ambalo limetumika kifungu namba 5, tulibadilishe liwe *shall* ili yule mtu awe na nguvu ya kufanya hilo jambo ambalo tunalikusudia kulifanya.

NAIBU SPIKA: Katika kifungu gani?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 5!

NAIBU SPIKA: 5, namba gani?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, niende tena kwenye kifungu namba 10(2) cha Muswada huu. Kifungu namba 10(2), kinapendekeza leseni itolewe kwa kipindi kati ya miaka 5 hadi 20, ndiyo mapendekezo ambayo tunayaleta hapa. Lakini kwa sasa hivi ni kwamba wenzetu wa *EWURA* wao tayari wanatoa leseni na naamini leseni hizo ni za miaka mitatu, mitatu. Sasa hapa napata *contradiction* tukisema 5 mpaka 20 katika hii sheria tunayoileta, wakati leseni zimekwishaanza kutolewa za miaka mitatu mitatu! Mimi nina mapendekezo kwamba kifungu hiki, kimsingi kibaki hivi hivi, isipokuwa ule muda wa kutoa leseni uwe kati ya ile miaka mitatu ambayo tumeianza hadi 20. Hayo ni mapendekezo katika kifungu namba 10(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba nigusie kifungu namba 9(4) cha Muswada huu ambao tunakusudia kuupitisha hapa Bungeni. Hii ni kuhusiana na maombi ya leseni kwa mwombaji na muda ambao maombi yake yanatakiwa yawe yamejibiwa.

Muswada huu unakuja kwa makusudi mazima ya kutaka kuboresha sekta ya mafuta hapa nchini. Sasa kwenye Muswada huu tunapendekeza kwamba mwombaji yeyote awe amejibiwa kwa kupewa au kukataliwa au kutolewa sababu nyingine maalumu ndani ya siku 40. Lakini kwa kuzingatia hali halisi tuliyonayo sasa hivi, na ili kuweza kuwapa hawa wenzetu wataalamu muda wa kutosha kujitosheleza kufanya *search* ya kutosha kumjua yule mwombaji, mimi naona hizi siku ni chache.

Napendekeza na ninashauri kwamba ili tuwape nafasi nzuri, basi tuwape miezi mitatu ambayo ni siku 90 kuanzia ile siku wanapopokea maombi hadi wanapowajibika kisheria kumjibu yule mtu kwamba amepata leseni au hajapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo itasaidia sana kuwawezesha hawa watu kujua ni mtu wa namna gani ambaye anawasilisha maombi kwao, vinginevyo tukiwapa siku 40, ni chache na wanaweza wakajikuta wameanza kutoa leseni nzito kama hizi kwa watu ambao ni *kanyaboya*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu hicho cha 9(4) ambacho napendekeza siku 90, nashauri kwamba mapendekezo haya ninayoyatoa ya siku 90, basi yaanze kutumika siyo *immediately* tunapopitisha sheria hii au baada ya kuwa *assented* na

President, tujipe muda, wajipange, ile *effective date* ianze baada ya mwaka mmoja baada ya sheria yenyewe kupitishwa ili wajipange vizuri kwa sababu sheria yenyewe ni mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nilizonazo binafsi ni kwamba tayari wenzetu wa *EWURA* wanayo maombi mengi sana, nadhani kwenye 400 hata 500 na watu wanaendelea kuomba na siamini kama tayari hayo maombi wamekwishayafanyia kazi. Sasa kwa hali hiyo nasema kwamba kwenye sheria hii ambayo tunaikusudia kuitunga, basi tuweke *provision* kama *transition period* ambayo itawapa hawa wenzetu nafasi ya kuweza kushughulikia haya maombi ambayo tayari yako mezani kwao. Vinginevyo tusipoweka kifungu hicho na maombi tayari yalikwishakuwa ofisini kwao, wanaweza wakajikuta kwamba wanakanganywa na sheria. Maombi yamekuwa mengi, yamelala pale na wakakurupuka, wakaanza kuvunja sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mimi kimsingi nimesimama hapa kuunga mkono hoja hii. Hoja ni nzuri na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karagwe, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Asante sana. (*Makofi*)

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nichangie katika Muswada huu wa usambazaji wa mafuta ambao ni muswada muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Lakini kabla sijafanya hivyo, ningependa kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe, nitume salamu zangu za rambi rambi kwa wananchi wa Mkoa wa Manyara na kule Kusini Kyela na kwingine kote ambako kumetokea matatizo na tukapoteza ndugu zetu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema peponi na wale ambao wamepata maumivu basi waweze kupona haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, katika mchango wangu, kwanza, ningeaanza kuipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla na taasisi zao kwa kuuleta Muswada huu ambao kama nilivyokwishasema ni muhimu sana katika uchumi wetu hususan katika maeneo ya uzalishaji na usafirishaji. Wananchi wangu wa Kisarawe kule kila inapopanda bei ya mafuta, basi na gharama za usafiri, nauli zinapanda na kwa kweli hawawezi kuzimudu hasa kule vijijini ambako barabara si nzuri sana. Kwa hiyo, kuuleta Muswada huu ambao nia yake kubwa ni kusimamia na kurekebisha kasoro mbalimbali, ni uokozi kwa mtu wa hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali vile kwa kuainisha majukumu ya taasisi zote husika zikiwemo Serikali yenyewe, *EWURA* na waendeshaji wa biashara ya mafuta. Katika Muswada huu kumewekwa mazingira ya ushindani, jambo ambalo litasaidia sana kuhakikisha kwamba bei zinatawaliwa kwa nguvu ya soko. Pia naipongeza Wizara kwa kuleta wazo la kuanzisha kuweka akiba ya mafuta, hatua ambayo itaisaidia sana nchi yetu kuepuka madhara yanayopatikana wakati unapotokea upungufu wa mafuta duniani au bei zinapopanda wakati bajeti zetu ni ndogo. Akiba za namna hii zitasaidia sana kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinaendelea nyakati hizo za matatizo. Wengi wetu tunakumbuka tuliyoypata katika miaka ya 1973, 1975, 1979 hadi 1984 wakati kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa mafuta duniani ambapo tulilazimika kufunga baadhi ya viwanda mpaka tukafika mahala ambapo tulikataza magari yasitembee baada

ya saa 8.00 kila siku ya Jumapili na kuuza mafuta kwa nyakati za mchana tu ili yaliyokuwapo kidogo yaweze kutumika. Sasa tukiwa na akiba za namna hii, nadhani hatua za namna hii hazitakuwa muhimu kuchukuliwa nyakati za matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali pia kwa kutaka kuanzisha Mfuko wa Nishati kwa madhumuni ya kuendeleza sekta hii. Pia katika Muswada huu yapo mazingira yanayoonyesha kwamba tegemeo letu kubwa lilikuwa mafuta katika kupata nishati za aina mbalimbali pamoja na kuzalisha umeme. Sasa wazo la kuangalia nishati mbadala kwa maana ya kuendeleza nishati ya mazao ya mimea, nafikiri ni jambo la busara sana ambalo litatufanya tusitegemee chanzo kimoja tu cha nishati katika huduma zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Muswada huu kueleza majukumu makuu ya taasisi mbalimbali, Muswada umetilia mkazo suala la usimamizi utakaotekelezwa na Mamlaka ya *EWURA* kama majukumu yalivyoorodheshwa katika *section 5(2)*. Chini ya kifungu namba 9, yameorodheshwa pia mambo yatakayozingatiwa katika kutoa leseni. Nafikiri utaratibu huu ni mzuri, utawezesha kuweka jukumu la kusimamia chini ya Mamlaka ambayo imeteuliwa kwa kazi hiyo. Ttunafurahi kuwa Serikali inaondokana na utaratibu wa kutoa leseni za mara kwa mara ambao unaleta usumbufu kwa wafanyabiashara kila leo kwenda kutafuta leseni. Kuweka kwamba leseni zitatolewa kati ya miaka 5 na 20, nafikiri ni jambo bora na litaondoa hata vishawishi vya kufanya watu watake kupewa rushwa kwa maana ya kila wakati wanapokuja kuombwa waweze kutoa leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo inawezekana wakawapo wafanyabiashara ambao wakitumia vibaya fursa hii kwa kuwa wanazo leseni za muda mrefu, basi wakaanza kufanya mambo ambayo yanakwenda kinyume na taratibu zilizowekwa. Lakini nafurahi kwamba katika *section 18(2)*, Mamlaka imepewa fursa ya kuwachukulia hatua za kufuta leseni wale wote ambao wataonekana wanavunja sheria. Mimi nafikiri hili ni jambo zuri litazuia mambo maovu ambayo yangeweza kufanywa. Sasa pamoja na kuipongeza Wizara kwa Muswada huu mzuri, yapo maeneo ambayo kwa kweli ningependa niyatolee maelezo na pengine Mheshimiwa Waziri angependa kufanya masahihisho. Kwanza, katika *section* ya 4, linazungumziwa jukumu la Waziri la kusimamia. Lakini katika *section* ya 4(c), Waziri anatakiwa atayalishe *plan*. Mimi nadhani hii ni kinyume na matarajio. Waziri kazi yake ni kusimamia siyo kutayarisha *plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri badala ya kusema "*The Minister shall prepare*", yatumike maneno "*The Minister shall cause to be prepared*", maana hiyo ni njia ya kusimamia, siyo yeye mwenyewe kukaa na kuanza kutayarisha ile *emergency plan*.

Kwenye jedwali la marekebisho, namshukuru Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia amezungumzia hili kwamba kumetolewa neno "*may*" likawekwa "*shal*" na mwenzangu akasema kwamba pengine lingerudishwa lile la "*shall*" lakini nadhani katika orodha hii

yapo mambo ambayo ni majukumu ya mamlaka kufanya. Kwa hiyo, yale yote yangetawaliwa na neno “*shall*” na yapo yale ambayo wanaweza wakayafanya wakitaka, au wakati mwingine sio lazima haya yangekuwa yanatanguliwa na neno “*may*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikieleza kwa haraka haraka, kwa mfano katika hiyo sehemu ya pili (a) unaweza ukaweka “*may*” (b) *shall* (c) *may* (d) *may* na (e) *shall* (f) *shall* na kadhalika mpaka mwisho.

Kwa hiyo, maana yake ni kwamba kuwe na vifungu vidogo viwili 5 (2) iseme kwamba, “*the authority shall...*” yakawekwa yale yatakayosemwa. Halafu kuwe na kifungu kile kidogo kitakachosema “*also...*” halafu wakaorodhesha yale ambayo sio lazima wakayafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea katika *section* ya 14(3) inasema: “*EWURA* itamjibu mwombaji kukubali au kukataa ombi lake la leseni katika siku 40.” Mheshimiwa aliyenitangulia naye amezungumzia muda, lakini mimi nalitazama vingine. Ili kibali kitolewe, nafikiri *EWURA* itabidi Bodi yake ikae. Sasa sioni ni namna gani Bodi inaweza ikakaa kila linapokuja ombi halafu baada ya siku 40 wapeleke. Nafikiri ingekuwa ni vizuri wangeweka muda wa kupokea maombi yote na halafu wakiweka *deadline* ndiyo kusema kwamba kuanzia siku ya mwisho ya *deadline* wao wajipe siku arobaini za kuweza kujibu, vinginevyo ama Bodi itakuwa inakaa kila siku ama sivyo wa-*delegate powers* zao kwa *Chief Executive* awe anakubali na kukataa kila baada ya siku arobaini. Mimi nafikiri wakilitazama hili litakuwa limekwenda sambamba ya madaraka ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika *section* ya 26(1) mstari wa pili yametumika maneno “*gradual adoption adaptation,*” mimi silipendi hili neno la “*gradual*” kwa sababu linakaribisha uzembe kama suala lenyewe ni kutaka kua-*adopt* kwa *international standards*, basi ingekuwa bora kuweka tu *programme of adoption and adaptation* kwa sababu *programme* lina *connotation* ya muda mrefu, siyo kitu cha mara moja tu. Ya pili, unaposema *gradual*, maana yake ni kwamba unaruhusu watu wengine wazembe katika ku-*adopt* na ku-*adapt*. Nafikiri walitazame vizuri na wakiliondoa neno hili, fungu hili litakuwa limekaa sawasawa.

Kwenye *section* ya 28(3) na (5) mwisho wa *section* kuna maneno yanasema: “*Recover the costing card in accordance with relevant laws*”, hivi tunaogopa nini kuzitaja zile sheria? Mimi nadhani teseme: “*Cost will be recovered from the owner (au holder of the operations)*”, au sivyo kuzitaja hizo sheria zenyewe ili kuhakikisha kwamba hakutakuwa na tafsiri mbalimbali ya sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jedwali la marekebisho *section* ya 43(2) kuna neno limetumika, “*shall*”, limerekebishwa na “*may*”. Kwa kufanya hivyo, nadhani hiyo haitasomeka vizuri kama umeliacha lile neno “*every*”. Haiwezekani kusema “*every*”, naomba nilisome jinsi lilivyo. “*Every unused capacity may be open to licensees in the manners related under this Act.* Mimi nafikiri hiyo ni sawa sawa, ama uondoe hilo neno “*every*” na useme “*any unused capacity may*” au sivyo, acha yote, anzia tu “*unused*”

capacity may be open to other licensees in the manner related under this Act.” Nafikiri hapo lugha itakuwa imekwenda vizuri na inaeleweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya kusema hayo sina haja ya kugongewa kengele ya pili na napenda kurudia kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Petroli. Lakini kabla sijaanza, naomba kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Muheza, nitoe salamu za rambirambi kwa ndugu zetu wa Mkoa wa Manyara na vilevile Mkoa wa Mbeya kwa kupata madhara makubwa ya mafuriko na vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa shukrani na kuwapongeza sana Naibu Waziri pamoja na watendaji wote katika sekta hii ya mafuta ambayo wameshiriki katika kuandaa muswada huu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu nitauzungumzia katika maeneo makubwa mawili. Kwanza, madhumuni makubwa ya muswada huu. Shabaha yangu nafahamu Waheshimiwa Wabunge walishiriki katika semina ile na wengi wetu tumeamini na tumekubali na bila shaka tutaunga mkono Muswada huu uweze kupitishwa. Lakini tutazungumza hayo kwa faida pia ya wananchi ambao hawakuweza kuhudhuria katika semina ile ili nao waelewe maana na nia hasa ya Muswada huu na faida zake. Kwa hiyo, nitazungumza katika maeneo makubwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtangi kabla ya kuwa Mbunge, alikuwa anauza mafuta huko *TPDC*. *(Kicheko)*

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mafuta yote yaliyokuwa yanakuja nchini hapa, mimi nilikuwa katika Idara ile na nilikuwa nahusika katika kuagiza mafuta yote yaliyokuwa yanakuja nchini kwa kiwanda cha *Tipper* na baadhi ya mafuta yaliyokuwa yanasafishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo nitakayozungumzia katika Muswada huu ni katika eneo la kwanza la ufanisi katika ununuzi wa mafuta kwa kiwango kikubwa yaani, *bulk purchasing* na nitazungumza ili wananchi waweze kufahamu faida zake ni nini hasa. Unaponunua mafuta kwa kiwango kikubwa kwa wakati mmoja na kusafirisha kwa wakati mmoja, unapata nafasi ya kuweza kupata bei nzuri. Wengi tunaofanya biashara tunafahamu *discount* inatolewa kutokana na kiwango kikubwa cha kiasi cha mafuta au bidhaa unayotaka kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukinunua kiwango kikubwa zaidi unapata *discount* kubwa zaidi. Kwa hiyo, kwa mfumo huu wa *bulk purchasing*, uwezekano wa kufanya bei zikashuka za gharama za kununulia mafuta ni mkubwa zaidi. Kwa hiyo, hayo ni manufaa makubwa ya kwanza ambayo Taifa hili litapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, unaponunua mzigo mkubwa utatumia meli kubwa kuleta mafuta na kwa msingi huo huo wa kiwango kikubwa cha mafuta maana yake gharama za usafirishaji pia zitapungua.

Vile vile, unapokuwa umeleta mafuta kwa niaba ya kampuni saba au kumi za mafuta ambazo kwa mpango huu wa sasa kila kampuni inaagiza mafuta yenyewe na kuleta kwa meli yake yenyewe, maana yake ni kwamba kama wiki iliyopita wakati semina hii ilipokuwa ikiendeshwa pale Dar es Salaam, bandarini zilikuwepo zaidi ya meli tano zilizokuwa zinaleta mafuta kwa ajili ya makampuni tofauti matano ya mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupakua mzigo wa tani elfu ishirini kwa mfano, meli moja inachukua zaidi ya siku nne. Kwa hiyo, meli zile nyingine tano zitasubiri na hazisubiri bure, zipo gharama za meli kukaa bandarini na kwa vyovyote hizi gharama zote ambazo meli zinakaa kusubiri ili ziweze kupakua pale, baadaye zinapitishwa hizo ndani ya bei ya mafuta ili kufidia hizo gharama kwa wale wanaoagiza mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, meli zikikaa pale ni lazima tuelewe dakika za mwisho anayelipia gharama zile ni wewe unayekwenda kununua mafuta kwenye kituo pale kwa sababu walioagiza watataka kufidia gharama zao zote.

Faida nyingine kubwa ni kwamba tunapunguza gharama za usimamizi kila meli tano. Gharama za kusimamia meli tano ni tofauti na gharama za kusimamia meli moja kubwa iliyoleta mzigo mkubwa kwa ajili ya makampuni yote ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine ni kwamba ni rahisi kusimamia udhibiti wa ubora wa mafuta mnayoleta nchini yanayokuja kutoka kwenye *refinery* moja au sehemu moja. Ni rahisi kujua kiwango cha mafuta yale na ni rahisi kusimamia kwa sababu baada ya kufanya ukaguzi mafuta yale yanakwenda kwa matumizi ya wananchi wote badala ya kila kampuni kuleta mafuta yake peke yake. Sio rahisi kusimamia udhibiti na ubora wa mafuta. Kwa hiyo, nimezungumzia hii *bulk purchasing* ili wananchi wajue faida yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ambayo nataka niizungumzie na nijaribu kuonyesha faida zake. Ndani ya Muswada huu sehemu ya pili, inazungumzia uwezekano wa kuwa na hifadhi maalumu ya mafuta, *Strategic Storage* ni nini manufaa yake? Ukitaka kujua manufaa ya hili jambo ni lazima tuangalie historia ya matukio ambayo yametokea.

Hapa kwanza tujikumbushe kwamba upo wakati vita vilitokea katika Ghuba ya Uajemi ambako ndiko mafuta yanakotoka na kwa hiyo, kukawa na athari za usafirishaji wa mafuta. Tunakumbuka *Suez-Canal* wakati fulani ilifungwa na hivyo meli hazikuweza kupita kuweza kuleta mafuta kwetu. Je, suala kama hilo likitokea na ninyi hamna akiba, nchi itafikia wapi? Hata kama mafuta yapo, lakini njia ya kuyafikisha hapa hakuna. Kwa hiyo, upo umuhimu wa kuwa na *strategic reserve* ili yaweze kutusaidia wakati wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaweza kutokea vita vya ghafla. Kuna wakati tuliwahi kuingia katika vita hapa na Uganda. Matatizo makubwa yalitokea, kiwango cha matumizi ya mafuta kutokana na vita kiliongezeka. Sasa kiwango kinaongezeka ghafla kwa sababu ya vita na kama hamna hifadhi ya mafuta na tusipokuwa waangalifu hata vita inaweza ikatushinda na nchi ikatekwa kwa sababu hatuna hifadhi ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta ni muhimu katika vita, kwa sababu ndege zinahitaji mafuta, vifaru, magari yote yanahitaji mafuta. Kwa hiyo, huo ni umuhimu wa kuwa na mkakati wa hifadhi maalum ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ushauri wangu sasa katika mambo haya mawili? Katika *bulk purchasing*, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri baada ya sheria hii kufikia hatua muhimu ikapitishwa na baadaye ikatiwa saina na Mheshimiwa Rais, hatua itakayofuatia sasa ni Waziri kukaa chini na kutengeneza utaratibu na kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo.

Wakati huo utakapokuwa umewadia, ushauri wetu ni kwamba, Wizara inayohusika pamoja na viongozi wote katika sekta hii tuwashirikishe wadau wanaohusika ili tufahamu kwamba kama ni *TPDC* ndiyo itakuwa imeteuliwa na ninaamini kuwa itakuwa imeteuliwa kuwa msimamizi wa utekelezaji wa mfumo huu wa ununuzi wa mafuta kwa jumla, kwa pamoja basi kuwe na utaratibu mzuri utakaokuwa wazi na ushirikishe wadau wote. Kwa maana hiyo, ni makampuni yote ya mafuta yaliyopo hapa nchini ambayo ndiyo watakaopata mafuta hayo kutoka katika chombo kitakachoundwa ili waweze kujua utaratibu gani na mpango utakaotumika, ninaamini kwamba *bulk purchasing* au ununuzi wa mafuta utafanywa kwa mpango uliokuwa wazi na mpango wa tenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, waelewe utaratibu wa tenda utakuwa vipi waelewe ni wakati gani tenda zitawekwa, waelewe ni utaratibu gani au ni makampuni gani yatashirikishwa au itakuwa ni tenda zilizokuwa wazi kwa mtu yeyote kuweza kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuweze kuhakikisha kwamba ni utaratibu gani makampuni gani ya mafuta baada ya mzigo ule au shehena ya mafuta baada ya mzigo ule au shehena ya mafuta kufika nchini watakavyoshiriki katika kulipia gharama na kununua mafuta hayo kutoka katika chombo hicho kitakachokuwa kinasimamia utekelezaji wa mpango huu ambapo ninaamini itakuwa ni *TPDC* na kama sivyo, basi kuna chombo maalumu kitakachokuwa kinasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni katika *storage*. Katika *storage* ni nini ushauri wetu? Ushauri wetu ni kwamba tuangalie, kwanza tunahitaji kuwa na *storage* ya kutosha kwa sababu tunahitaji kununua mafuta mengi kwa wakati mmoja, lakini ukitazama mahali ambapo tunapakulia mafuta pale wanaita Kurasini *Oil Jet*, *Jet* hii ni moja tu na ni hatari kwa sababu lolote linaweza kutokea, *Jet* ikagongwa ikaharibika, meli ziko nje haziwezi kupakua mafuta. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba wakati

tunafikiria mahali tutakapohifadhi mafuta, lakini vilevile ni lazima tufikirie jambo la pili, ni mahali gani tutaweza kuwa na sehemu ya pili ya kupakulia mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na sehemu ile zamani tukiitumia kwa kupakulia mafuta yasiyosafishwa kwenda katika *refinery*, kiwanda kile cha kusafirishia mafuta. Naamini kabisa kwamba hiyo ni sehemu muhimu sana ya kuendelezwa ili tuweze kuitumia tutakapoleta meli kubwa ya kupakulia mafuta.

Lakini ni dhahiri kwamba inawezekana tukaweza kutumia *refinery* iliyokuwepo kwa sababu kuna matenki makubwa yaliyo na uwezo wa kuchukua hata tani laki moja kwa wakati mmoja. Je, tumefanya maandalizi gani basi ili kuona kwamba tunayo-*facility* kama hiyo itakayowezesha kupokea mafuta yatakayokuja kwa wingi kwa wakati huu? Tufanye matengenezo ya *CPM*, tufanye ukarabati wa matenki ya *Tipper*, mwekezaji ndani ya *Tipper* amefanya nini? Je, atashirikishwa katika uwekezaji wa mafuta? Je, makampuni ya mafuta yaliyopo yatakuwa radhi huyo anayemiliki *storage* ya *Tipper* ambaye pia ni mmoja kati ya watu wanaoagiza makampuni ya mafuta kwamba yeye ndiye awe msimamizi wa hizo *facilities*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba tutazame uwezekano wa Serikali wa kununua tena *Tipper* ili pawe mahali huru patakapoweza kuhifadhi mafuta kwa ajili ya watumiaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni *EWURA*. Tuwe waangalifu sana tusije tukachanganya majukumu ya chombo tutakachokipa madaraka haya ya kuagiza mafuta haya, majukumu yake yasije yakagongana na majukumu ya *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwamba tuangalie upya sheria ya *EWURA* ili tuweze kuimarisha mamlaka hii tuweze kuipa nguvu zaidi iweze kusimamia kazi hii kwa umakini zaidi lakini kwa uhakika na kwa uhalali na kwa uhuru kabisa na bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuimarisha *EWURA*. Wanahitaji elimu, wanahitaji sheria nzuri zaidi, wanahitaji kuwa na watu wenye uzoefu katika sekta hii ya mafuta ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini wananchi wanatarajia kutoka *EWURA*? Niseme tu kwa kifupi kwamba imekuwa na bahati ni *Regulatory Board* ambayo inaungwa mkono na sehemu kubwa ya makampuni ya mafuta. Hili ni jambo la faraja sana kwa *EWURA* kuungwa mkono na makampuni mengi ya mafuta. *EWURA* ijitahidi sana iweze kufanikiwa katika kusimamia bei za mafuta ili wasimamiaji wa mafuta waweze kuridhika kwa viwango vya bei ambavyo vinapangwa na makampuni ya mafuta, tusiyaachie makampuni ya mafuta yakajilimbikizia faida kubwa zaidi badala yake wananchi wakaumia kwa bei kubwa. Tuangalie hilo, linawezekana na nimesema hivyo kwa sababu nina uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya *liberalization* ukitazama mfumo wa bei kulikuwa na eneo ambalo kulikuwa na *TPDC Margin* kwa sababu *TPDC* ilikuwepo,

kulikuwa na *Refinery Margin* kwa sababu *Refinery* ilikuwepo. *Refinery* haipo, *TPDC* haipo, *margin* zilizokuwepo ndani ya mfumo wa bei ziko wapi? Zote zimemezwa na makampuni ya mafuta! *EWURA* mtusaidie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho wananchi wanategemea ni *EWURA* kukomesha mtindo wa uchanganyaji wa mafuta, unatuletea madhara makubwa sana. Tunawategemea sana *EWURA* mtafanikiwa. Hii wanayoita chakachua ni lazima ikomeshwe inahatarisha maisha ya watu, inahatarisha vyombo na magari ya wananchi na ya Taifa hili na ni aibu sana katika Taifa kama hili, wageni wanakuja wanasikia nchi hii ina chakachua, yaani watu wanachafua mafuta na wanaingiza magari yao wanalipa bei kubwa na wanapakia mafuta machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa muda ulionipa na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Umetumia vizuri muda wako kwa kutupa semina tulio wengi sasa. Nitamwita Mheshimiwa Ruth Msafiri aendelee pale.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache katika Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu sasa.

Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri ambaye ni mara yake ya kwanza kuwasilisha Muswada mbele ya Bunge lako Tukufu lakini amewasilisha kwa ustadi mkubwa kabisa na tumeweza kumwelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kusema kwamba mafuta tunayozungumzia siku ya leo ni bidhaa muhimu sana ambayo tunaweza kusema kwamba ina changamoto kubwa sana katika suala zima la kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Kwa hali hiyo, ni suala ambalo ni nyeti kulileta kwa wakati huu na kwa lengo la kuweka sheria mpya ambayo itazingatia mazingira ya sasa. Ni suala ambalo ni muafaka na mimi nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri sana Serikali pamoja na ushiririkiano wanaokusudia kuufanya, chombo chetu *TPDC* ambacho kiliwahi kufanya kazi ya mafuta nchini na kikaifanya kazi hii vizuri kikiwa chini ya utaratibu wa Serikali, tunapoileta hii sheria sasa hivi, mojawapo ya dhamira yetu ni kuiomba sana Serikali kwamba pamoja na kuruhusu Serikali iwe huru. Kwa umuhimu niliousema kwamba mafuta ni kitu muhimu sana katika masuala mazima ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, ni lazima Serikali iwe na mahali ambapo inaweza na yenyewe ikajidai nako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali katika Muswada huu iweke mazingira mazuri ambayo itaweza kuiandaa upya *TPDC*, Muswada wetu huu uipe nguvu,

uisaidie ili iwezeshe kumudu kazi kubwa iliyopo mbele yetu na ambayo ipo mbele yake, ndiyo tunataka kuikabidhi kuhakikisha kuwa tunakuwa na mafuta nchini ambayo yataosheleza kwa matumizi ya watumiaji wengine wote pamoja na matumizi mengine yeyote ambayo tutakuwa tunayahitaji katika nchi yetu.

Kwa mujibu wa Muswada huu, *TPDC* inakusudiwa kupewa nguvu za kudhibiti vyombo vingine, sasa huwezi kutegemea kwamba unakipa chombo mamlaka ya kudhibiti vyombo vingine wakati chenyewe hakina nguvu kikashindwa na vyombo vingine. Kama ambavyo msemaji aliyeketi sasa hivi alikuwa anapendekeza kwamba itakaposhindaniwa, basi ionekane kuipa nafasi *TPDC*. Mimi nasema tujaribu kuipa nafasi *TPDC* kwa sababu tumeshaona madhara mengi katika mambo mbalimbali yaliyojitokeza. Kwa hiyo, sasa hivi tunapokwenda na sheria hii npendekeza kwamba tuisaidie sana *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kwamba Taifa kutokuwa na takwimu halisi ya mafuta ni kitendo cha hatari, tungeweza tukahujumiwa kwa namna yoyote ile bila kufahamu, lakini nadhani sasa tutakuwa na utaratibu mzuri utakaowezesha Taifa kufahamu matumizi ya wiki, mwezi, robo mwaka, miezi sita na kadhalika, kitu ambacho kitatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka kwamba hata mapato ya nchi kutokana na *product* nyingine za mafuta yalikuwa sio sahihi na sasa itaiwezesha *TRA* kukusanya vizuri mapato yake kwa upande huu ambao pale mwanzo haikuwa inajulikana. Kwa hiyo, mipangilio yetu mingine pia katika uchumi itakwenda vizuri zaidi na kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema kwamba itapewa mamlaka kwamba itasimamia bei, tunaomba kuangalia upande mzima wa hiki kitengo ambacho kimekuwa kikilifedhehesha Taifa letu cha kuchanganya mafuta. Hiki kitendo kwa kweli cha aibu na mimi napenda kila mmoja aliyekuwa anashiriki kufanya kitendo hiki na hata sasa hivi ninapozungumza kwa kweli popote katika Taifa letu ajisikie aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta haya yamekuwa yanachanganywa kwa namna mbalimbali hasa watumiaji wa *diesel* wamekuwa wakiathirika sana, akina mama wanaopika wanalipukiwa sana na mafuta kwa ajili ya kuchanganywa mafuta, tunaotumia taa za kandili pia taa zimekuwa zinalipuka ovyo ovyo na kusababisha madhara mbalimbali, watumiaji wa magari wengi hata Waheshimiwa Wabunge nimewasikia wanalalamika kwa sababu ya kutumia mafuta ambayo yamechanganywa ovyo ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kweli kupata bei nzuri na faida kubwa lakini ubora wa bidhaa anayoiuza ndiyo changamoto yake kubwa anayotakiwa kuisimamia kwa uaminifu. Tabia ya kupenda kuongeza bei ama kutokuongeza bei lakini kutafuta faida kubwa kwa kutumia udanganyifu ambao kwa wenzako unawaletea uharibifu, hili jambo hata Mwenyezi Mungu halipendi. Kama huwaogopi wenzio, basi mwogope Mungu ambaye humwoni, lakini yeye anakuona. Kwa kweli limekuwa ni jambo ambalo linatia aibu na limefedhehesha wengi. Mimi nashauri kwamba, pengine kungekuwa na chombo

maalumu ambacho kitaendelea kusikiliza malalamiko ya hawa watumiaji nje ya adhabu ambazo zimetolewa katika Muswada huu, kuwe na chombo kinachopokea malalamiko kutoka kwa watumiaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika wale wadau walioshiriki *BP* na waagizaji wengine wa mafuta, lakini watumiaji hawa wadogo wadogo wanaoathirika hawakuwakilishwa na mawazo yao hayakufikishwa. Wako wengi ambao hawaonekani, watu wenye vibatari pia ni wengi sana tunawaona maeneo mbalimbali, hata vijijini tunatumia sana vibatari pamoja na kandili, lakini kwa sababu ya bei ya mafuta kupatikana kwa taabu, watu wanaona kibatari kinabana sana mafuta na kwa kuwa anahitaji mwanga inabidi akitumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ninakiomba katika sheria hii baada ya kuwa Serikali imeshadhibiti suala zima la chakachua wakati tuko kwenye semina lilikuwa limetolewa pendekezo kwamba bei zilingane, kama *petrol*, *diesel* na pengine hata mafuta ya ndege, bei za mafuta zisilingane kwa sababu ya hofu ya hao wanaochakachua. Bei hizi zitakapolingana zitaumiza watumiaji wengine ambao kimsingi wasingeweza kuumia. Cha msingi sheria ibane namna ya kuingiza mafuta na namna ya kusambaza na namna ya kuwaadhibu wale ambao watakuwa wamekiuka taratibu. Lengo langu kubwa ni kutetea bei ya mafuta ya taa isije kuwa ndiyo sababu, kwamba Wabunge mlipitisha wenyewe na Rais amekwisha saina, basi tumeona sisi *EWURA* hatuwezi kupata bei nzuri ya mafuta au kudhibiti bei ya mafuta, kwa hiyo, bei iwe moja ili kusudi wale wanaochakachua wasiendelee kuchakachua hiyo itakuwa haikuwatendea watumiaji wote haki sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimependa niliseme hilo kusudi katika utekelezaji wa sheria hii izingatiwe kwamba tunapozungumzia hayo mafuta na mafuta ya taa yamo, tusije tukayaingiza katika mkondo wa kuyaongezea bei hali ambayo inaweza kuwaumiza watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kipengele kingine pia hapa ambacho kinadhamiria kueleza kwamba pale *Part III*, Ibara ya (7) inasema: “*Person shall not perform petroleum supply operations without having obtain a licence in accordance with the provisions of this Act*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na suala hili kwamba asiwepo mtu yeyote ambaye atakuwa anasambaza bidhaa za mafuta bila kuwa na leseni iliyo halali. Lakini napenda sana kuwe na watu ambao watasaidiwa kwa kifungu hiki hiki. Nasema hivi kwa uzoefu wa Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu, mimi ninalo eneo moja tu ambalo lina kituo cha mafuta ambayo ni ya pampu, maeneo mengine yaliyobaki hakuna vituo vyenye pampu. Kwa hiyo, badala yake wapo wauzaji wadogo wadogo ambao wanauza mafuta pamoja na *products* nyingine kwa kutumia maduka madogo madogo, ninamaanisha mapipa, magaloni, kitu ambacho mara nyingi sheria inakipiga marufuku.

Lakini kwa mazingira yalivyo, sio rahisi kwa mtu yeyote yule anayetaka lita mbili, tano au kumi kufuata mafuta kule ambako kuna kituo kikubwa cha mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachopenda kuomba hapa ni kwamba, hawa wauzaji wadogo wadogo wasaidiwe na sheria, wahalalishwe na waboreshe mazingira yao ili kuweza kuuza mafuta ndani ya vyombo ambavyo vitaweza kuwa vya usalama zaidi, lakini kuwasaidia zaidi kwa sababu mara nyingi wanapouza mafuta ndiyo yaliyo na michanga na vitakataka. Sasa hii ni kwa sababu hawajaangaliwa rasmi ili kuboresha mazingira yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri nao wasaidiwe kwa sababu sio kila eneo lina *pump system* iliyo nzuri inayoruhusiwa, au wewe ni *branches* za wale wenye pampu wakiwa kwenye *agency* zao au ni wawekezaji wadogo wadogo waliokuwa tayari kufanya hii biashara na wenyewe wapewe leseni na leseni zao zikubalike wasaidiwe kujengewa mazingira mazuri ili waweze kuuza mafuta. Kwa sababu isipofanyika hivyo, bei ya mafuta kwa mfano kwa Mkoa wa Kagera itapanda kupita kiasi kwa sababu ni lazima mtu anayetaka kununua mafuta kwenye Jimbo langu lazima waende Bukoba Mjini ama waende Kamachumu au Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili naona linaweza kuwaumiza watu wengi na hata kuna maeneo mengine kwa mfano ninapokuwa na safari za Visiwani kwangu hakuna vituo vya mafuta, lakini mafuta ya magaloni yapo. Wasaidiwe hawa ili wauze mafuta vizuri kwenye hali ya usalama kwa sababu yanaweza kulipuka na yanaweza kusababisha madhara mengine hata kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kulisema hilo kusudi iweze kuangaliwa kwa kuwa mara nyingi wanafuatwa sana na vyombo vya sheria wakiwabana na kuwazuia badala yake wawasaidie kwa sababu huduma wanayoitoa ni muhimu na inatakiwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nirudie kuipongeza Serikali kwamba imeleta Muswada huu katika wakati muafaka na naamini Muswada huu utasaidia pande zote, Serikali na Watanzania wengine wanaotumia na mitambo mbalimbali itakuwa sasa imepata mafuta mazuri yasiyokuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Lucy Owenya. Kwa orodha yangu ndiye aliyebaki.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa udhibiti wa biashara ya mafuta.

Awali ya yote napenda kuungana na wenzangu kuunga mkono Muswada huu kwa sababu umekuja wakati muafaka ambapo bei za mafuta zinapanda mara kwa mara. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wakati akitoa hoja yake amesema atajaribu kuiwezesha *TPDC*. Hili ni jambo la muhimu kabisa kuiwezesha *TPDC* kwa sababu tumegundua kwa sasa hivi kuna ongezeko kubwa la ugunduzi wa gesi asilia na katika ugunduzi huo wawekezaji watakuwa wanakuja wengi. Kwa hiyo, ni vizuri *TPDC* wakawezeshwa wakamilike zaidi katika hisa za uchimbaji wa gesi asilia. Hii inawezekana kabisa kwa sababu katika vyombo vya habari tumeona nchi kama Libya walianza kwa kuwekeza kwenye gesi asilia, walikuwa wanawekeza kwa *percent 73* lakini kwa sasa hivi nchi ile inashikilia *percent 93*, kwa hiyo kwa Tanzania inawezekana kabisa kwa sisi kuweza kufanya hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia katika vipengele vya Muswada, vilevile *TPDC* ikiwezesha kuwa na *percent* kubwa katika hii gesi asilia, haina maana kwamba magari yetu yote yanaweza kuwa yanatumia gesi badala ya petroli na hii itapunguza bei katika kutumia *petrol* nchini. Nasema hivi kwamba *TPDC* ipewe uwezo, wawe na *depot* ya kuweza kuhifadhi gesi na wao ndio washikilie hizo asilimia na waweze kuuza wazawa waweze kununua *shares* kutokana na hizo gesi na hii inawezekana kwa kuanzia na magari yetu *especially* magari ya Serikali ni mengi yatumie gesi asilia na haya ambayo yapo katika magari tuliyonayo kwa sasa hivi yaweze kubadilishwa yawe *duel system* ambayo inaweza kutumia *both petrol and gas*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada kifungu cha 32 kinazungumzia kuhusu *petroleum fee*. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini wanachaji *petroleum fee* katika nishati hii tu ambapo nishati nyingine kama makaa ya mawe, gesi na makaa ya kuni havitozwi kodi ya maendeleo ya nishati. Kwa kutoza kodi ya maendeleo ya nishati ya petroli kwenye petroli tu ina maana bidhaa ya petroli itazidi kupanda bei. Kwa hiyo, ningeshauri labda wote wangetozwa kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Muswada kifungu cha 45 kinazungumzia kuhusu adhabu. Tumeona hapa Tanzania makampuni mengi *especially* yanayohifadhi mafuta hasa wakati wa bajeti huwa wanahifadhi mafuta hayo kwenye *tanks* zao au kwenye *petrol station* zao kwa kisingizio kwamba bei ya dunia imepanda, lakini unakuta mafuta hayo wanayo hawayauzi, wanakuja kuuza kwa bei ya juu. Ningeshauri kwamba kosa hili liwe ni kosa la jinai na wapewe adhabu kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakubaliana na Muswada kwamba tuwe na *Strategic Oil Reserve*. Hili ni suala zuri kabisa kwa sababu tunaona hata juji juji hapa katika masuala ya kisiasa nchi jirani hapo Kenya kulikuwa na matatizo ya mafuta, lakini wenzetu pale *Dar es Salaam Independent Conference* tulivyokuwa tunapata ile semina, walisema Kenya nao wanayo *Strategic Oil Reserve*. Kwa hiyo, nafikiri hilo ni jambo zuri kwa sisi pia kuwa na hiyo *Strategic Oil Reserve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa Mheshimiwa Waziri atuelezee kwa sababu hapo zamani walikuwa wamesema kutakuwa na njia ya kutengeneza mafuta kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, sijui Serikali imefikia wapi katika mkakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ningependa kutoa tu angalizo kwamba Serikali isichukulie mafuta kama kigezo kikuu cha kodi, hivyo kuongeza kodi kwa mafuta mara kwa mara Serikali inapotaka kuongeza mapato yake katika nchi. Kwa hiyo, wachukulie kama hilo ni suala muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja na niishie hapo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Najua Mheshimiwa alijiandaa kuzungumza jioni lakini akakuta anaitwa saa hizi, lakini bado amezungumza vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani kuna michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge pale mwanzoni, wengine walikwenda kifungu hata kifungu. Kwa hiyo, naona itakuwa vizuri kama Waziri atakwenda ofisini kwake na wenziwe wakaangalie yale mapendekezo mliyotoa kusudi mchana tukirudi watoe majumuisho halafu tupitishie Muswada.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.40 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi sikuwa na wachangiaji wengine, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri anazo dakika 15, anayejibu hoja anayo saa moja. Mnaweza kugawana hiyo saa 1.15 mtakavyoona inafaa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria ya Mafuta. Naomba kwanza niseme kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ama kwa hakika nitakuwa sikutenda haki kama sikutambua mchango mkubwa wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili na kwa namna ya pekee wale wa Kamati ya Nishati na Madini katika kuboresha Muswada huu katika hatua zake zote uliopitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango hiyo imekuwa ni ya kujenga na kwa hakika ni ishara ya nia kubwa dhahiri ya ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge na kufanya kazi na Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba kwa dhati ya moyo wangu nikushukuruni kwa maelekezo hayo Wabunge wote, pamoja na pongezi zenu kwetu, mimi na Mheshimiwa Waziri. Ni matarajio yangu kwamba mtaendelea kutupa ushirikiano huu mimi na Mheshimiwa William Ngeleja,

Waziri wa Nishati na Madini ili Wizara yetu iendelee na iweze kutoa mchango mkubwa zaidi kwa maendeleo ya Taifa letu kwa ridhaa yenu Waheshimiwa Wabunge wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyoielezwa, Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ya Usambazaji wa Petroli na bishara zitokanazo na petroli. Ni Muswada ambao kusema kweli umechelewa sana hasa kwa kuzingatia mazingira yanayotawala uchumi wa Watanzania kwa hivi sasa na kwa maana hiyo, kwamba umeungwa mkono na Wabunge wote waliochangia ni jambo la faraja sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Waziri wangu hajajibu hoja, nami naomba nichangie kidogo kulingana na baadhi ya mchango ya Wajumbe. Mzee Athumani Janguo katika mchango wake amezungumzia suala la mabadiliko ya Sheria ambayo tumeyazingia. Lakini nilitaka kusema tu kwamba ni ushauri ambao umetusaidia katika kuboresha utekelezaji wa Sheria hizi hasa kwa kuzingatia kwamba tayari kuna Sheria ya *EWURA* ambayo ilikuwa imetangulia miaka miwili hali ya kwamba Sheria ya Mafuta ilikuwa imebaki nyuma. Kuna ushauri ambao tumeupokea wa *Bulk Procurement* kama alivyotushauri Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyozungumza tunaunga mkono. Nimeunga mkono kwa asilimia mia kwa mia ushauri huu. Kuna suala hapa la kubadilisha mazingira ambayo sasa hivi yanatawala utendaji kazi wa *TIPPER*. Nadhani kwa mazingira maalum ya *strategic petroleum reserves* ambazo zinakusudiwa na malengo ya kiuchumi yanayokusudiwa kufikiwa na uwezo huo unaotolewa na Sheria hii mpya, nadhani ni ushauri ambao uko sahihi.

Nilitaka kutoa mfano kidogo hapa, nilikuwa nafikiria suala la kufanya utafiti kidogo, kwamba hili jambo la kuwa na akiba ya dharura ya mafuta ni jambo ambalo liko kwenye nchi zote kubwa na kimsingi kama alivyoieleza ni jambo ambalo limeanza kwenye miaka ya 1970 kufuatia matatizo katika masoko ya dunia yaliyotokana na vita vya Ghuba mwaka 1972/73. Baada ya hapo, nchi nyingi zimekuwa na utaratibu huu wa kuweka mafuta ya akiba na kujiwekea muda maalum, wanakisia kwamba mafuta haya yanatakiwa yawepo kwa ajili ya matumizi ya kama wiki mbili ama wiki tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Bunge hili limelipokea hilo na limeliridhia kusema kweli ni jambo ambalo limetupa nguvu sana. Kama nilivyosema *strategic petroleum reserves* huko zinasimamiwa na Idara mbalimbali.

Mimi nadhani kwa misingi ambayo tumejiwekea sisi humu ndani kulikabidhi jukumu hili *EWURA* ni sawa sawa na kimsingi *EWURA* yenyewe itakuwa inasimamiwa na Wizara ya Nishati na Madini na hivyo Wizara ya Nishati na Madini itakuwa inaweka malengo kwa kulingana na hali halisi ya uchumi na mahitaji ya Taifa kwa wakati huo. *EWURA* kwa kweli itakuwa ni msimamizi kwa mamlaka ya kisheria ambayo imepewa na Sheria yenyewe ya *EWURA*, lakini sasa itasisitizwa na Sheria hii ya Mafuta ambayo tunaliomba Bunge lako liridhie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi amezungumzia suala la *single by moring* ambayo ni sehemu ya kupakulia mafuta huko baharini na kwamba tupate *SBM* mpya ya kisasa ambayo itakuwa na uwezo zaidi wa kupakua mafuta kwa kiasi kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku hizi chache zilizopita nadhani tumeshuhudia kwamba kulikuwa na matatizo katika kupakua mafuta ambayo yametokana na uwezo wetu wa kupakua mafuta. Kwa hiyo, nadhani huu ni ushauri ambao ni mzuri tu na tunaupokea na tumeshauriana kwamba tuupokee kwa sababu unaboresha zaidi malengo ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa nadhani na Mheshimiwa Mntangi amezungumzia suala la *TIPPER*. Nadhani nikubaliane naye moja kwa moja na niunge mkono ushauri huo kwa sababu kwa mazingira ya kuhitaji kuihifadhi mafuta nadhani ni vizuri tukaangalia upya utaratibu wa kuhifadhi *TIPPER* haswa tayari pana miundombinu, *infrastructure* zilizokuwepo pale na ambazo zinahitaji ukarabati kidogo na kuboreshwa zaidi ili kukabiliana na mahitaji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakati *TIPPER* inaundwa miaka hiyo, nadhani kama miaka 35 iliyopita au miaka 40, nadhani Mheshimiwa Mntangi atanishauri. Mahitaji ya mafuta miaka hiyo yalikuwa ni machache sana kuliko yalivyo sasa hivi. Kwa hiyo, kuna ulazima kabisa Serikali kuliangalia hili upya kwa kushirikiana na *TIPPER* yenyewe na *PPA* na *TPDC* na wahusika wote wanaohusikana na suala la *TIPPER* kwa ajili ya kuwa na maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma hapa katika utafiti huu nchi nyingine zinakuwa na *reserves* katika maeneo mengi. Ni kwamba Bunge lako peke yake naomba liridhie na Wabunge wengi wameunga mkono kuwa na maghala mawili, matatu nadhani itakuwa ni jambo la msingi. Lakini wa sasa hivi ushauri tuliupokea wa kuhifadhi *TIPPER* na kuikarabati nadhani ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ruth Msafiri amezungumzia suala la *TPDC* kuwezesha ili iingie kwenye biashara ya mafuta. Mwanzoni kulikuwa na mgogoro kidogo wakati wa kulielewa hili na nadhani mgogoro ulikuwa unatokana labda na watu ambao wamo kwenye biashara hiyo kwa kusema labda sasa *TPDC* inataka iingie kwenye ukiritimba na kadhalika. Lakini kusema kweli nadhani *concept* yake ya kuwa na *TPDC* kwenye biashara ya mafuta ni kama suala la kuwa na *TANESCO* kwenye biashara ya umeme na kadhalika. Jambo ambalo linaweza kuathiri uchumi wa Taifa kwa muda mchache na kwa kiasi kikubwa namna hii kusema kweli hatuwezi tukaliacha katika mikono ya watu binafsi katika makampuni binafsi *totally* bila Serikali kuwa na mkono hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma Sheria ya wenzetu Wajapan na Wamarekani, suala la kuwa na udhibiti wa namna fulani katika biashara ya mafuta kwa ngazi ya Taifa *actually* linachukuliwa kama ni suala la kiusalama pia kwamba huwezi kuliacha tu hivi hivi suala la mafuta ukawaachia. Wenzetu wanakuwa na *interest*

nyingine, wakati mwingine zinaweza zikaangalia masuala ya faida tu na kama Taifa ni lazima tujiweke kwenye mazingira ya kuwahami wananchi katika mazingira magumu na hivyo kusema kweli *TPDC* kuingia kwenye biashara ya mafuta ni ushauri ambao tumeupokea na tuufanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba kutakuwa katika biashara hii kuna wafanyabiashara wakubwa halafu kuna wafanyabiashara wadogo wadogo, na kuna watumiaji wadogo wadogo pia, na wakati mwingine kutakuwa na matatizo katika biashara na hivyo lazima tujiwekee mazingira ya kupokea malalamiko katika ngazi hii ya biashara. Kuna *Consumer Consolitative Consuler* ambayo iko chini ya *EWURA* ambayo kazi yake ni hii, lakini kwa kuwa *EWURA* imepewa majukumu maalum katika masuala ya mafuta. Nadhani kama yatajitokeza hayo yatapelekwa huko katika ngazi ya kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Ruth Msafiri, amezungumzia suala la bei ya mafuta ya taa isipande kwa sababu ya wachakachuaiji. Mimi naunga mkono hili, lakini pia nizungumzie kusema kweli ubaya kabisa wa hawa wachakachuaiji, kwa sababu wanachukulia ni biashara ambayo kusema kweli haimpi faida mtu mwingine yeyote isipokuwa wao wenyewe. Wengine wote inawasababishia hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalizungumza kwa uchungu kwa sababu na mimi ni mwathirika. Siku moja nikiwa Kilwa nilinunua mafuta lita 100 narudi mjini, gari ikaniharibikia maeneo ya Utete kuelekea Kibiti na palikuwa na simba wakati huo na ilikuwa jioni. Kwa hiyo, ilikuwa vigumu kushuka kuangalia matatizo ya gari hali ya kwamba wadudu waharibifu wananguruma nje. Lakini hiyo ilitokana na kuuziwa mafuta machafu. Nadhani ilikuwa lita kama 80, maeneo ya Somanga pale. Hatukufika hata kilomita 40 gari ikafa kabisa na mafuta ya lita 80 utengenezaji wake gari likagharimu milioni moja na halikupona tena. Sasa magari mangapi yanaharibika katika mazingira haya? Inawezekana wakati mwingine labda magari haya yabeba abiria, wagonjwa na kadhalika. Sasa watu kama hawa ambao wanatuuzia mafuta ya namna hii hawazingatii kabisa mahitaji yetu sisi na usalama wetu sisi watumiaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Ruth Msafiri, tunashukuru kwamba pia Waheshimiwa Wabunge mmeliangalia hasa kwenye sura ya adhabu ambazo wanabidi wapewe hawa wahusika wa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani pia haya yameanguka kwenye majukumu ya *EWURA* na sisi kwa pamoja tutayafanyia kazi.

Nilichotaka kusema Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba hili suala la uchakachuaiji, linashamiri kwa sababu kuna kodi ndogo kwenye mafuta ya ndege *Jet AI*. Kwa hiyo, wanaingiza mafuta kwa lengo la *Jet AI* halafu yanachanganywa na dizeli kwa sababu huku kuna kodi ndogo huku kuna kodi kubwa na wanatoka hapo wanapata faida, *super profit* kusema kweli. Kwa hiyo, hili jambo la masuala ya kodi kama mnavyofahamu haliko kwetu. Sisi kwetu liko suala la udhibiti wa *quality* viwango vya mafuta. Hili liko chini ya Wizara ya Fedha, Serikali ni moja. Kwa hiyo, nadhani

wenzetu wa Wizara ya Fedha wamelisikia na watalipokea kulifanyia kazi ili kuangalia namna ambavyo tunaweza tukafanya kazi kwa pamoja kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ruth Msafiri pia amezungumzia vizuri sana kuhusu wauzaji wadogo wadogo ambao wanauza mafuta kwenye mazingira ambayo yako mbali na ambapo wao tu ndiyo wanawezesha upatikanaji wa nishati hiyo. Nadhani tukubaliane tu kwamba hatuwezi kuanzisha Sheria, nadhani itakuwa vizuri zaidi kuwaweka kwenye *Regulations* za Waziri ili yeye aweze kuwatungia Kanuni za kuwawezesha kufanya kazi katika utaratibu ambao unaangalia masuala ya usalama, masuala ya ujumla ya mazingira ambayo wanafanyia kazi.

Mheshimiwa Lucy Owenya, amezungumzia suala la *TPDC* iwezeshe awali kabisa ili iweze kuingia katika uwekezaji wa gesi katika hatua hizi za awali. Naomba niseme hili ni wazo zuri sana haswa kwa sababu tukiingia sasa hivi kwenye hatua hii hapo baadaye tunapokuwa na uzalishaji mkubwa wa gesi sisi kama Taifa tunakuwa na ushiriki mkubwa zaidi katika matumizi ya gesi hiyo na faida zitokanazo na matumizi ya gesi hiyo.

Pia katika wazo lake kwamba tutakapofika hatua hiyo kama Taifa tukiwa *TPDC* imeshakuwa na hisa kubwa pia inaweza kuingia kwenye *Public Offerings* kwa kuwauzia wananchi hisa. Nadhani ni wazo ambalo limepokelewa na ushauri huo tutauzingatia, tutaufanyia kazi kwa sababu ni jambo la muda mrefu. Lakini kusema kweli ni ushauri ambao unazingatia sisi kama Watanzania kuwa na manufaa zaidi na rasilimali zetu na kuwa pia na mtazamo wa muda mrefu kuhusu mwenendo wa yote haya hasa kwa sababu pia ni lazima tuangalie huko mbele ya safari hatuwezi tutakaa tunaendekeza matumizi ya mkaa haswa kwenye miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha misitu inateketea, gesi tunayo na nadhani wataalam wanajaribu kufanya mizania lakini hasara inayopatikana kwa kutumia mkaa huenda ikawa hata ni kubwa zaidi kuliko uwekezaji ambao tunahitaji kama Taifa kuingiza ili miji hii mikubwa sasa iache kutumia mkaa na itumie nishati ya gesi hapo itakapopatikana ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika kufanya tathmini tu, inaonekana labda kitungi cha gesi kwa matumizi ukilinganisha na magunia ya mkaa, gesi ina nafuu zaidi na ina matumizi makubwa zaidi. Kwa hiyo, ni mambo ambayo Serikali tumeyapokea kama ni ushauri na tutafanyia kazi kuona namna ambavyo sasa tunawekeza tukawekeza hapa tunavyoendelea kupata gesi zaidi kwenye vianzo mbalimbali kama hivyo vya *Mnazi Bay*, Mkuranga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hoja ya uharibifu wa *flow metre* kama tulivyowasilishiwa kwa maandishi na Mheshimiwa Victor. Kusema kweli ushauri tumeupokea na Wizara itaufuatilia. Lakini kusema kweli ni jambo ambalo linatumiza sana na lipo katika utaratibu huo huo hatuwezi kukaa tunaangalia hali hii, hali ya kwamba nchi inapata hasara kubwa na wachache wanafaidika.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tunabidi tushirikiane Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu ili mashine hizi ziweze

kutengenezwa upya au hata ikibidi kununua upya kwa sababu hasara inayopatikana na kutokuwa na *flow meters* zinazofanya kazi kwa uhakika ni kubwa mno. Kwa hiyo, ushauri wa Mheshimiwa Mwambalalwa tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata ushauri wa Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, kuhusu umuhimu wa kutumia kiwanda cha *TIPPER*. Kama nilivyosema, tumekubali na *TIPPER* wakati hata wa kusimama shughuli ili kuwa na wataalam wazalendo na shughuli za kukarabati matenki zinaendelea ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa vya kuzuia majanga (*safety prevention equipments*). Tunakubaliana naye kwamba katika yote haya kwa wakati wote utunzaji wa mazingira ni suala ambalo lazima lipewe kipaumbele kwa sababu ya uharibifu mkubwa unaweza kutokana na matumizi yasiyofaa ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata hoja inayouliza kuhusu utafiti wa jumla wa masuala ya mafuta hasa kwenye Ziwa Rukwa ambao ulikuwa unafanywa miaka hii iliyopita. Kampuni ya *AMOCO* ya Marekani ilifanya utafiti katika miaka ya 80 huko nyuma. Hivi sasa Kampuni ya Sonango ya China inaangalia kutafuta mafuta katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema na Sheria hii inakusudia kuwezesha hilo, Wizara inashirikiana na *EWURA* na tutaendelea kufuatilia kwa makini masuala yote haya ya utafiti *exploration* ya mafuta. Lakini pia kuangalia kwa ujumla masuala ya ufanisi kuzingatia masuala ya ujumla ya usalama na uhifadhi wa mazingira. Kwa hiyo, juhudi inaendelea katika maeneo hayo na sisi tunaendelea kufuatilia, lakini tunaamini kabisa kifungu cha 44 cha Muswada huu wa Sheria kinakataza mtu yeyote kuuza mafuta ya petroli au bidhaa za petroli, lakini pia ni katika sehemu mojawapo ambayo inawezesha *EWURA* kufanya kazi zake kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nakusudia hapo kuzungumzia hoja ya Mheshimiwa Sigonda, alikuwa anazungumzia kuhusu biashara binafsi ya kuweka mafuta kwenye mapipa na majumbani ili kufanya biashara. Kwa hiyo, naomba kurudia tena hapa kwamba kifungu hicho 44 ni mahususi kwa ajili ya eneo hilo na kwamba Sheria imezingatia kwamba lazima pawe na *considerations* za usalama na za hifadhi za mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa ametoa pongezi kwa kuipa *TPDC* nafasi ya kushiriki kwenye biashara pamoja na Sekta binafsi. Kama nilivyosema, nadhani nimeshaelezea kwamba nafasi ya *TPDC* katika biashara hii ni ya kipekee. Kwa sababu ya masuala maalum ya kiusalama na ya kiuchumi na maslahi mazima ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzee Ngasongwa ameomba kwamba *bio-fuels* zitambulike kisheria, lakini pia liangaliwe suala la mazingira. Nadhani hii ni kweli juzi tulikuwa tunaangalia programu moja ya *CNN* mambo haya ya *bio-fuels* yanapokelewa sana huko *Far East*, Indonesia. Lakini wamegundua kwamba ni mambo ambayo lazima yafanywe kwa uangalifu kwa sababu kuna *environmental degradation* ambayo unafaidika nafasi moja, lakini hasara nyingine zinapatikana upande wa pili. Kwa hiyo, lazima tufanye *environmental impact assessments* na Sheria inaelekeza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mzee Hamza Mwenegoha, ameipongeza Serikali kwa kuwa na hifadhi ya mafuta. Lakini amesema pia kuwa *EWURA* wapewe madaraka ya kuchukua hatua za kisheria kwa watakaotumia leseni vibaya. Nadhani *EWURA* wanayo madaraka chini ya Sheria ya kuchukua madaraka kwa wanaotumia leseni vibaya na Sheria hii imesisitiza pia adhabu na Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mridhie hatua hizo ambazo zinaletwa kwenu leo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaribu katika Sheria hii na tunashukuru Waheshimiwa Wabunge wameliona na wamelielekeza kwamba Sheria hii pia imezingatia maelekezo au vipengele vinachokuliwa na Sheria nyingine, kama Sheria ya mazingira.

Kwa hiyo, tumejaribu kuonisha hizi mbili. Kwa mfano, Sheria ya Mazingira inasisitiza kuhusu utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kwa mwenye kuchafua mazingira kupewa adhabu kali. Sasa hili ni jambo ambalo linakuwa *balanced* na Sheria zote.

Kwa hiyo, Wabunge wameliona hili na wamelisisitiza, tunashukuru sana. Ni suala la umuhimu kuwa na nishati mbadala. Pia suala hili limezungumziwa na Mheshimiwa Anasitazia James Wambura na tumelipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea kama mwongozo katika kazi tunazokusudia kufanya pindi Sheria hii itakapokuwa imeridhiwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba tumepokea maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge kwa haya niliyoyaeleza na kwa namna ilivyo biashara hii inakwenda, ni biashara ambayo haikomi hapa baada ya kuwa na haya tuliyokuja nayo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo hapa ambayo tumeweka kwa ajili ya kudhibiti uhalifu na udanganyifu ndani ya biashara ya mafuta na huenda hivi sasa tunavyozungumza wajanja nao wanaanza kupanga mbinu za namna ya kupitia mlango wa nyuma kwa Sheria hii tunayoileta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba kwa kiasi kikubwa Sheria hii itakidhi matakwa na mahitaji ambayo yanaletwa. Lakini pia naomba nisisitize kwamba ni Sheria ambayo ni *revolving* kwa maana nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, itakuwa ni jukumu letu kukaa kila saa na kuangalia utekelezaji wa Sheria hii kwa maana ya *regulatory impact evaluation* na pindi tunapona kwamba labda pana tatizo, basi nadhani ni busara kuja kwenu kwa Wabunge na kushauriana nanyi na kuangalia kama tunaweza kuleta hoja za kuoboresha mara moja kwa sababu kutokufanya hivyo na kuiacha Sheria hii ikidumaa hali ya kwamba wenzetu wameizunguka, inaweza tusikidhi haja ambayo tunaleta Sheria hii kwa ukamilifu wake kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri wao tuliopokea na kwa maana hiyo, naomba kuunga hoja Muswada huu asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa ufafanuzi kwa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Muswada wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada, ningependa kuanza kwa kuwatambua wale ambao wamechangia kuboresha Muswada huu ulioko mbele yetu, kwa kuchangia kwa kuongea, kwa kuzungumza ama kwa kutumia maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawatambua waliochangia, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi aliyofanya kwa ajili ya kufafanua hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wetu leo kwa wale ambao walipata fursa ya kuongea, kuzungumza, wa kwanza kabisa alikuwa ni Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko - Mbunge wa Kasulu Mashariki ambaye alitoa Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati, aliyetoa Taarifa yake kutoka Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes - Mbunge wa Karagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Herbert James Mtangi, Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum na hatimaye alikuwa Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa naibu Spika, kwa wale waliopata fursa ya kuchangia kwa maandishi tulikuwa nao Mheshimiwa Anastazia James wambura, Mbunge wa Viti Maalum Mtwara,

Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Mwinchumu Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Hamza Abdalah Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Alhaji Dr. Juma Ngasongwa, Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogoiyo Sigonda, Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blande kwa mara ingine tena, Mbunge wa Karagwe na hatimaye tulikuwanaye Mheshimiwa Castor Raphael Ligalama, Mbunge wa Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi zimeshatolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado tuna hoja ambazo tunahitaji kuendelea kuzifafanua. Mimi nitaanza na hoja ambazo, ushauri, maoni yaliyotolewa na kamati ya Bunge kwa Nishati na Madini iliyowasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako, Mbunge. Zilikuwepo hoja nyingi lakini niseme tu kwanza waliunga mkono hoja ya Muswada huu lakini baadaye kukawa na maoni pamoja na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo walileta mbele yetu na kuishauri Wizara yetu, wametoa maoni kwamba wadau waelimishwe vizuri kuhusu sheria hii mpya na kwasababu kwa kufanya hivyo itakuwa imewasaidia sana wadau wanaojishughulisha na sekta hii ya mafuta ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri lakini pia waweze kuepokana na adhabu ambazo wanaweza kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu pamoja na taasisi zetu kama *TPDC*, *EWURA*, zitafanya jitihada za kuwaelimisha wadau wote kuhusu sheria hii mpya kwahivyo maoni na ushauri huo tunaupokea na tunaahidi kuendelea kuutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maoni mengine na ushauri kwamba wafanyabiashara waweke bima ya kumfidia atakayeathirika kutokana na biashara hii ya mafuta. Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wetu ni kwamba ushauri huu tutauzingatia wakati wa kutengeneza kanuni na kwenye masharti ya leseni. Ndiyo njia ambayo tunaona ni bora zaidi kutekeleza maoni na ushauri huu. Kulikuwa na hoja nyingine ya kuishauri Serikali, kwakweli ni kuelekeza kuhusu shirika letu la viwango *Tanzania Beural of Standards*. Lipewe uwezo ili liweze kutekeleza majukumu yake katika sheria hii. Sisi tuansema Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu ni mzuri na tunaupokea na kwakweli ndio dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kuliimarisha shirika hili la *TBS* kwa kushirikiana na mamlaka na taasisi nyingine za kiserikali kuhakikisha kwamba linakuwa na uwezo mkubwa zaidi ili liweze kusaidia sana manufaa ya watumiaji katika sekta hii ya mafuta kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu suala la *floor meter* zifanye kazi, lakini pia wakatushauri wafanyakazi ambao wanahusika katika vituo hivi walipwe vizuri zaidi. Na kwa kweli maadili ya uaminifu wao yazingatiwe sana.

Serikali iongeze umakini wa kufanya *vetting* pengine, kuwachuja ni wapi wanaostahili sana kuifanya kazi katika maeneo hayo kwasababu imani ni kwamba kumlipa mfanyakazi maslahi mazuri sana ni jambo moja lakini yeye kuridhika kwake

kwa hicho anachokipata na hatimaye kutimiza wajibu wake kwa maslahi ya umma ni jambo tofauti.

Sisi tuauchukua ushauri na maoni haya kwa dhati kabisa kwamba tutaendelea kushirikiana na mamlaka zingine ili kuhakikisha kwamba hali iliyopo sasa inaboreshwa kwaajili ya manufaa ya umma. Ushauri huu tunauzingatia na tutaangalia pia uwezekano wa kutumia njia nyingine ya *floor meters*. Kwa mfano, kuna hii teknolojia sasahivi ya *ultrasonic meters* ambayo wataalamu wanasema inaweza kuwa ni mojawapo ya njia za kusaidia sana kuboresha ufanisi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa *TRA na TPA* wafanye ukaguzi wa mara kwa mara ili kuboresha ukusanyaji wa kodi. Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba ushauri huu tumeupokea, tutakwenda kuufanyia kazikwa kushirikiana na taasisi na mamlaka zingine ambazo tunahusiana nazo katika utekelezaji wa majukumu haya katika sekta hii ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni *TIPER* iboreshwe na isimamiwe na *TPDC*. Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu utazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuangalia mikataba ya sasa ya kuendesha *TIPER* katika jukumu la uwekaji wa mafuta katika eneo hili, tuatakwenda kulifanyia kazi tuone jinsi gani tunaweza kujiandaa na kufanya ndivyo bora zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa *Kurasini Oil Jet* uimarishwe ilikuwa ni hoja nyingine. Ushauri huu tumeupokea utazingatiwa na kwakweli tumeendelea, hata kabla ya kuwasilisha Muswada huu, tumekuwa tukiendelea na juhudi kwa kushirikiana na wenzetu wa bandari pamoja na mamlaka ya mapato kuona jinsi gani tunaweza kuimarisha maeneo haya ili hatimaye matatizo tunayopata sasa yasiendeleo kujitokeza kwa kiwango kinachoonekana sasa. Wizara na *TRA* wajipange vizuri ili kudhibiti ukwepaji wa kodi, hili tumeendelea kulifafanua Mheshimiwa Naibu Spika, tumelipokea tutaendelea kulifanyia kazi. Lakini niseme tu kwamba kwenye suala la *KOJ* pia tutapenda kuishirikisha Wizara ya Mambo ya Ndani kwasababu tunaamini kwamba itatusaidia sana na hasa kupitia ile Kamati ya usalama iliyo chini ya Wizara hiyo. Kwahiyo tutaendelea kushirikiana na wenzetu hawa ili tujiimarishwe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni ile *energy account* tuliyoitaja katika mojawapo ya ibara za muswada wetu itumike na *TPDC* ili kuendeleza shughuli za mafuta. Mheshimiwa Naibu Spika, malengo au madhumuni ya kuweka ibara hii katika muswada huu na hatimaye itakapokuwa sheria, nia yetu ni kuhakikisha kwamba *account* hii inatumika kuendeleza sekta ya nishati kwa ujumla, kwa maana ya kuliimarisha shirika letu la mafuta ya petroli *TPDC*. Lakini pia kuna taasisi nyingine kama wakala wa nishati vijijini, tunaamini kwamba kwa kutumia mfuko huu sekta hii itakuwa inaimarika zaidi na hatimaye ushiriki kwa mfano wa *TPDC* katika masuala ya utafiti wa mafuta na gesi utaendelea kuimarika zaidi kama amabvyo Waheshimiwa wachangiaji walivyokuwa wanachangia na wakaonesha dhamira hiyo. Kwasababu kama tukifanya vile *TPDC* itapata uwezo zaidi na hatimaye Taifa litakuja lifaidike zaidi mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni *information system* iimarishwe. Sisi tunasema ushauri huu tunaupokea na utatekelezwa kama moja ya majukumu ya *EWURA* na sisi Wizara tutaendelea kuratibu utekelezaji wa maagizo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *emergency supply plan* ihusishe wadau wote, ilikuwa ni ushauri mwingine. Ushauri huu ni mzuri tunauchukua na kwa kweli tunaahidi kwenda kuufanyia kazi. Pamoja na hiyo Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maoni mengine ambayo yalitolewa na sisi tungependa kukiri kwamba tumeyatambua na tunaheshimu na tunaendelea kuyafanyia kazi. Mojawapo ilikuwa ni masharti yote yatakayotungwa na Waziri kwenye kanuni kwa lengo la kuweka taratibu bora za kusimamia uingizaji wa mafuta chini ya utaratibu wa uagizaji wenye ufanisi, yaani *efficient procurement*, kanuni hizo zieleze wazi namna njia hiyo itakavyotumika na kanuni ziainishe wazi adhabu zitakazotolewa kwa watakaokiuka sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalikuwa ni maoni na ushauri kutoka kwenye Kamati ya Nishati na Madini. Tunalithibitishia Bunge lako kwamba tutakwenda kuyafanyia kazi na ni maoni yetu kwamba kanuni nzuri zaidi zenye ufafanuzi wa kutosha tutaziweka katika maelekezo ya ziada katika, ni namna gani jambo hili lifanyike tutaliweka kwenye kanuni kama ambavyo tumedhamiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa miundo mbinu ya barabara pamoja na usimamizi thabiti wa *EWURA* na Tume ya Ushindani iboreshwe ili kusiwe na kisingizio cha kupandisha bei ya mafuta kutokana na umbali wa watumiaji hasa walioko mbali na bandari za Tanga na Dar-es-Salaam. Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoona jambo hili linahusu wadau wengine wakiwamo wa Wizara ya Miundombinu na tunahitaji kuliangalia kwa mapana zaidi. Lakini ushauri huu ni mzuri tunaupokea kutoka kwenye Kamatai na tunaendelea kuwasiliana na wenzetu tuone jinsi gani tunaweza kufanikisha, lakini niseme tu kwamba kwa kweli juhudi zinaendelea za Serikali kuendelea kuboresha miundombinu iliyopo sasa lakini tunaamini kwamba kadiri siku zinavyokwenda na sisi pia tutakuwa tunazidi kujipanga vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji wa kambi ya upinzani alikuwa na hoja kadhaa ambazo tungependa kuzitambua, pamoja na mambo mengine lakini pia zipo chache ambazo tungependa kuzitambua na kuzitolea ufafanuzi. Kwanza tunaishukuru kambi ya upinzani kwa ujumla, michango yao yote iliyoonesha kuunga mkono hoja hii na chini ya taarifa iliyosomwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, tunakushukuru sana kwa niaba ya kambi nzima ya upinzani kwa kuunga mkono Muswada huu. Kulikuwa na hoja ya kutaka kujua ibara ya tano moja, yatolewe maelezo jinsi *EWURA* itakavyofanya *economic regulations*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba ukisoma kwenye huu Muswada kwenye ile ibara ya tatu kwenye kile kifungu cha *interpretation*, tafsiri pale. *Economic regulation* imetolewa ufafanuzi lakini niseme tu kwamba mazingira ambayo *intervention* inafanyika au *economic regulation* ni nini? Itafanyika wakati ambapo kuna *market failure*. Ndio dhana halisi ya kwanini kunakuwa na *intervention* ya mamlaka ambayo imekabidhiwa hii *regulatory authority*.

Jambo hili ni la kawaida kwasababu Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi katika mazingira kama haya soko letu hivi lilivyo la mafuta pamoja na kwamba tunasema liko ni soko huria lakini haliko huria asilimia 100 na ndio maana katika masoko kama lakwetu ambayo hayajafikia kiwango cha, halijakomaa kiasi cha kusema sasa nguvu ya soko iendeshe mambo yote, kunakuwa na hizi *regulatory functions* ili *regulatory authorities* kuhakikisha kwamba zinadhibiti mahali inapotokea. Na hili tunaliongelea tukiunganisha pia na hoja iliyokuwa imetolewa na Mheshimiwa Said Amour Arfi kwa niaba ya kambi ya upinzani kuhusu ibara ya 31.

Na wapo Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema nakumbuka na Mheshimiwa rafiki yangu Mheshimiwa Blandes kulikuwa na mapendekezo katika hoja yake ya maandishi kwamba tuangalie namna ya kuiboresha lakini niseme tu kwamba kifungu kilivyosimama hiki matumizi yake ni mahala amabpo kutakuwa na matatizo kwa mfano ikitokea kwamba wahusika katika soko hili kwa mfano waagizaji wa mafuta wanaamua kufanya *cut-tail* au *syndicate* wanakubaliana kupanga bei. Katika mazingira hayo ndio ambapo Serikali itaingiza mkono wake kuchungulia zaidi kutaka kujua hasa kuna nini hapo? Na kwanini mazingira haya yawe hivyo kama ambavyo inaweza kuwa imejitokeza. Kwahivi ndiyo dhana halisi ya kuleta hizi *intervention*.

Lakini kwa kweli lengo la ujumla ni kuhakikisha kwamba soko linakuwa huru na lianendeshwa na nguvu za soko. Lakini kama ilivyo kwenye sekta nyingine kama ya mawasiliano ambayo tunafahamu miaka ya 2000 mwanzoni kulikuwa na mgogoro mkubwa katika makampuni ya simu, lakini mdhibiti *regulator* kwa maana hiyo aliingilia kati kupanga zile bei za jumla za *inter-connection* kati ya kampuni moja na nyingine.

Lakini pia hata kuhakikisha kwamba zile bei ambazo anatozwa mlaji zinakuwa hazina madhara sana kwa kuangalia vigezo mbalimbali.

Ndio mazingira ambayo tunaongelea kwamba kuna wakati ambapo unaona kwamba mambo hayaendi sawa, hayaendei kama tulivyotarajia pamoja na kuliachia soko likiwa huru basi ndio hapo mkono wa Serikali unaingilia lakini niseme kweli utaratibu huu unatumika karibu nchi zote duniani. Kwasababu si rahisi sana kuwaachia wahusika nguvu ya soko ikatawala na hasa ikatoa kile ambacho kinatarajiwa kwa manufaa ya walaji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Msemaji wa kambi ya upinzani alitaka pia ufafanuzi kwenye kifungu cha sita kuhusu adhabu, anayekiuka kifungu namba tano, 42 na 43 ziwe ni faini na kifungo kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu hizi zote kuna adhabu ya kutumia adhabu hizi zote kwa pamoja. Hata hivyo Mahakama inapewa nafasi ya kutoa adhabu kutokana na mazingira ya utendaji wa kosa na hii sababu yake ni rahisi tu kwamba katika ile dhana ya mgawanyo wa madaraka kwa ile mihimili mitatu ya dola swala linapofikia hatua ya sasa nani mtu atoe hukumu, inakuwa ni chombo kile cha Mahakama. Ndio maana tunasema pengine isingekuwa vizuri sana sisi hapa tukaweka, utekelezaji wake

utakuwa mgumu kutokana na hiyo dhana ya mgawanyo wa madaraka kwa hii mihimili mitatu ya dola.

Kwahiyo nasema Mahakama itaamua, lakini sisi walau kifungu kilivyo kinasimama kikielekeza hivyo kama Mahakama kwa busara zake itaona kwamba hii inafaa basi utekelezaji wake uwe kwaa kiwango hicho. Mheshimiwa Msemaji, wa kambi ya upinzani alikuwa na hoja nyingine kuhusu kifungu namba 11, alikuwa anasema badala ya kuhamisha leseni inapendekezwa leseni ifutwe kama muhusika ameshindwa kutekeleza masharti.

Kutokana na mazingira ya utoaji wa leseni ambazo zinatolewa kwa kipindi kirefu sana kuna umuhimu wa kuruhusu uhamishaji wa leseni. Hata hivyo hakuna leseni itakayohamishwa mpaka izingatie masharti yatakayowekwa na *EWURA* ambaye ndiyo mdhibiti katika hii sekta ya mafuta na maji. *EWURA* inaandaa utaratibu utaratibu unaosimamia uhamishaji wa leseni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli niseme jambo hili ni la kawaida sana kibiashara kwasababu kunakuwa na mambo mengi, mtu anapokuwa anaanzisha biashara unakuwa na mipango yako, lakini wakati mwingine kabla hujafikia malengo yako kuna matatizo mbalimbali yanaweza kukukumba.

Mfano wake ni rahisi hata katika mipango ya hatua ya mtu binafsi, unaweza kuwa na mambo yako ukapanga ujiwekee utimize haya baada ya muda Fulani lakini kwasababu mbalimbali unaweza kukwazwa kutekeleza hayo au kutimiza azma yako uliyopanga, kwahivi ndio maana kunakuwa na hiyo fursa. Lakini cha msingi ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti vizuri kupitia huyu mdhibiti wetu ambaye ni *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani ilikuwa na hoja nyingine kuhusu ibara ya 24 moja na 33 moja, kwa maoni yao walikuwa wanaona kwamba vinakinzana. Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme tu kwamba nia ya vifungu hivi ni kulinda soko huru. Mfumo wa soko huru huleta ufanisi kwamaana ya *efficiency* na kwenye ibara ya 24 ukiangalia vimetajwa vitendo vinavyozuwia nguvu za soko zisifanye kazi ambavyo sheria ya ushindani inavikataza.

Tunachotaka kusema Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni kwamba vifungu hivi kwa ujumla vinatambua nguvu ya soko. Na ni kulinda hiyo dhana itekelezeke, lakini katika mazingira Fulani kama nilivyokwisha kuelezea kwa msingi hasa wa ile *economic regulation na intervention* za wadhibiti zinavyokuwa basi wakati mungine inakuwa tu muhimu kwamba kuingilia.

Kifungu namba, ibara ya 37, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alitaka kujua *specification* ziwe ni zile za kimataifa na sisi tunasema Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo dhamira, ushauri huu utazingatiwa na kwa kawaida viwango vya nchi yoyote huwa vinaainishwa na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja zingine nyingi za kawaida ambazo zimetolewa na kambi ya Upinzani lakini kama nilivyosema wakati natoa ufafanuzi kwenye baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini yako mambo mengi ya maelekezo, ushauri ambayo kwa ujumla wake tunayachukua na kwenda kufanyia kazi.

Kwa waheshimiwa ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa kuzungumza, Mheshimiwa Gosbert Blandes, alikuwa na mapendekezo kadhaa na alipitia kwa kweli aliamua kujikita kwenye vifungu. Ushauri wake wa kwanza ulikuwa ni kuhusu kifungu cha tano ibara ya tano na kapendekeza badala ya kutumia neon *may* tutie mkazo zaidi kwa kutumia neon *shall*.

Niseme tu kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutazingatia na tutatekeleza kwa ushauri wake. Lakini pia alikuwa na hoja kuhusu ibara ya 10, ibara ndogo ya pili leseni ziwe ni kati ya miaka mitatu mpaka 20. ushauri huu tunauchukua tutakwenda kuufanyia kazi tuone jinsi gani ni bora tunaweza kuufanyia kazi kuboresha hali iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tisa, ibara ya tisa ibara ndogo ya nne, Mheshimiwa Mbunge Blandes, alitaka alitushauri muda wa kuomba na kupata leseni kwakweli isiwe siku 40 kama ambavyo tulikuwa tunadhamiria na akashauri iwe siku 90. lakini pia akaongezea akasema, hizo siki 90 hizozisianze sasa hatakama sheria hii itapitishwa kwamaana ya taratibu za kawaida Mheshimiwa Rais, atakapokuiwa amei *accent* na kusaini, tuwape mwaka mmoja wa kujiandaa. Tunakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kwamba pengine na kwasababu kuna waheshimiwa wengine wamechangia kwa kweli katika hili kwa kuandika ama kuzungumza kwamba pengine siku 40 ambazo sisi tulikuwa tumedhamiria na kwasababu tulikuwa tumefanya *consultation* na wenzetu wa *EWURA* kwasababu mchakato mzima uliwahusisha wakajiridhisha.

Lakini Mheshimiwa Spika, tunakubali ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwamba ni vyema basi tukawanao *flexible* katika hili tukubali hizo siku 90 lakini ile hatua ya pili baada ya hapo tuwe na *grace period* ya kujiandaa kwasababu pengine kuna mambo mengi ambayo yako *pending* sasahivi.

Ukisoma muswada ambao umesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, ukausoma na lile jedwali la marekebisho kwenye muswada mulionao mutaona kwenye ibara ya 54, imezingatia ule ushauri wa kwamba kuwe na *grace period* ya mwaka mmoja. Itazingatiwa, lakini sasa baada ya marekebisho inakuwa ni ibara ya 56. kwahivi tunaendelea na hili tunakushukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kuliona na waheshimiwa wengine ambao walichangia katika hilo lakini tunazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Blandes, aliendelea kwa kutushauri sheria itekelezwe baada ya kukamilisha maombi yaliyoko sasahivi. Kama nilivyosema

lote nalo hilo limezingatiwa kwasababu ile *grace period* ya mwaka mmoja ipo kwenywe ile ibara ya 56 kwa sasa lakini ukisoma ile ule muswada wa kwanza ni ibara ya 54.

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge, alielezea alitupa ushauri mzito kwa mambo mengi lakini niseme tu kwamba baadhi ya hoja alizozitoa Mheshimiwa Janguo, Mheshimiwa Naibu Waziri, alizitolea ufafanuzi lakini na mimi niseme machache katika hilo. Mheshimiwa Janguo, alitushauri kifungu cha ibara ya nne, majukumu ya Waziri ya kusimamia kwa hicho kifungu nne E, kinaonesha utendaji na sio usimamizi. Ibara ya nne E kinaonesha Waziri ana jukumu la kiutendaji badala ya usimamizi. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Janguo kwa kukiona na sisi tumekaa, na akapendekeza na hata namna ya kui *draft, wording* yake tuibadilishwe kidogo. Angependekeza tuanze neon *course to be prepared*, ukisoma ile *wording* ya ile ibara. Nashukuru na tunampongeza Mheshimiwa Janguo, kwa kuliona hilo na sisi tunasema Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu tunauchukua na tutaufanyia kazi. Na tunakubali kurekebisha *wording* kama ilivyo, tutaanza na *course to be prepared* halafu tutaendelea kuiboresha hiyo ibara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Janguo, aliongelea kifungu cha 14 ibara ya 14 tatu hii ya siku 40 kama nilivyosema wakati naelezea hoja aliyotoa Mheshimiwa Blandes, sisi tumeshakubali tumeshazingatiwa. Alikuwa na hoja ingine katika ibara ya 26 moja, maneno *gradual adoption and the adoption* ina matatizo neon *gradual* liondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya neon hilo ni kuwezesha viwango vizoeleke na wadau na kutoa muda wa *TBS* kufanya tathmini za viwango vya kimataifa ili vilingane na mazingira ya hapa nchini. Kwasababu ni jambo ambalo tunakuwa kama tunalianzisha kwa mara ya kwanza pengine ni vyema tukawapa nafasi, fursa ya kujifunza na pia tujipe fursa ya kuona kubaini mapungufu au udhaifu utakaojitokeza katika utekelezaji wa azma hii. Kwahivi tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Janguo, ukubaliane na sisi kwamba kwa sasa pengine ni busara tuliache lakini kadiri tutakavyokuwa tunakwenda tutaona jinsi ambavyo *behavior* ya utekelezaji wa jambo hili utakuwa inatuonesha ni kipi cha kufanya sasa, lakini tunakushukuru kwa ushauri wako. Pia ulikuwa na maoni kuhusu ibara ya 28 tatu, *recovery of relevant costs* sheria zake zitajwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *relevant laws* kama zilivyotumika hapa ina zina maana pana zaidi ya *recovery of products from the owner*. Sheria hizi ni nyingi na hazitaji *recovery* tu lakini zinaendelea hata kuweka masharti ya ziada kwa muhusika.

Hivyo ni bora kuwa na sentensi ya aina hii tuakdhani kwamba kuliko kujibana, kwahivyo tukaiacha hivyo kwasababu ina wigo mpana zaidi. Ibara ya 43 ibara ndogo ya pili Mheshimiwa Janguo, alipendekeza neon *may* libadilishwe liwe *shall*, neon *every* liwe *any* au ifutwe kabisa. Tunashukuru na tunampongeza Mheshimiwa Janguo kwa kutushauri na niseme tu kwamba ushauri huu tumeuzingatia na ushauri huo utatekelezwa na itasomeka kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapa nyingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amezielezea lakini nipende kusema baadhi ya hoja ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri, hakuzitolea ufafanuzi kwa jinsi ambavyo tulikuwa tumekubaliana na hasa kwa

Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi. Mheshimiwa Gosbert Blandes, alikazia mchango wake wa maneno kwa kuandika.

Lakini kama nilivyofafanua kuhusu tafsiri sahihi ya ile ibara ya tano na 31 jinsi zinavyo *link* tunaamini kwamba ilivyo kwasasa imekaa vizuri Mheshimiwa Blandes, na kwasababu moja inaelezea habari ya bei lakini bei kimsingi azma kubwa ikiwa ni kuendeshwa na nguvu ya soko hasa hiki kifungu cha 31.

Lakini kule namba tano tukawa tunaongelea mamlaka ya *EWURA* lakini pia kwa kuzingatia hiyo nguvu ya soko. Lakini katika mazingira Fulani tukasema kwamba *intervention* inaweza kufanyika, kwahivi Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa nadhani kwamba hili tukubaliane kwasasa tuliache lakini tunakushukuru kwa kuliona hilo. Mheshimiwa Mwenegoha, alitoa hoja nyingi za kutushauri pamoja na kutupongeza lakini namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amelitolea ufafanuzi na niseme tu kwamba kwa ujumla wake yapo mengi ya kuzingatia lakini kuhusu suala la mazingira, kwasababu sheria ya mazingira ipo inaelekeza na adhabu zake kwa mtu ambaye anakuwa anakiuka maeklekezo ya vifungu vya sheria ya mazingira tunaamini kwamba kila inapojitokeza basi sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii, muswada huu utakapokuwa sheria utasomwa pia na sheria zingine ambazo zinatumiwa kwa sasa kwahivyo tunaamini kwamba utekelezaji wake hautakinzana na madhumuni yaliyokusudiwa katika muswada huu.

Mheshimiwa Athumani Janguo, alikazia pia mchango wake wa mdomo kwa maandishi na kwakweli ametushauri mambo mengi tunashukuru sana. Na niseme tu machache kati ya yale uliyoyashauri Mheshimiwa Janguo ni hili la kusema sheria hii itakapokuwa imepita itamke wazi kuwa *TPDC* inaruhusiwa kuingia kwenye biashara na mpango wa dharura. Na ukaongelea ibara ya nne C, na hili ni shauri zingatia la kupendekeza itakavyosomwa. Lakini tunakushukuru sana kwa michango ambayo umetusaidia Mheshimiwa Janguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nirudie tena kusema kwamba tunawashukuru sanasana Waheshimiwa wabunge kwa pamoja kuanzia ngazi ya Kamati lakini hatimaye kwa michango ambayo mmetutolea hapa na niseme tena kwa niaba ya Wizara yetu tunafarijika sana jinsi ambavyo umetuongoza na tunawaahidi kuendelea kufanya mambo yyetu kwa umakini zaidi tukitegemea ushauri wenu kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Sasa kabla ya hatua nyingine, Mheshimiwa Waziri, alikuwa naeleza kukubaliana na hoja walizotoa Waheshimiwa Wabunge, katika vifungu Fulani.

Sasa tutakapofika kifungu hicho itabidi musimame na kueleza hayo munayotaka kubadilisha. Kwa sababu mungekuwa mumesambaza *supplementary amendment order* tungekuwa tumeitumia hiyo. Kwahiyo pale ambapo hapana *supplementary paper* tutakapofika kifungu hicho mutaeleza maneno yanayotakiwa kuwepo. Katibu.

KATIBU: Kamati ya Bunge zima.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Tukae.

KATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetumia *Bill Supplement* namba 12 ya tarehe 12 Oktoba, ukurasa wa tano kifungu cha kwanza.

NAIBU SPIKA: Kifungu cha kwanza, kinaafikiwa? Enhee, Mheshimiwa Shelukindo?

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Usambazaji wa Petroli wa Mwaka 2007 (The Petroleum Supply Bill, 2007)

Ibara ya 1

MHE. WILLIAM SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba katika ile *shadow* ya marekebisho kile Ibara cha kwanza kina mabadiliko pale ya kuwa *Petroleum Act* ina mabadiliko pale ya kuwa *Petroleum Act* badala ya *Petroleum Supply Act*. Nadhani jana tulizungumza labda wenzetu walifanya marekebisho hawakuyafanya hapo, *Petroleum Act* badala ya *Petroleum Supply Act* Ibara cha kwanza kile kama ilivyo kwenye *shadow of ammendment*.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunakubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge tutarekebisha kasoro hiyo.

MWENYEKITI: Au iseme umerekebishaje?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Kwa kuondoa hilo neno *supply* inakuwa *the petroleum act*.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tunaondoa *supply* in a *act*.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 2

Ibara ya 3

Ibara ya 4

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara cha 5

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 6

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 9

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Pamoja na Mabadiliko yake)

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

Ibara ya 14

Ibara ya 15

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Pamoja Mabadiliko yake)

Ibara ya 20

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima Pamoja Mabadiliko yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima pamoja mabadiliko yake)*

Ibara ya 30

Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima pamoja mabadiliko yake)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima pamoja mabadiliko yake)*

Ibara ya 37

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 43

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishakubaliana kama nilivyokuwa nafafanua kwamba tumezingatia hasa wa Mheshimiwa Janguo kwa hivi tutarekebisha kama alivyokuwa amependekeza.

MWENYEKITI: Alipendekeza nini.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Badala ya kutumia *may* tunaweka *shall*.

MWENYEKITI: Hiyo katika Ibara gani cha 41, 103 moja

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, 43 mbili.

MWENYEKITI: 43 mbili kuna mambo mawili kuna *every unused capacity* mnaandika nini? neno *every* lilikuwa linaondokana 42(2) Mheshimiwa Mbunge alipendekeza.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge alitaka tuondoe neno *every*.

MWENYEKITI: Muweke nini, *any unused or what*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Iwe *any unused*.

MWENYEKITI: Kwa hiyo tunaondoa *every* tunaweka *any*, halafu na lingine.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yalikuwa kwamba *any unused capacity shall* badala ya kutumia neno *may*.

MHE. ATHUMAN S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo niliyotoa pendekezo la sahihisho nilisema kutumia *every* halafu kisha kusema *may*, ah *shall* inakuwa haiwezekani kwa hiyo nimeshauri ama waondoe neno *every* na kisiwepo kitu chochote kingine waanzie tu *unused capacity shall* au waweke any badala ya *every* kwa hiyo wanahiari ya kuamua kuweka any badala ya *every* au kufuta yote haya na kuanzia *unused* hapa.

MWENYEKITI: Ukiweka *any* ondoa *every shall* inabakia.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ajaribu kui-*phares* kuione kama tulimwelea vizuri wakati anachangia, samahani Mheshimiwa Janguo kama anaweza kui-*phares*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janguo hebu eleza ulivyosema.

MHE. ATHUMAN S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika nimeacha ile sheria nadhani unaposema *every may* haieleweki sasa.

MWENYEKITI: Tunakubaliana wote kwamba neno *every* linaondoka tunaweka any, sasa ukiweka any itasomeka hivi.

MHE. ATHUMAN S. JANGUO: Ukiweka *any* unaondoa lile neno *shall* unasema *any unused capacity may be opened to other licences in the manner splinted under this act* au sivyo ondoa kabisa yote acha *unused* halafu uendelee kusema kwamba *shall*.

MWENYEKITI: Ninyi Wizara mnapendekeza lipi sasa.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Kama unavyoona mwanzoni sisi tulielewa tofauti, lakini kwa sababu Mheshimiwa Janguo amesema pengine angependekeza *in any case* kama tunge-*construct* kwa kuondoa *every* pengine tutangulie na *any unused capacity shall be opened to* nadhani tungependa isomeke hivyo tunaweka *an then* tunaondoa *every* kwa ku-*substitute every* shall inabaki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge sasa tunafanya hivi tunaondoa *every* basi tukiondoa *every* tukaona *any* inatosha.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 44

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

*(Ibara kipya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

MWENYEKITI: Kumbukeni hapa tume-*renumber* tulipoongeza 45 mpya basi namba zingine zote zinabadilika.

Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 54

*(Ibara mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

MWENYEKITI: Kwa hiyo tuna *renumber* tena.

Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
zima Bila Mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Usambazaji wa Petroli wa Mwaka 2007

[The Petroleum Supply Bill, 2007).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima limeupitia Muswada wa Sheria ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa sheria ya biashara ya Mafuta yaani *The Petroleum Act* ya mwaka 2007 kama ulivyorekebisha au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Usambazaji wa Petroli Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nipeleka hatua haraka sivyo ilivyopaswa kuwa. Sasa tumekamilisha Muswada huu wa Petroleum Bill kesho tutaendelea na Miswada mingine miwili, nafikiri Mheshimiwa Waziri ni Muswada wa *Financial* mtaona kwenye *order paper*.

Lakini kesho ndiyo siku ya Alhamisi siku ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa na kipindi cha kujibu maswali ya papo kwa papo ya Wabunge na elewa kwamba mmeshagawiwa mwongozo kuhusu maswali kwa Waziri Mkuu nafikiri mmepata kwa sababu ni siku ya kwanza ni vizuri mkasome vizuri hiyo miongozo kwa sababu haitakuwa vizuri mara uambiwe sio sawasawa hujafanya nini na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, tumesema Waziri ataulizwa maswali ya kisera na wakati huo huo haitakuzuia Mbunge kuuliza swali lako kwa Waziri anayehusika lakini Waziri Mkuu ataulizwa maswali ya kisera yaliyo mafupi atakayeuliza swali atapewa nafasi moja ya kupata swali la ufafanuzi kama lazima maana yake inakuwa kama tradition lazima mtu aseme swali na lingine na lingine sio lazima unaweza kuuliza hivyo.

Kwa hiyo, utaratibu ni kwamba kesho asubuhi kabla ya saa mbili na nusu wale wanaotaka kumuuliza Waziri Mkuu maswali yao wapeleke majina pale *reception* ya jengo la utawala kwa hiyo mtu anayepokea majina yale ataondoka ikifika saa mbili na nusu.

Kwa hiyo, Spika atatumia majina ambayo yaliyoletwa kwenye meza yake na ofisi na atakuwa anawaita watu kufuatana na taratibu zinazohusika kwa muda tuliokubaliana

nusu saa, ikifika nusu saa wengine watakuwa hawajatosha basi wajiridhishe pengine Alhamisi nyingine. Kwa hiyo naomba muusome ule muongozo vizuri kusudi kusiwe na mkaanganyo wa aina yoyote ile.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hivyo hatuna shughuli nyingine katika *order paper* yetu kwa hiyo naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.15 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 10 Aprili, 2008 saa tatu asubuhi)*